ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi

26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu

77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 11 Disemba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Kuweka Vifungu vya Usajili na Mambo Mengineyo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): *Bismillah Rahman Rahiim.* Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, kuhusu hotuba ya maoni ya kamati juu ya mswada wa Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matumio ya Kijamii Zanzibar na Kuweka Vifungu vya Usajili na Mambo Mengineyo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 7

Kuhamishwa kwa Kaburi la Marehemu Pili Khamis Mpera

Mhe. Ussi Yahya Haji – Aliuliza**:-**

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu yaliyofanywa na wakulima na wakwezi wa Visiwa hivi palikuwa na wajumbe kumi na nne (14) ambao ndio vinara wa Mapinduzi hayo. Kwa vile kati yao kumi na tatu (13) wameshafariki dunia, ukiondoa Jemedari Mkuu Mhe. Hayati Abeid Amani Karume ambae ni Rais wa kwanza ambaye amezikwa Afisi kuu ya CCM Kisiwandui, waliosalia wote wamezikwa maeneo ya asili yao.

a) Je, Marehemu Mhe. Pili Khamis Mpera aliyezikwa sehemu ambayo inapoteza heshima kwa kiongozi kama yeye, Serikali ina mpango gani wa kurejesha heshima ya kiongozi wetu huyo.

b) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuliondoa kaburi lile kwa heshima zote na kwa taratibu za dini yetu ya Kiislam na kulipeleka kwao Kinyasini kwa kushirikiana na Familia ya Mheshimiwa huyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 7 lenye vifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Mapinduzi matukufu ya Zanzibar yalifanywa na Wakulima na Wakwezi mnamo 12/01/1964, Majemedari 13 kati ya 14 waliongoza Mapinduzi hayo wameshafariki Dunia, tunawaombea kwa Mwenyezi Muungu roho zao azilaze mahali pema Peponi Amiin. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Muungu ampe afya njema na maisha marefu yenye kheri Mhe. Ramadhan Haji Faki ambaye ni Kiongozi pekee wa Mapinduzi hayo tulienaye hadi sasa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 7 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Marehemu Pili Khamis Mpera amezikwa katika eneo la Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui mahali ambapo sio mbali na alipozikwa Jemedari wa Mapinduzi hayo Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, kwa heshima zote za Kitaifa na kwa makubaliano na Familia yake, kama zilivyo taratibu za mazishi ambapo ni kawaida kwa familia ya Marehemu ndio yenye kusikilizwa eneo wanalotaka kuzikwa marehemu wao. Hata hivyo, ushauri wa Mhe. Ussi Yahya Haji tunaupokea.

b) Mhe. Spika, serikali haina sababu ya kulihamisha kaburi la Marehemu mzee wetu, mzee Pili Khamis Mpera, na iwapo Familia yake itafikiria kufanya uamuzi huo, basi serikali itakaa pamoja na familia hiyo ili kuona namna ya kuupokea uamuzi huo, ili kwa kadiri ya ushauri wao kuheshimu mashauri ya familia hiyo. Ahsante.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya serikali, nakubaliana na serikali kwamba kwa wakati huo Mhe. Pili Khamis Mpera alistahili kuzikwa hapo. Lakini kutokana na ushauri nilioutoa, kwa nini nimetoa ushauri huu. Kaburi lile tangu azikwe Mhe. Pili Khamis pale wakati wenzake wote 12 wamezikwa makwao, ukiondosha Jamadari Mkuu Mhe. Abeid Aman Karume.

Kaburi la Mhe. Pili Khamis Mpera hakuna anayelijua sasa, ukenda pale hata mbwa na nini wanalikojolea. Kwa hivyo, ningeomba kwa kipindi hiki ambacho serikali ikazungumza na wazee wake kuhusu kuliondosha au kuliwacha pale, serikali ikachukua juhudi ya kuliwekea alama maalum ili kaburi lile…

Mhe. Spika: Swali Mhe. Mjumbe. Uliza swali usitoe maelezo.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Je, serikali ina mpango gani wa kulihifadhi kaburi lile kabla hawajazungumza na wazee wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu kaka yangu Mzee Ussi Yahya Haji swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza napenda Mhe. Spika, na Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, waelewe kwamba Serikali hii ya Awamu ya Saba ya Mapinduzi ya Zanzibar na inayoongozwa na Dk. Ali

Mohammed Shein, itaendelea kuwaenzi waasisi wetu wa Mapinduzi na tutaendelea kuyaendeleza malengo na madhumuni ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Hiyo ndio dhamira ya mwanzo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba upo umuhimu wa kila hali kuweka kumbukumbu za viongozi wetu hawa, ambao ni Majamadari wa Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964 na serikali inachukua kila hatua. Hata ule ujenzi wa mnara wa Mapinduzi hapo Kisonge Michenzani, moja katika dhamira yake kubwa serikali ni kuweka kumbukumbu za ile kamati ya watu 14 katika mnara ule na maelezo yao kwa ufasaha. Kwa hivyo, upo kila umuhimu, kila walipolazwa viongozi wetu hawa huweka kumbukumbu ili tuweke vyema historia yao ili na vizazi vyetu vya baadae viweze kuelewa.

Kwa hivyo, serikali siku zote itachukua kila hatua ili kuhakikisha kumbukumbu za wazee wetu hawa zinawekwa vyama. Pale ambapo kumetokea makosa ya aina yoyote, basi makosa hayo yatarekebishwa ili kuweka heshima na hadhi ya viongozi hawa watukufu.

Mhe. Spika, serikali siku zote itaendelea kuwathamini viongozi hawa wote 14, akiwemo Mzee Said Washoto, Mzee Seif Bakari, Mzee Yussuf Himid, Mzee Abdalla Said Natepe, Mzee Said Iddi Bavuai, Mhe. Mohamed Abdalla Kaujore, Mhe. Khamis Daruweshi, Mhe. Pili Khamis, Mhe. Hamid Ameir, Mhe. Hafidh Suleiman, Mhe. Mohamed Mfaranyaki, Mhe. Khamis Hemed Nyuni, na Mhe. Ramadhan Haji Faki na wale wote waliotangulia mbele ya haki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa njia moja au nyengine tutaupokea ushauri wote watakaokuja nao familia na sisi tutajitahidi kuweka kumbukumbu katika mazingira mazuri, na pale penye kasoro zozote patarekebishwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu marefu sana ya serikali naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza. Kwa sababu Mhe. Waziri umekiri kuwahifadhi Mapinduzi wetu, lakini hukueleza dhamira hasa ya kuhifadhi kaburi lile la muasisi yule.

Je, ni lini serikali itatamka wazi kuliwekea vyanzo vizuri na kuonekana kaburi lile la muasisi yule, kuliko kuwekwa vile lilivyokaa hivi sasa?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza la Mhe. Mohamed Said Dimwa na naomba kumjibu kama ifuatavyo. Mhe. Spika, sote tuliokuwa hapa tuna enzi na kuheshimu sana kazi kubwa na nzuri walizofanya waasisi wetu hawa. Kuanzia hii leo serikalini tutakaa na tufikirie namna bora ya kuliimarisha zaidi kaburi lile ili kumbukumbu iwepo kuanzia sasa na siku nyingi zilizoko mbele yetu.

Nam. 10

Serikali Kuandaa Utaratibu wa Kukutana na Wananchi

Mhe. Panya Ali Abdalla (Kny: Mhe. Hidaya Ali Makame) - Aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi ndio viongozi watarajiwa katika nchi yetu, pia ndio watu ambao wanakumbana na changamoto kubwa za kimaisha. Kwa kuwa wana mambo mengi wanayoyafahamu ambayo wanaweza kusaidia katika kuendeleza nchi yetu kiuchumi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa utaratibu wa kukutana na wananchi wazalendo, wapenda amani na maendeleo ili kuweza kutoa maoni yao na changamoto mbali mbali ambazo zinaweza kusaidia kuleta maendeleo katika nchi yetu.

(b) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuweza kuandaa mbinu mbadala za kuweza kukutana na wananchi kila baada ya miezi ili kuweza kuibua mbinu mbali mbali za maendeleo katika nchi yetu.

(c) Ukiachia Kamati za Baraza la Wawakilishi, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuhakikisha inawafikia wananchi wa kawaida kwa kuandaa kama kipindi au jambo muhimu ambalo kikawaida mwananchi anaweza kufikiwa na kuweza kutoa maoni au michango au ushauri kwa maendeleo yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kwa pamoja kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, katika kutekeleza azma ya utawala bora Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka utaratibu mzuri wa Viongozi kuanzia ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa hadi Serikali Kuu ili kuwapa fursa wananchi kuwasilisha maoni na changamoto mbali mbali zinazowakabili katika maeneo yao. hatua hii, imeweza kutatua changamoto nyingi kwa haraka na kupelekea maendeleo katika maeneo husika.

Mhe. Spika, Viongozi wetu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi akiwemo Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi wanatekeleza kwa vitendo jambo hili, kwani kila mara wamekuwa wakifanya ziara katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu kwa lengo la kuhimiza maendeleo, pamoja na kutoa fursa kwa wananchi kuwasilisha maoni na changamoto zinzaowakabili katika maeneo yao kwa lengo la kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika, serikali kwa sasa haina haja ya kuandaa mbinu mbadala kwa sababu viongozi wetu wa ngazi mbali mbali, kuanzia Shehia hadi taifa, wanafanya kazi ya kukutana na wananchi na kuwatatulia changamoto zinazowakabili kwa vizuri. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza kutokana na swali mama hili. Lakini vile vile nimshukuru sana na nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana ya swali mama.

Mhe. Spika, katika miaka hii tumeshuhudia kwamba kiwango cha uzalendo cha wananchi wetu na hususan watumishi kimeshuka sana na wenzetu Tanzania Bara wameliona hilo. Juzi waliweza kuazimisha au kuzindua siku ya kuwashajihisha wazalendo. Sasa hali hiyo inawakumba vile vile

wananchi wetu wa Zanzibar kiwango cha uzalendo kimeshuka sana, kiasi ya kwamba maelendeleo yetu yanategemea sana kila mara serikali kuweza kujitutumua yenyewe.

Je, serikali yetu ina mpango gani wa kuweza kuamsha hisia za uzalendo kwa wananchi wetu kama ilivyokua wakati ule wa zamani. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe Rashid Makame Shamsi Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kwa kiasi fulani hamasa ya uzalendo imeshuka nchini mwetu, na ndio maana Mhe. Rais wetu na viongozi wake katika serikali wanahimiza sana juu ya kurudisha ari ya uzalendo nchini. Ndio maana anachukua kila hatua ya kuimarisha sana kikosi chetu cha JKU, ili vijana wetu wapite pale wazidi kupata ari na kuelewa historia yao kwa msingi wa kuimarisha uzalendo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la uzalendo ni letu sote viongozi na wananchi kwa jumla. Kwa hivyo, bado serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha kwamba tunaujenga kwa vitendo uzalendo katika nchi yetu, ili sote tuweze kujitelea kwa nchi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vinavyokuja.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hakuna jambo zuri kwa serikali au kwa kiongozi yeyote kuliko kuwa karibu na jamii na kwa kuwa changamoto zimo nyingi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, hasa katika Zanzibari hii mimi nalilia kilio cha maji katika maeneo yetu mbali mbali.

Je, Mhe. Waziri kwa kuona hilo lina haja, hawaoni Waheshimiwa Mawaziri wakaandaa vipindi maalum ili wakaweza kusikiliza maoni ya wananchi kwa kupokea simu mbali mbali ili kujua kero ziko katika maeneo gani ili kuzipatia ufumbuzi kuliko hivi tulivyo sasa hivi tuko kimya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni muhimu kuwa karibu na wananchi na nakubaliana naye Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, utaratibu wetu tuliojipangia katika serikali kwa mujibu wa sekta, kila waziri au kila kiongozi huchukua hatua za kuona namna gani atakutana na jamii ili kutatua tatizo linaloikabili sekta husika. Mhe. Rais wetu amekuwa ni mfano wa kutembelea maeneo mbali mbali nchini ili kuwa karibu ya jamii na kutatua changamoto zinazowakabili, na hivyo hivyo kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa upande wa mawaziri wanafanya kila jitihada ya kukutana na jamii. Lakini aidha, nataka nimuhakikishie Mhe. Ali Suleiman Shihata ushauri wake tutazidi kuupokea tuufanyie kazi, ili tuone ni kwa namna gani tutakuwa karibu zaidi na wananchi wetu, nia na dhamira ni kutatua matatizo yaliyopo kwa wananchi na kuwahakikishia wananchi kuwa na hali bora za maisha na maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Nam. 74

Utatuzi wa Mgogoro wa Soko la Samaki Tumbe

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwenye majumuisho yake baada ya kukamilisha ziara ya Mkoa wa Kaskazini Pemba aliagiza kufanyike ufumbuzi unaohusiana na Soko la Samaki Tumbe ili lianze kutumika mara moja.

Je, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefikia hatua gani juu ya swala la utatuzi wa mgogoro unaolihusu Soko la Samaki la Tumbe ili litumike kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu na kukidhi haja iliyokusudiwa na Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nikubali kwamba hili lilikuwa ni agizo la Mhe. Rais ambapo alitoa agizo hili wakati akifanya ziara yake katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ni jambo ambalo aliliagiza na agizo hilo Mhe. Spika, limetekelezwa kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wamefanikiwa kutatua mgogoro unaohusu soko la samaki na mboga na sasa linatumika kama ilivyokusudiwa na serikali.

Mhe. Spika, soko hili la Tumbe lilianza kutumiwa rasmi na wananchi tarehe 10/10/2017 kufuatia makubaliano yaliyofikiwa na Serikali ya Mkoa, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na wananchi wa Tumbe katika kikao kilichofanyika tarehe 2/10/2017 katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba.

Mhe. Spika, Serikali ya Mkoa ilifanya ziara rasmi kuangalia shughuli za Soko zinavyoendelea tarehe 7/11/2017 ambapo wananchi walionekana kuwemo ndani ya soko na shughuli za soko zikiendelea kama kawaida.

Mhe. Spika: Mhe. Omar Seif Abeid suala la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri kwanza namshukuru Mheshimiwa kwa majibu mazuri, kwanza nimefurahi kwa kufuata na kutekeleza agizo la Rais ni jinsi gani nimeonekana kwamba wameweza kutekeleza lile agizo alilolitoa Mhe. Rais pale. Lakini pamoja na majibu hayo nilikuwa na suali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa lile soko limeshahamiwa na bado kuna changamoto za hapa na pale ndogo ndogo zinazohitajika kutatuliwa Je, ni lini Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya itazimaliza changamoto ziliopo pale kama joto jingi liliopo ndani ya soko lile, uingiaji wa maji sehemu za kusafisha mitaro ya kutolea mabaki yanayosafishwa kwenye samaki ili soko lile liweze kutumika kwa vizuri na liwe kwenye kiwango kama kilichokusudiwa ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mheshimiwa Muwakilishi wa Jimbo la Konde kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba soko la Tumbe kwa sasa hivi limekabiliwa na changamoto kama ambavyo Mhe. Mwakilishi ameweza kufanya uchunguzi na uwezo wa kupata kufuatilia katika kubaini hilo. Lakini sambamba na changamoto hizo tukumbuke kwamba soko hili limekaa kwa muda mrefu ambalo wananchi baada ya kujengwa halikuweza kutumika kutokana na sababu mbali mbali ambazo ziliweza kujitokeza au changamoto ambazo zimejitokeza.

Kutokana na kwamba sasa agizo hili limeshafanyiwa kazi na wananchi wamesharudi katika soko lile na hizo changamoto ambazo amezisema Mhe. Mwakilishi ni za uhakika, tutahakikisha kwamba hatua zinaendelea kuchukuliwa na mpaka hivi sasa ambavyo natoa ufafanuzi tayari makisio na utaratibu wa kufanya hesabu kuona kwamba ni gharama kiasi gani ambazo zinahitajika katika kufanikisha shughuli hizo zimeshafanyika. Kwa upande ambao Taasisi zilizokuwa na dhamana ya jambo hili tutaendelea kushirikiana kuona kwamba zinatatuliwa ili kusudi kwamba soko hilo liweze kutoa huduma kama vile awali ambavyo limekusudiwa.

Nam. 15

Utaratibu wa Utoaji Talaka Mahkama ya Kadhi

Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Aliuliza:

Mara nyingi tumekuwa tukisikia matangazo katika vyombo vya habari kuwa wanaume waliowakimbia wake zao wanaitwa Mahkamani kwa ajili ya kwenda kujibu mashtaka ya wake zao. Na wasipokwenda Mahkamani, Mahkama inatoa uamuzi la upande mmoja wa mwanamke. Na uamuzi mkubwa mara nyingi unakuwa ni kupewa talaka na Mahkama.

(a) Je, Mahkama inapopokea kesi ya mwanamke yule aliyeshtaki, kabla ya kutoa hukumu inawashirikisha wazazi wa yule mwanamme ambaye hakufika Mahkamani.

(b) Baada ya Mahkama kutoa talaka, kuna masharti gani anayopewa mwanamme yule au wazee wake kuhusu kuwahudumia watoto kwa mwanamke aliyemuacha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vipengele (a) na (b) kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mahakama huwa inatoa matangazo katika redio ya wito kwa wadaiwa ambao wameshindwa kupatikana katika utaratibu wa kawaida wa kuitwa Mahakamani kwa ajili ya kusikiliza kesi zinazowakabili. Na wasipofika au kutoa taarifa za dharura zao, basi Mahakama inamsikiliza mdai peke yake na kutoa uwamuzi wa upande mmoja.

(a) Mhe. Spika, Mahakama inaposikiliza kesi ya madai ya talaka kwa mwanamke ya upande mmoja baada ya mwanamme kushindwa kufika Mahakamani, hatua muhimu inayochukuliwa ni ya usikilizaji wa ushahidi wa upande wake, ambapo pia anaweza kuwaita mashahidi ikiwa anao ili aweze kuthibitisha dai lake hilo. Na pale ambapo Mahakama itaona kuna ulazima wa kupata maelezo ya upande wa wazazi wa mwanamme haitoshindwa kufanya hivyo. Lengo lilikuwa ni kutatua mgogoro wa ndoa hiyo katika utaratibu na misingi ya kisheria.

(b) Mhe. Spika, endapo Mahakama itasikiliza kesi inayohusiana na dai la talaka na baadae kutoa maamuzi ya kutengua ndoa hiyo kwa mwanamke (mke) kupewa talaka,

- Mhakama haitokuwa na mamlaka kisheria kutoa amri au masharti yanayohusiana na huduma ikiwa wanandoa hao wamebahatika kupata watoto (mtoto).

- Hii ni kwa sababu dai la msingi lililopelekwa Mahakamani lilikuwa ni talaka, ambalo halihusiani kabisa na suala la huduma kwa watoto ambalo nalo kisheria ni dai linalojitegemea (Labda liwe ni miongoni mwa maombi (madai) ya msingi katika kesi husika).

Mhe. Spika: Mhe. Tatu Mohamed Ussi swali la nyongeza.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba Mhe. Waziri aniambie ni talaka ngapi zimeweza kutolewa katika Mahakama ya Kazi kwa mwaka huu wa 2017.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nahisi kama suali kama unaweza kulijibu Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ukweli naomba sijasikia hilo suala naomba Mhe. Tatu Mohammed Ussi arejee hilo suala.

Mhe. Spika: Ametaka kujua ni talaka ngapi zimetolewa kwa mwaka huu kwa utaratibu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa hili suala lake la nyongeza linahitaji takwimu kwa hivyo kwa heshima naomba nimwambie Mhe. Tatu Mohammed Ussi suali lake nitamjibu kwa maandishi ili apate jawabu sahihi zaidi. Nashukuru.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Miraji suala la nyongeza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala dogo tu la nyongeza lenye vipengele a na b.

Lakini kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo yanatupa imani sana katika utekelezaji, lakini katika majibu hayo kuna tuhuma pia zinazosemekana baadhi ya wanawake wanaokwenda Mahakamani wanapewa talaka hapo Mahakamani, lakini wale Mahakimu wanaotoa talaka hizo huwa wanawaoa hao wanaowapa talaka.

a. Je, Mhe. Waziri Mahakama zako zinafanya kitendo hichi na wewe unakitambua.
b. Je, huoni kama kitendo hicho kinashusha imani ya wanaume ambao wake zao wanakwenda kuwalalamikia katika Mahakama zetu hizi.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala ambalo Mhe. Miraji Khamis Mussa amelisema Ofisi yangu hailitambui hilo, sambamba na hilo kwa kuwa nimejibu suala (a) inaonekana kwamba suala (b) litakuwa limeshajibika katika suala (a) nashukuru.

Mhe. Spika: Ahsante tunaendelea Wizara inayofuata Katibu.

Nam. 5

Idadi ya Watu Katika Mkowa wa Mjini Magharibi

Mhe. Ussi Yahya Haji – Aliuliza:

Kutokana na maelezo ya vyombo vya habari vya SMZ inaelezwa kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi unakisiwa kuwa na watu zaidi ya asilimia arobaini na sita (46%) ya idadi ya watu wa Unguja na Pemba.

(a) Je, kutokana na sensa ya mwaka 2012 mpaka mwezi wa Juni 2017 kumekuwa na ongezeko la wananchi wangapi.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kwa kutoa huduma za kijamii katika Mkoa huo.

(c) Je, ifikapo mwaka 2020 Mkoa huo unatarajiwa kuwa na idadi ya watu wangapi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali namba 5 la Mheshimiwa Mwakilishi naomba kutoa maelezo ya utangulizi kuwa kwa kawaida Sensa ya Watu na Makaazi nchini hufanyika kila baada ya miaka kumi (10) na ndio inayotoa takwimu za idadi ya watu katika ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa na Taifa. Tarehe iliyofanyika Sensa ndio huchukuliwa kama kigezo cha kukadiria ongezeko la idadi ya watu ambapo Sensa ya mwaka 2012 ilifanyika tarehe 26/8/2012 na hivyo tarehe hiyo ndio rejea *Reference* ya kupimia ongezeko la watu kwa Tanzania. Kwa mujibu wa sensa hiyo, Zanzibar ilikuwa na watu 1,303,569, kati yake wanawake ni 672,892 na na wanaume ni 630,677.

Kwa kulinganisha na matokeo ya Sensa iliyotangulia ya mwaka 2002, Sensa ya mwaka 2012 ilibainisha kuwa idadi ya watu hapa Zanzibar inaongezeka kwa kasi kubwa ya asilimia 2.8 kila mwaka. Aidha, kwa kipindi hicho Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na wakaazi 584,678, sawa na asilimia 44.9 ya wakaazi wote wa Zanzibar ambapo wanawake walikuwa 301,088 na wanaume walikuwa ni 283,590.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavo:-

a. Kwa kuzingatia tarehe ya rejea ya Sensa ya Watu na Makaazi, hadi kufikia tarehe 26/8/2017 Mkoa wa Mjini Magharibi umekadiriwa kuwa na idadi ya watu 679,833 wanawake 355,150 na wanaume ni 324,683. Hii ni sawa na ongezeko la watu 95,155 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

b. Idadi ya watu na muundo wake kwa kuzingatia jinsi na umri ni kigezo cha msingi na muhimu kwa Serikali kupanga mipango yake ya kuwahudumia wananchi. Kama ilivyo kwa Mikoa mingine, kigezo hiki na vyengine vinatumika kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa kutumia mazingatio hayo, Serikali imekuwa ikiibua na kutekeleza miradi muhimu ya kuhudumia jamii ikiwemo hii ifuatayo kwa Mkoa wa Mjini Magharibi:

    - ✓ Ujenzi wa Skuli za Sekondari Mpya katika maeneo ya Bububu, Fuoni, Chumbuni, Kinuni na Mwembeshauri; Ujenzi wa Skuli za Msingi Mpya Fuoni Mambosasa na Kwarara;

    - ✓ Ujenzi wa nyumba za kisasa kupitia mradi wa ng'ambo tuitakayo,

    - ✓ Ukarabati mkubwa wa hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na kuimarisha huduma za afya katika vituo vya afya mbali mbali katika Mkoa huu kama vile kituo cha afya Fuoni.

- ✓ Kuimarisha miundombinu ya umeme inayoendana na mahitaji.

- ✓ Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama ambapo tayari imetekeleza miradi miwili mikubwa iliyofadhiliwa na Serikali ya Japan na imo katika utekelezaji wa Mradi mwengine unaofadhiliwa na Serikali ya India kupitia Benki yake ya *Exim* na pia inaandaa Mradi mwengine chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan. Miradi yote hii itakapokamilika itaondoa kabisa tatizo la maji katika Mkoa huo;

- ✓ Ujenzi wa barabara mbalimbali za Mjini na zile za kuingilia Mjini ambazo zote zimo katika Mkoa huo ikiwemo Barabara ya Mazizini – Fumba, Barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni, Barabara ya Amani – Dunga, Barabara ya Bububu – Mkokotoni na hata ya Mfenesini – Bumbwini sehemu yake imo katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

c. Mkoa wa Mjini Magharibi unakadiriwa kuwa utakuwa na wakaazi 733,914 ifikapo mwaka 2020, kati ya hao wanawake 380,324 na wanaume 353,590.

Mhe. Spika: Mhe. Ussi Yahaya Haji suala la nyongeza.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba kuulisa suala moja la nyongeza.

Je, atanisaidiaje ifikapo 2020 *Population* ya Mkoa wa Mjini Magharibi itakuwa zaidi ya nusu ya watu wa Unguja na Pemba,

a) Je, Mhe. Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum, anaungaliaje Mkoa wa Mjini Magharibi ili kuongeza majimbo ya uchaguzi.

b) Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na wataalamu wako wa Mipango unaiangaliaje Zanzibar Katika Mikoa yote mitano ili iwiane kimaendeleo ukizingatia kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi unaelemewa na watu kutoka Mikoa mbali mbali ya Unguja na Pemba, ili wasije katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Mikoa iliyosalia utaiandalia je maendeleo yao.

Mhe. Waziri wa fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba ayarejee masuala yake yote ya nyongeza sikusikia naomba awe karibu kidogo na *mic*.

Mhe. Spika: Kaa karibu na *mic* Mheshimiwa.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika tukifika 2020 Mkoa wa Mjini Magharibi utakuwa na idadi kubwa sana ya wananchi wa Unguja na Pemba.

a) Serikali Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika inaangaliaje kuongeza Majimbo ya uchaguzi katika Mkoa huu.

b) Mkoa wa Mjini Magharibi inaonekana Serikali *resource* zake nyingi wanaelemea Mkoa wa Mjini Magharibi. Je, Mikoa minne iliyosalia Serikali itatoa juhudi gani ili iwiane na juhudi zinazofanywa katika Mkoa wa Mjini Magharib ili kuondosha tatizo la wananchi kuhamia zaidi katika Mkoa wa Mjibi Magharibi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mhe. Ussi Yahya Haji kama ifuatavyo.

Suala la ukataji wa majimbo lipo kwa mujibu wa sheria na Sheria ndio inayoelekeza na kazi hiyo ipo kwenye Tume ya Uchaguzi, pale itakapoonekana kuna haja ya kukata majimbo ya uchaguzi kwa mujibu wa idadi ya watu na kwa kuzingatia vigezo vyengine Serikali itafanya hivyo.

Lakini suala jengine la nyongeza la Mheshimiwa nadhani linahusiana na msongamano labda kwa kuongezeka kwa kiasi kukubwa idadi ya watu katika Mkoa wa Mjibi Magharibi, Serikali inafanya au itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba katika Mkoa huu hakutokuwa na idadi kubwa ya wananchi nadhani hilo ndio suala lake la msingi.

Na kama nimelisikia vizuri hivi sasa Serikali ina utaratibu kupitia mipango miji ya kutengeneza miji katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, najua kabisa kutakuwa na miji midogo midogo karibu 13 katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Lengo la Serikali kuwa na miji hiyo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata sehemu nyengine ya kuishi huduma zinazohitajika katika miji zinapatikana katika maeneo hayo watakapokuwepo. Kwa mfano kwa Mkoa wa Kaskazini Mahonda ni sehemu moja inayofikiriwa lakini kwa Mkoa wa Kusini Chwaka inafikiriwa kuwa eneo la mji, Makunduchi inafikiriwa kuwa eneo la Mji ikiendelezwa miji hiyo wananchi wataweza kubaki katika maeneo hayo na kupunguza msongamano katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Lakini sambamba na hilo jitihada zinachukuliwa na Serikali za kuhakikisha maendeleo yote yanayohitajika kwa wananchi ya kiuchumi na kijamii yanapatikana katika sehemu zote za Unguja na Pemba hilo litatusaidia sana kupunguza idadi ya watu kubwa kukaa katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) swali la lanyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri na kuhakikisha kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi una watu wengi na wanazidi kuongezeka siku hadi siku, lakini pamoja na ongezeko hilo kuna Wilaya mbili Magharibi (a) na (b), Wilaya hizi Mheshimiwa ndio zenye watu wengi kuliko Wilaya ya Mjini na kwa bahati mbaya huduma za jamii bado ziko nyuma kabisa hususan narudia ile ile kilio cha maji katika maeneo yetu, lakini pia

miundombinu siku za mvua mitaro yetu inahatarisha amani na usalama wa watu wetu. Je, kwa kuwa hili ni tatizo na wizara imekiri kwamba mkoa watu umebeba watu wengi na hasa Wilaya hizi mbili Magharibi "A" na "B" wizara kwa makusudi ina mpango gani wa kuongeza nguvu au kumuongezea Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum uwezo zaidi kuendesha mipango mbali mbali ya kuweka sawa mazingira yetu ya usalama wa michirizi ya maji siku za mvua lakini pia upatikanaji wa maji katika maeneo ya majimbo yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika naomba kujibu swala la nyongeza la Mhe. Ali Sulieman Ali (Shihata) kama ifuatavyo, na kama nilivyosema katika jibu la suala mama ni kwamba Serikali ina mpango wa kutekeleza miradi mingi ya huduma za maji na hasa inalenga katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Kwa kukisia karibu dola milioni 220,000,000 zinatarajaiwa kutumika kwa ajili ya kutatua tatizo la maji hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na hiyo inasaidiwa kupitia mkopo nafuu wa Serikali ya India ambao utatoka katika *Exim Bank* ya India lakini kuna fedha zitatolewa na Serikali ya China, fedha zitatoka pia Serikali ya Japan kusaidia lakini vile vile kuna mradi ambao unatekelezwa mradi unafadhiliwa na *ADB* yote miradi hii inalenga kuondoa tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mimi ningewaomba wananchi wakazidi kustahamili wakati taratibu hizi zinakamilika ili tatizo hili liweze kufanyiwa kazi na kuondoka kabisa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na pia katika maeneo mengine ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibiwe swali langu nambari 16.

Nam. 16

Mhe. Mussa Foum Mussa (Jimbo la Kiwani) – Aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 Bodi ya Mapato Zanzibar imekadiriwa kukusanya Tsh. 347.29 bilioni sawa na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka 2017/2018 ya Tsh. 1.09 trilioni, na Mamlaka ya Mapato Tanzania imepangiwa kukusanya Tsh. 258.72 bilioni sawa na asilimia 24 ya Makadirio ya 2017/2018 ya Tsh. 1.09 trilioni.

Je, Mhe. Waziri mpaka sasa vyombo hivyo vimeshakusanya kiasi gani kwa kila kimoja.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:-

Mheshimiwa Spika**,** kabla ya kujibu swali namba 16 la Mhe. Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba Serikali imekadiria kukusanya jumla ya TZS 1.087 trilioni na bilioni 87,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2017/18 na kwamba kati ya fedha hizo, mapato ya ndani ni TZS bilioni 675.8 ambapo *ZRB* imekadiriwa kukusanya TZS bilioni 347.3 na *TRA* TZS bilioni 258.7. Kiasi kilichobakia kwa mapato ya ndani cha TZS bilioni 69.8 ambacho kilitarajiwa

kutokana na mapato ya Mawizara. Kwa upande wa mapato ya Wizara tunatarajia kukusanya TZS bilioni 48.8 na *PAYE* kwa Wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar TZS bilioni 21.0. Kwa kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka huu wa fedha 2017/2017 kwa maana kuanzia Julai hadi Novemba, makisio ilikuwa ni kukusanya jumla ya TZS bilioni 270.3 ambapo *ZRB* ilikadiriwa kukusanya TZS bilioni 159.8, *TRA* TZS bilioni 101.7, na *PAYE* TZS bilioni 8.75.

Mhe. Spika, baada aya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali na Mhe. Mussa Foum Mussa kama ifuatavyo.

Jumla ya makusanyo yote ya ndani hadi mwisho wa Novemba 2017 ni TZS bilioni 265.99, sawa na asilimia 98.4 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya makusanyo hayo, *ZRB* imekusanya TZS bilioni 154.6 sawa na asilimia 58 ya makusanyo yote na asilimia 96.7 ya lengo la miezi mitano ambalo lilikuwa kukusanya TZS bilioni 159.8. Mapato hayo yanahusisha makusanyo ya Kodi ya bilioni TZS 136.23 na mapato yasio ya Kodi ya TZS bilioni 18.57.

Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imefanikiwa kukusanya jumla ya TZS bilioni 102.44 katika kipindi hicho, sawa na asilimia 100.7 ya lengo la kukusanya TZS bilioni 101.7. Aidha, jumla ya TZS bilioni 8.75 kutokana na PAYE sawa na asilimia 100 ya lengo la kipindi hicho.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwanza napenda kuvipongeza vyombo vyetu hivi vya kukusanya mapato kwa jitihada yao kubwa ya ukusanyaji wao mzuri wa mapato.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika kwa kuwa vyombo hivi vinaendelea kukusanya mapato kwa kiwango kizuri na kwa kuwa watu wa kale walisema kwamba *mcheza pao hutunzwa* jee, Mhe. Waziri vyombo vyake hivi wafanyakazi wake una lengo gani la kuwatunza kwa vile wameendela na kazi nzuri.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mussa Foum Mussa na kwanza niungane naye kuwapongeza sana watendaji wa *ZRB* na *TRA* kwa kazi nzuri wanayoendea kuifanya ya ukusanyaji wa mapato na kwa kusema kwamba matarajio yetu kwa sababu *quarter* ya mwanzo kwa kawaida huwa hatufikii lengo na hasa kutokana na kwamba bajeti inapitishwa katika mwezi wa Julai sasa mambo mengi ndani ya mwezi wa Julai yanakuwa hayajakamilika lakini bado ameweza kufikia kiwango kikubwa sana cha ukusanyaji cha asilimia karibu nukta 97 ni hatua kubwa sana.

Na matarajia ni kwamba katika *quarter* inayokuja ambayo hii tuliyonayo sasa hivi tutaweza kufika lengo na kuziba ile nakisi tuliyoipata katika *quarter* ya kwanza, lakini nimueleze tu kwamba wafanyakazi hawa wanapongezwa na mwaka jana tuliwapongeza wafanyakazi wa *ZRB* kwa kuwa *bonus* maalum na hiyo ilitangazwa na ilitolewa ahadi na Mhe. Rais mwenyewe na utaratibu huo utakuwa unaendelea kila mwaka pale vyombo vyetu hivi vitakapofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza, lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na taasisi *ZRB* kwa kazi nzuri lakini kwa majibu yale kwa ujumla naomba Mhe. Waziri nikuulize swali kama ifuatavyo.

Kwa sababu utekelezaji huu lazima uwe na kipimo cha tathmini kilichofanyika ili kujua ule uwezo wa utekelezaji wa taasisi hii ya yale malengo ya Serikali jee hapa walipofikia kuna kipimo chochote cha Serikali cha kulitathmini au kutathmini taasisi hii ya *ZRB* kuona kuna uhalisiya na yale matarajio ya wananchi katika kukusanya kodi hizi lakini na vile vianzio tulivyonavyo ahsante mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipando: Mhe. Spika naomba kujibu swali la nyongeza Mhe. Mraji Khamis Mussa (kwanza) kama ifuatavyo.

Sina uhakika kama nimesikia vizuri lakini kama nimemsikia vizuri ni kwamba *ZRB* kwanza tujuwe kwamba lengo walilopangiwa *ZRB* katika nmwaka wa fedha 2017/2018 limeongezeka kwa asilimia 33% ya lengo lililokuwepo mwaka 2016/2017 *thirty three percent* tuliwaongezea ni kima kikubwa. Na kama ndani ya kima hicho kikubwa bado wameweza kufikia asilimia kubwa ya 97.4 ni mafanikio makubwa sana.

Kwa kila mwaka *ZRB* inajitathmini yenyewe na kuona changamoto zilizopo lakini kila mwezi pia wanajitathmini na kuna kamati ambayo iko pale wizarani inaongozwa na Katibu Mkuu kuangalia mwendezo mzima wa masuala ya makusanyo ya mapato kupitia katika vyombo vyetu viwili vya *TRA* na *ZRB* kwa hiyo tathmini hiyo ipo na ndio maana nimesemwa kwamba pamoja na *ZRB* kutofikia lengo kwa robo ya kwanza lakini bado *projection* zinatuonesha kwamba *quarter* hii ya pili tutaweza kufikia lengo lakini vile vile kulizidi kuziba nakisi ya robo ya kwanza, Mhe. Spika kama nilisikia vizuri swali lake.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kuniona kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake ya msingi ambayo yanatia moyo katika jibu lake amesema kwamba Serikali ina mpango maalum na ushapita wa kuwapa *bonus* wafanyakazi kwa kuwa kitengo hiki kinafanya kazi vizuri ya kukusanya mapato, haoni kwamba kuwe na *special bust* mbali kwa zile ahadi ya kuwaongeza *bonus* lakini aangalie mfumo mzima na jitihada wanazochukua kikweli kweli kukusanya mapato yaani kwa ufupi kwamba ipo haja ya kuongezewa hata *package* zao kusudi weweze zaidi ya kuwa na moyo wa kufanya kazi kama walivyo hivi sasa. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kama ifuatavyo. Nakubaliana nae kwamba kuna haja hiyo na hivi karibuni tukumbuke kwamba *ZRB* imefunga mkataba na Shirika la *Singapore Corporation Enterprise* na moja ya kazi ambayo Shirika lile wamekubaliana na *ZRB* ni kuangalia kwanza mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato nchini yaani kutokana na vyanzo vya ndani, na ndani yake limo suala zima na kujenga uwezo wa watendaji wetu *Capacity Building component* kwa maana ya mafunzo. Lakini la tatu pia kuangalia utendaji mzima na jinsi gani tunaweza tukawa *rised* wafanyakazi wetu hawa pale wanapofanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo, utaratibu huo upo na ndani ya mageuzi hayo ya mfumo wa ukusanyaji wa kodi nayo Serikali itayazingatia.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa ruhusa yako swali langu namba 36 lipate majibu.

Nam. 36.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Jimbo la Chumbuni) – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamiliki mali nyingi sana kwa mfano majengo, gari, mashamba n.k na ndio msimamizi mkuu wa mali za Serikali kupitia Idara ya Uhakiki Mali. Kwa muda mrefu sasa Wizara ilitoa muongozo wa kuhifadhi mali zake kwa Wizara na Taasisi za Serikali na mali hizi huhifadhiwa kwenye daftari la kumbukumbu za mali *(Fixed Asset Register).*

a) Ni kiwango *(rate)* gani kilichotolewa kwa Mawizara na Mashirika ya Serikali katika utekelezaji wa kufuata muongozo wa Wizara kwenye eneo la *Depreciation* hasa kwenye magari na vespa.

b) Zipo Wizara na Taasisi za Serikali zilizoleta maombi Wizara ya Fedha ya kuomba kuuza magari au vifaa chakavu na ni utaratibu gani unaotumika kuhakiki mali hizo mpaka kuziruhusu kuuzwa.

c) Kuna utaratibu gani wa Wizara yako kupita na kuhakiki mali za Serikali, na kama uhakiki umefanyika, mara ya mwisho ulifanyika mwaka gani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:

Mhe. Spika**,** naomba kujibu swali namba 36 la Mhe. Miraji Khamis Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, kiwango cha uchakavu kinachotumiwa kwa gari na vyombo vya maringi mawili ni asilimia 20.

b) Utaratibu unaotumika katika kuhakiki mali zinazopendekezwa kuuzwa ni kwa Wizara husika kuomba kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kufanyiwa ukaguzi na uhakiki wa mali yenyewe. Idara ya Mitaji ya Umma hufanya uhakiki na ukaguzi wa hali ya mali kwa kuangalia umuhimu wake katika eneo iliopo na athari pindi ikiondoshwa, lakini pia historia ya matengenezo na gharama zake, thamani ya kwanza ya kununuliwa na ya sasa kwenye vitabu kwa kuzingatia uchakavu kutokana na muda iliyotumika, hali halisi ya mali yenyewe, aina ya mali inayopendekezwa kuuzwa au kuondoshwa, na makisio ya thamani ya soko. Matokeo ya ukaguzi na uhakiki huo ndio yanatoa mapendekezo ya ama kubakishwa mali hiyo kwa matumizi ya Serikali au kuondoshwa na namna ya uondoshaji wa mali hiyo.

c) Mhe. Spika, kwa ujumla Serikali inamiliki mali nyingi sana. Uhakiki wa mali hizo hufanyika ama zinapotaka kuondoshwa mali hizo, kila au baada ya muda kupita au inapojitokeza haja maalum kama vile kuziorodhesha tena mali zote katika Daftari la Mali za kudumu. Kwa mfano, Wizara ya Fedha na Mipango, kupitia mradi wa Usimamizi wa Fedha za Umma

uliofadhiliwa na Serikali ya *Norway*, ilihakiki, kuthamini na kusajili katika Mfumo wa kompyuta mali za Serikali zipatazo 140,000 kupitiya Wizara tano na wizara hiyo ni Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Zoezi hilo la kuhakiki hizi wizara tano zimefanyika katika mwaka mwa fedha uliopita 2016/2017 na hivi sasa tunajiandaa na zoezi limeshaanza kwa wizara jengine katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 na zoezi hilo linaendeshwa kupitia mradi ulio chini ya wizara yaani miradi wa usimamizi wa mageuzi ya sekta ya fedha nchini.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia na ile azma nzuri ya Serikali ya kutambua mali zake na katika majibu pia nayapongeza ilipoonekana Serikali ina mali nyingi sana ambazo pengine hata nyingine hazijui.

Lakini Mhe. Waziri kuna baadhi ya Wizara ya Taasisi za Serikali pita hasa katika ukaguzi hata zile *asset aegister* za kutambua uwepo wa mali za Serikali kwa kila wizara na taasisi za Serikali hamna au hawana kabisa na ziko baadhi wanazo lakini pia katika kutizama zile *financial statement* unakuta baadhi ya yake mashirika hata kudhiainisha katika ripoti zao za kila mwaka ili kujua alau kuna thamani gani na uwezo gani wa kila taasisi haupo.

a) Je, Wizara yako kwa ujumla ina mikakati gani kwa kila wizara na taasisi ya Serikali kuwa na *asset register* linakalotuwezesha kuelewa zile mali za kudumu.

b) Kwa kuwa hizi Taasisi ambazo zinazo pia hizi *asset register* huwa hawana umiliki wa zile gari mara nyingi wanakuwa wanakwambia ziko Wizara ya Fedha kuna utaratibu gani wa pale mnapowakabidhi zile mali lakini kuwapa thamani lakini na zile *register* wa zile mali ili waweze kuwa nazo wa ukaguzi pale ambapo inahitajika, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika naomba kujibu swali la Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwanza) la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kama nilivyosema kupitia Program ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha ambayo sasa inakwenda katika awamu ya tatu zoezi la kuhakiki mali katika kila wizara litafanayika na nimesema kwamba tayari wizara tano zimekamilika katika mwaka wa fedha uliopita. Kwa mwaka huu unaendelea katika wizara zilizobakia na mara kukamilika zoezi la uhakiki basi huwa linaandaliwa *asset register*. Kwa hivyo, matarajio yetu kwamba kila wizara na kila Taasisi za Serikali itakuwa *asset register* iliyokamilika baada ya uhakiki huo.

   Lakini kwa kuongezea hapo niseme tuu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara hivi karibuni imekamilisha zoezi la kutathmini na kuhakiki maghala yote ya Serikali Unguja na Pemba na mali nyengine za majengo hiyo kazi imekamilika na ripoti yake itawasilishwa Serikalini hivi karibuni.

   Sasa hayo yanafanyika kuhakikisha kwamba *asset* zote za Serikali kwanza zinatambulika na thamani yake inajulikana na *record* kamili kupitia *asset register* zinakuwepo katika kila Taasisi. Lakini niseme zaidi kwmaba hivi karibuni tutakamilisha Sera ya Kudhibiti Mali za

Serikali ambayo inaitwa *Public Asset Management Policy* kazi hiyo imekamilika na sera hiyo itawasilishwa Serikalini hivi karibuni kwa lengo la kuhakikisha kwamba mali za Serikali popote zilipo kwanza zinajulikana, lakini pia zinakuwa *manage* vizuri, zinasimamiwa vizuri ili ziweze kuleta tija inayokusidiwa katika kuongeza kasi ya maendeleo ya uchumi katika nchi yetu.

b) Alizungumizia suala kwa nini Wizara ya Fedha haitoi umiliki wa vyombo kwa zile taasisi umiliki upo lakini kuna Idara maalum kuna mambo ambayo yanasimiamiwa kupitia Serikali kuu kwa maana ya *central contral* iko Wizara ya Fedha ni sawa sawa na wahasibu. Wahasibu wako katika kila Wizara lakini Msimamizi Mkuu wa Wahasibu wote yuko chini ya Wizara ya Fedha.

Kwa hiyo mali za Serikali zote zinasimamiwa na *central* na Wizara ya Fedha kwa umiliki kwa matumizi uko katika sekta na taasisi zote za Serikali.

Nam. 106

Uhaba wa Walimu na Ongezeko la Wanafunzi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi katika kuleta Mapinduzi ya Elimu na kwa kuboresha mfumo mzima wa elimu kuanzia msingi hadi elimu ya juu. Hata hivyo, tatizo linakuja zaidi kwa elimu ya msingi kuanzia kutoa elimu kwa walimu na ukosefu wa walimu, jambo ambalo bado mfumo wa elimu ya msingi ni tatizo na linakabiliwa na changamoto nyingi.

(a) Kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi mwaka hadi mwaka, serikali imejipanga vipi kuanza utaratibu wa kujenga skuli za ghorofa ili kupunguza wingi wa wanafunzi madarasani.

(b) Je, suala la walimu kustaafu kwa wingi na kwa wakati mmoja na uajiri ukachukua muda kuziba nafasi zilizoachwa wazi ni lini tatizo hilo litaondoka.

(c) ni kwa nini serikali huwa inajipanga kuandikisha wanafunzi wengi kila mwaka lakini hakuna kuajiriwa walimu wengi ili ya kuendana na mahitaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye vipengele (a), (b) na (c), kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Sera ya Elimu bila malipo ya Serikali ya Mapinduzi imekuwa mkombozi kwa wanafunzi wengi hasa watoto wa wakulima na wafanyakazi kuweza kupata elimu bila ya malipo katika ngazi ya elimu ya lazima. Kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya skuli na wanafunzi mwaka hadi mwaka kulingana na ongezeko la idadi ya wanafunzi. Pia, ni kweli kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi katika ngazi ya msingi kutokana na ongezeko la

idadi ya watu na kusababisha msongamano wa wanafunzi katika madarasa katika baadhi ya skuli na kupelekea skuli nyingi kufundisha kwa utaratibu wa mikono miwili na wakati mwengine baadhi ya skuli kuwa na uhaba wa walimu kwa baadhi ya masomo.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Katika kukabiliana na wingi wa wanafunzi na uchache wa ardhi, serikali kwa kuhsirikiana na wahisani mbali mbali wa ndani na nje inajenga skuli za kisasa za ghorofa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Baadhi ya skuli hizo ni Skuli ya Sekondari ya Kwarara, Skuli ya Msingi ya Fuoni Pangawe, Skuli ya Bwefoum, Skuli ya Mwembeshauri, Fuoni, Bububu, Chumbuni na Kinuni kwa Unguja na Skuli ya Muambe, Kizimbani, Micheweni na Wara kwa upande kwa Pemba. Ujenzi wa skuli hizo unaendelea hivi sasa.

Katika mwaka 2018, serikali inakusudia kuanza ujenzi wa skuli tatu za ghorofa katika maeneo ya Mwanakwerekwe na Kwarara kwa Unguja na katika eneo la Wingwi, Pemba. Aidha, katika kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, wizara itakamilisha ujenzi wa madarasa 200 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi Unguja (120) na Pemba (80). Tunaamini jitihada hizo zitapunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa nafasi katika baadhi ya skuli zetu na pia kupunguza msongamano mkubwa ulioko wa wanafunzi katika madarasa.

(b) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi, Serikalini imekuwa ikiomba nafasi za walimu waliostaafu na nafasi za kazi zinatangaziwa ili kuziba upungufu wa walimu katika baadi ya skuli. Mara tu baada ya kupokea kibali cha kustaafu kwa walimu, wizara hutayarisha maombi ya kujaza nafasi hizo ili kuziba pengo lililoachwa. Kwa mfano, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Julai, 2017 jumla ya wafanyakazi 254 walistaafu kazi, kati yao wafanyakazi 104 Unguja na 150 Pemba. Nafasi za kazi za kujaza nafasi hizo tayari zimeshatangaziwa na Tume ya Utumishi, Serikalini.

Aidha, kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 - Juni 2017, wizara ilipata kibali cha kuajiri walimu 289, kati ya walimu 223 Unguja wakiwemo Sayansi Shahada 110, Sanaa Shahada 36 na Stashahada 75 na Cheti 2. Kwa upande wa Pemba walimu 66 wameajiriwa wakiwemo walimu 41 wa Shahada ya Sayansi, 20 wa Stashahada, wa Cheti 5 na wahudumu 2.

(c) Naomba nikiri kwamba uandikishaji wa wanafunzi wapya hauendi sambamba na nafasi za kazi za walimu zinazotengwa kila mwaka kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu ambalo huwa hatulitarajii. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017, wizara ilipanga kuajiri walimu 771 na katika mwaka 2017/2018 wizara imepanga kuajiri walimu 1,140 wakiwemo walimu 390 wa Sekondari 390 na walimu 750 za maandalizi na msingi. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimsifu Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufafanuzi lakini pamoja na kwamba ametoa maelezo mengi ya

kujengwa kwa nyumba za ghorofa katika skuli nataka nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri umesema katika mwezi wa Januari mpaka Julai 2017 una ukosefu wa walimu 254, Unguja ni 104 na Pemba 150. Ninavyofahamu kwamba wanafunzi wanaendeshwa na *syllabus* na mwaka unakwenda mbio mbio.

a) Je, unajitayarisha vipi kwamba kabla ya wanafunzi wale hawajastaafu wewe tayari usha-*cover* ile nafasi ili matatizo haya ya wanafunzi ya ku-*mis* masomo yasitokee.

b) Darasa lina uwezo wa kubeba wanafunzi wangapi ambao mwalimu anaweza kusomesha, maana yake madarasa yetu sasa hivi yamekuwa kama zizi la ng'ombe wanaingizwa tu watu mia mbili na zaidi. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza yenye (a) na (b).

a) Ni kwamba sasa hivi baada ya kupata kibali kutoka Wizara ya Nchi, (OR), Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma tayari, sasa hivi tumeshatoa matangazo na mchakato unaendelea. Kufuatia mazungumzo tuliyofanya karibuni kati ya taasisi zinazohusika na ajira tunatarajia kwamba mwishoni mwa mwezi wa Disemba baadhi ya nafasi hizo zitapatikana. Kwa hivyo, tukianza kazi mwakani Januari, basi tutapata baadhi ya walimu.

b) Kuhusu uwiano baina ya mwalimu na darasa, hii inategemea ngazi. Kwa mfano, katika ngazi ya maandalizi kipimo hasa ni mwalimu mmoja wanafunzi ishirini, lakini katika ngazi za msingi na sekondari ni kati ya mwalimu mmoja na wanafunzi arubaini mpaka arubaini na tano. Hicho ndio kigezo, hatujafikia huko lakini azma ya serikali ni kuweza kufikia katika kiwango hicho. Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri alizungumzia swali zima la uboreshwaji na ujenzi wa skuli katika Mji wetu wa Zanzibar. Je, unajua kwambak una changamoto ya kujengewa skuli zisizokuwa na kiwango bora katika maeneo yetu. Kwa mfano, Skuli ya Madungu, skuli hii haijafika si zaidi ya miaka minne au mitano kufunguliwa, leo hii ile skuli imekuwa ni aibu, fedheha kwa upande wetu imekuwa inavuja kupita kiasi, imepasuka imepelekea kupoteza pesa nyingi sana za mkopo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Je, serikali inalitambua hilo.

b) Ni hatua gani zilizochukuliwa kwa mkandarasi yule aliyeitia hasara Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga skuli iliyokuwa chini ya kiwango.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaelewa kwamba kuna baadhi ya majenzi tunayojenga yako chini ya kiwango. Majengo yote tunayojenga sisi wenyewe na

mengine yanayojengwa kwa kupitia *contractors* mbali mbali nayo pia baadhi yake yako chini ya kiwango. Na kwa maana hiyo kwa mfano wa Skuli ya Madungu ambayo tumeitaja tunaielewa, tumeshaikagua mara nyingi, tumeshaifanyia tathmini na wakati wowote tutaifanyia ukarabati.

b) Kuhusu swali la hatua za kuchukuliwa. Ni kwamba katika masuala ya ujenzi ni masuala ya kisheria, na kwa maana hiyo hatua zinazopaswa kuchukuliwa ni za kisheria. Kwa bahati mbaya kwamba katika ujenzi kulikuwa na *guarantee* ya mwaka mmoja, sasa *guarantee* ya mwaka mmoja imeshapita. Kwa hivyo, kisheria ni tabu kuweza kumshtaki mtu, lakini hata hivyo tunashauriana ili kuweza kuona tunachukua hatua gani za *contractors* wote ambao walijenga chini ya kiwango. Pia na kufikiria kwamba suala hili lisitokee tena katika nchi yetu. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii kwa majibu yake mwanana ambayo ameyatoa. Lakini vile vile napenda nimuulize swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wizara yako inachukua hatua mbali mbali ya kuhakikisha inawajengea wanafunzi wetu maeneo mazuri au skuli nzuri kuweza kutoa huduma ya elimu. Je, ni vigezo gani mnavyotumia katika wizara yako kujenga skuli sehemu moja, kwa mfano kama Wingwi na baadhi ya sehemu nyengine ambazo zinajitokeza ukilinganisha na baadhi ya sehemu nyengine ama Wilaya ikawa skuli hizi hamna na bado ni kero kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kwamba wizara katika kujenga skuli kwa kweli tunatumia vigezo viwili vikubwa. Kimoja idadi ya wanafunzi waliopo katika sehemu hiyo, na kigezo cha pili haja ya kuwepo skuli hiyo. Mhe. Spika, ndio utaona mara nyingi kwa mfano katika Wilaya ya Magharibi, skuli nyingi tunazijenga huko kwa sababu kuna idadi kubwa kabisa ya wanafunzi. Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haibahatishi inakwenda kwa vigezo vyake. Ahsante sana.

Nam. 51

Ahadi ya Kupatiwa Gari Ndogo za Mizigo Wakulima wa Mwani

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali langu Nam. 51 lakini kabla ya kupata majibu naomba swali hilo nifanye marekebisho kama yafuatavyo:

Lengo lilikuwa si kununua vikeri ilikuwa ni kununua vihori. Kwa hiyo, naomba lisomeke neno vihori kila lilipokuwa linasomeka neno gari au vikeri. Naomba swali langu lijibiwe pamoja na marekebisho yake. Hivyo naomba nijibiwe pamoja na marekebisho yake.

Kwa kuwa kwenye Hotuba ya Bajeti 2016/2017, serikali ilitamka kwamba itanunua gari ndogo za mizigo hori 500 na kuwapatia wakulima wa mwani Unguja na Pemba. Jambo ambalo lilileta faraja kubwa kwa wakulima hao wa mwani kwa matumaini kwamba upatikanaji wa gari hizo utasaidia kazi za ubebaji wa mwani kwa masafa marefu kutoka kwenye maeneo husika yanayolimwa hadi sehemu za kukaushia mwani huo.

(a) Je, gari hizo zilizoahidiwa tayari zimeshanunuliwa.
(b) Kama zimeshanunuliwa, ni kiasi gani cha fedha zilitumika kununulia gari hizo.
(c) Kama hazijanunuliwa, ni lini zitanunuliwa na kugaiwa kwa wakulima wa mwani ili kukidhi lengo la serikali lililokusudiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haijatoa ahadi ya kununua gari ndogo kama alivyosema kuwapatia wakulima wa mwani wa Unguja na Pemba katika hotuba ya bajeti kwa mwaka 2016/2017. Aidha, serikali kupitia Ilani ya CCM 2015/2020 ilitoa ahadi ya kununua vihori 500 ili kuwawezesha wakulima wa mwani kubebea mwani wao kutoka maeneo ya mashamba ya mwani hadi ufukweni kwa ajili ya kuanika mwani wao baada ya kuvuna.

(b) Mhe. Spika, wizara imewasiliana na Makampuni ya kutengeneza vihori kwa ajili ya kupata vigezo (*specification*) ambapo Kampuni moja *SASL* tayari imeshawasilisha. Aidha,wizara inawasiliana na *FAO* kwa ajili ya ufadhili na utekelezaji wa agizo hilo. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa majibu mafupi ya Mhe. Naibu Waziri, mimi swali langu lilikuwa na kifungu (a), (b) na (c) wamenijibu kifungu kimoja tu ndio wamenijibu lakini sawa. Pamoja na majibu hayo waliyonijibu kwa kuwa Kampuni ya *SASL* imeshaleta *specification* na bila shaka tayari kumeshajuulikana hata na hesabu kutahitajika kiasi gani ambacho kitatumika.

a) Ni kiasi gani cha fedha kitahitajika ili kununua hivyo vihori 500 kwa ajili ya kuwapa hao wakulima wetu.

b) Je, ni lini yatakamilika mazungumzo baina ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Shirika la *FAO* ili kupata hizo fedha ambazo zitalipwa kwa hao *SASL* ili iweze kununuliwa na kukabidhiwa wakulima. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kama nilivyosema serikali kupitia ilani ya CCM ya 2015-2020 kwa hiyo baina ya miaka hii mitano basi tunategemea kulitimiza agizo hilo. Vile vile katika swali lake la (a) alitaka kujua ni gharama ngapi.

b) Mhe. Spika, mpaka tulipofanya gharama ilikuwa ni laki mbili kwa kihori kimoja, na hivi ni vihori 500, lakini kila leo ikiendelea inaweza ikazidi bei. Kwa hivyo, hata nikikupa gharama ya sasa hivi kwa baadae inaweza ikaja ikabadilika. Nashukuru sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika kazi ngumu ni kazi ya ukulima wa mwani, lakini nakumbuka katika bajeti iliyopita ambayo tunaendelea nayo imo kununua vihori 500 vya wakulima wa mwani. Lakini unasema kwamba imo katika ilani ya miaka mitano ya Chama cha Mapinduzi.

Je, tushike lipi hapa, tushike ilani ya Chama cha Mapinduzi ama tushike bajeti hii ambayo tunaendelea nayo. Na kuwachelewesha hawa huoni kwamba unawaumiza zaidi wakulima wa mwani na kazi ngumu wanayoipata.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kama unavyofahamu bajeti zetu zote hapa zinaangalia mambo matatu.

Kwanza ni *vision* 2020, ilani ya uchaguzi na *strategic plan* ya Zanzibar. Kwa hiyo, ukiona bajeti yote imetokana na utaratibu huu ndio maana serikali inapimwa katika utekelezaji wake kama je imetekeleza ilani ya uchaguzi ambayo sisi Waheshimiwa Wajumbe hapa pamoja na Rais ndio iliyotuweka madarakani. Kwa hivyo, lazima tusimamie maagizo hayo matatu ya nchi ilani ya uchaguzi ambayo ndio inatangazwa kwa wananchi, version 2020 hayo ndio maelekezo tunayofanya. Kwa hivyo, hakuna kosa lolote bajeti ya serikali kuelezea kwamba tunatekeleza ilani ya uchaguzi ni jambo sahihi kabisa.

Nam. 20

Uimarishaji wa Huduma za Uchunguzi wa Matibabu

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Katika sehemu ya malengo yake Wizara ya Afya ilijipangia kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ikiwemo kununua vifaa vya uchunguzi na mashine ya *DNA.*

Je, mashine ya *DNA* imeshanunuliwa.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wenye afya njema na wazima katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 20 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara tayari imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1 katika bajeti yake ya mwaka huu kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya *DNA* na kwa hivi sasa hatua za mawasiliano na makampuni mbali mbali yaliyothibitishwa kutengeneza mashine hizo zinaendelea kwa ajili ya ununuzi. Ahsante nakushukuru.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili la ununuzi wa mashine hii ya *DNA* limekuwa la muda mkubwa, na kwa kuwa mara nyingi inatolewa ahadi ya kununuliwa mashine hii.

Je, Mhe. Waziri atatwambia ni mwezi gani kwa kipindi hiki cha bajeti ya mwaka huu mashine hiyo itafika.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake zuri sana la nyongeza.

Naomba kwanza kabisa niseme kwamba utaratibu wa kununua mashine hii kuna utaratibu maalum sio mtu yeyote tu anaweza kwenda kununua mashine hii au haiuzwi kama shati au tai nzuri ya Mhe. Ahmada au mwengine yeyote.

Mashine hii ina utaratibu maalum ni makampuni matano tu duniani ambao wanatengeneza mashine hii, tumeshafanya uchunguzi wetu na tumefanya mawasiliano nao na ni kampuni moja ambayo ina kibali ya kuuza mashine hizi Barani Afrika. Na wakala wao wa kuuza mashine hii yuko Nairobi na kuna utaratibu maalum na vibali maalum, kwa sababu mashine hii sio kwamba inatumika katika uchunguzi tu au hapa imeandikwa matibabu, haitibu mashine hii, lakini inatumika zaidi katika uchunguzi na uchunguzi mwengine ambao inatumika mashine hii ni uchunguzi wa kiusalama zaidi, ndio maana *Police*, *Interpol* na wengine wanakuwa na vibali maalum vya kununua mashine hii.

Kwa hivyo, kwa kufuata taratibu zote hizo ambazo tunaendelea nazo kwa wataalamu wetu Mkemia wetu Mkuu ambaye ndiye atakuwa mdhibiti wa mashine hii ameshafanya mawasiliano na kampuni hiyo husika, lakini siwezi kusema lini au mwezi itategemea na hizo taratibu zitakavyoendelea.

Hapo awali mashine hii ilikuwa moja kwa moja katika eneo la sheria zaidi kupitia katika ile *reform* nzima ya sheria, haikuwa moja kwa moja kwa Wizara ya Afya, yaani vyombo vya sheria Ofisi ya *DPP* na kadhalika ndio waliokuwa wanalifuatilia suala hili zaidi kwa sababu linatumika kwenye ushahidi. Lakini baada ya muda ikaonekana kwamba ni vizuri kwa ajili ya kuchunguza vile vinasaba iwekwe Wizara ya Afya iweze kupata na uchunguzi mwengine wa kiafya, kiasili na mambo mengine yanayokwenda na hayo. Kwa hiyo, ndio maana ikaletwa Wizara ya Afya na baada ya kuletwa ndio ikawa inafuatiliwa na hatua hizi ndizo zilizofikiwa mpaka sasa hivi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona, lakini niseme tu kwanza nitambue kwamba hili suala la mashine moja katika *pioneer* alikuwa ni Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, alikuwa akipiga kelele sana kuhusu suala hili na tumpongeze sana kwa jambo hili kwamba serikali imeamua.

Mhe. Spika, kwa kuwa hizi mashine nyingi ambazo serikali inanunua na kuziweka katika *laboratory* yetu kule Mnazi Mmoja zimekuwa zinadorora na hazitumiki hasa na mapungufu yanatokana kutokana na ukosefu wa *reagent* na fedha kutokuwepo au kutokana na sheria ya manunuzi inayotumika hivi sasa.

Mhe. Spika, nitamuuliza Mhe. Waziri je, anajipangaje kuhakikisha kwamba hii mashine ya *DNA* pale ambapo serikali itanunua haitakuwa pambo kule Mnazi Mmoja na kuhakikisha hizi *reagent* zote zinapatikana ili kuweza kutimiza majukumu yake.

La pili, mashine hii inataka kutumika sana katika masuala ya kuhakikisha masuala ya udhalilishaji yanayofanyika sasa hivi na katika kampeni zote ili kuweza kupata kidhibiti na kuhakikisha kwamba wale ambao wanafanya matendo haya panapatikana *easy evidence* au udhibiti kwenda kupelekwa mahakamani au polisi.

Je, Mhe. Waziri yeye mwenyewe amejipangaje kuhakikisha kwamba haya yote ambayo pamoja na wizara nyengine kwa ujumla ataweza kusimamia yote ili hii mashine iweze kutumika ipasavyo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu maswali yake ya nyongeza mawili kama ifuatavyo.

Naomba kwanza nimwambie kuwa mashine hii haitakuwa katika *laboratory* iliyoko Mnazi Mmoja, mashine hii itakuwa katika Afisi ya Mkemia Mkuu iliyoko pale Maruhubi na pale wana jengo jipya ambalo wanajenga sasa hivi na eneo lake limeshatengwa kwa ajili ya mashine hii, itakuwa na sheria yake maalum juu ya ushahidi nani atakayeruhusiwa kutafuta *test* hizo au nani atakayeruhusiwa kuomba *test* ya namna hiyo. Mara nyingi inakuwa ni vyombo vya ushahidi polisi ama Ofisi ya *DPP* zaidi, kwa hiyo haitakuwa Mnazi Mmoja itakuwa kule na itakuwa na bajeti yake na masuala yake ya *reagent* kule kule Afisi ya Mkemia Mkuu.

La pili, katika kudhibiti imezungumzwa kudhibiti vitendo hivi vya udhalilishaji wa watoto. Mashine hii haitodhibiti ila itafanya uchunguzi, kudhibiti tutatakiwa sisi wenyewe ndio tujidhibiti. Mashine hii itafanya uchunguzi baada ya tukio kutokea itafanya uchunguzi kutafuta hivyo vinasaba ili kuweza kumjua nani aliyehusika moja kwa moja.

Mhe. Spika, na hilo naomba niseme litakuwa chini ya ile Sheria ya Ushahidi moja kwa moja na ndio maana katika Afisi ya Mkemia Mkuu katika Bodi yake, *DPP* ni mjumbe ambaye anaingia kisheria kwa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. *DPP* anaingia katika Bodi ya Mkemia Mkuu kwa sababu hiyo moja wapo na kuna vyombo vyengine vya sheria na usalama ambavyo vinaingia katika Afisi ya Mkemia Mkuu kwa sababu wao wanafanya uchunguzi sehemu mbali

mbali mpaka bandarini, *airport* na kadhalika. Sio uchunguzi wa vinasaba hivi tu vya *DNA*, lakini kwenye masuala yote ya madawa ya kulevya na mambo mengine.

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba hii mashine hii itakuwa sio ya udhibiti mashine hii itakuwa ya uchunguzi, udhibiti huko si kwetu sisi wenyewe. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 67

Utaratibu wa Kutoa Taarifa za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Mamlaka ya Udhibiti na Utafutaji wa Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ndiyo wenye wajibu wa kutoa taarifa juu ya utafiti wa awali wa Mafuta na Gesi Asilia, ambao sasa hivi unaendelea kwa hatua ya pili, ambapo hatua ya awali ilihusisha utafiti huo ukifanywa kwa kutumia ndege kwa eneo la ardhini na sasa hivi zipo meli (3) ambazo zitafanya utafiti huo baharini.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kutoa taarifa kwa jamii juu ya muendelezo wa kazi ya utafiti inayoendelea hivi sasa ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

(b) Je, ni muda gani utakaotumika kufanya utafiti huo hadi kukamilika ili kuanza rasmi.

(c) Je, gharama za utafiti huu zinagharamiwa na nani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika**,** katika utoaji wa taarifa kwa jamii, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na uchumbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ni kuwa na utaratibu maalumu wa kutoa taarifa kwa jamii juu ya suali hili la utafiti lililoendelea huko baharini. Kwanza kabisa Mamlaka ilishirikiana na Idara ya Habari Maelezo kwa kutoa taarifa kila siku kupitia Redio na Televisheni juu ya zoezi linavyoendelea na kuonesha ni maeneo gani zoezi litafanyika kwa kila siku kupitia mistari iliyochorwa kitaalamu katika utafiti huo. Hata hivyo, kwa mashirikiano ya Idara ya Habari Maelezo, tumekuwa na maonesho ya sinema pamoja na utoaji wa elimu na taarifa mbali mbali juu ya utafutaji wa mafuta kwa maeneo tofauti ya Unguja na kwa kuzingatia maeneo ambayo zoezi hilo litapita kwa kutumia mistari iliyochorwa kitaalamu.

(b) Mhe. Spika, kwa muda utakaotumika kufanya utafiti huo hadi kukamilika ili kuanza rasmi. Kwa hivi sasa zoezi la baharini limechukua muda wa mwezi mmoja katika kutafuta taarifa za kuwepo kwa miamba ya kuhifadhi mafuta na Gesi Asilia baharini, baada ya hapo itahitajika kuchukuliwa taarifa hizo na kusomwa kwa kutumia teknolojia maalumu, hatua hiyo inaweza kuchukuwa kwa kipindi cha miaka miwili (2), Baada ya

hatua hiyo, kutakuwa na hatua ya kuweka vifaa vya uchimbaji wa mafuta kwa majaribio, hatua ambayo inaweza kuchukua muda wa miaka 3. Hivyo basi, utaona kwamba zoezi lote hadi kufikia uchimbaji wenyewe linaweza kuchukua muda usiopungua miaka minane (8).

(c) Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu wa uchimbaji wa mafuta kama ilivyo katika nchi nyengine gharama za utafiti huwa zinagharamiwa na makampuni ya mafuta ambayo tunaingia nayo mikataba, hadi pale utafiti huo utakapofikia hatua ya uchimbaji na uuzaji ndipo zitakaporejeshwa gharama zote zilizotolewa na kampuni husika. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri ya kitaalamu, yenye ufafanuzi wa kina nashukuru sana kwa faida ya Wazanzibari.

Kwa kuwa utafutaji wa mafuta ni gharama kubwa na ya muda mrefu ambapo gharama zenyewe zitahitakika kulipwa hapo baadae hiyo kazi itakapokamilika. Mwenyezi Mungu atujaalie yawepo ili tuweze kurejesha hiyo gharama. Je, kwa upande wetu kuna mtu yeyote anayeiwakilisha serikali wakati wa matumizi wa hizo gharama zinapoendelea. Kwa sababu gharama zinafanyika na zinatumika. Je, sisi tuna mwakilishi yeyote anayewakilisha serikali ili kujua gharama halisi zinazotumika na ili kuja kuepusha kutofahamiana kutafautisha baina ya gharama halisi iliyotumika na itakayosemwa na hao wenye makampuni ambao wanafanya kazi hiyo hivi sasa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kwamba ndio kuna utaratibu maalum ambao wanasaidia kujua gharama halisi mpaka hatua itakapofikia. Ahsante sana.

Nam. 4

Matumizi ya Nyumba ya Living Stone

Mhe. Ussi Yahya Haji - Aliuliza:

Ni muhimu kwa nchi yoyote duniani kuweka historia ya mambo mbali mbali yaliyotokea katika nchi husika. Hapa Zanzibar, ipo historia muhimu ya Living Stone Mmishionari aliyefika Zanzibar mnamo miaka ya 1851 – 1874, aliyepewa nyumba ya kuishi hapo Kinazini karibu na msikiti Mabuluu kwa miaka kadhaa, nyumba hiyo inajulikana nyumba ya Dr. Living Stone.

(a) Je, serikali imebadilisha matumizi ya nyumba hiyo.

(b) Kwa vile maelezo ya mvumbuzi huyo ni muhimu hususan kwa kukuza utalii wa Zanzibar. Je, maelezo yake pamoja na vifaa alivyokuwa akitumia vinapatikana wapi.

(c) Je, lile bango mbele ya nyumba ile lililokuwa limeandikwa *"LIVING STONE HOUSE"* na lenye kuashiria uwepo wa nyumba ile liko wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika. kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena niipongeze Timu ya *Zanzibar Heroes* kwa hatua ambayo imefikia, lakini pia naomba bado niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi tuiombee dua timu yetu katika mchezo wake wa leo pia ifaulu.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli serikali imebadilisha matumizi ya nyumba hiyo ya Dr. Living Stone baada ya jengo hilo kupewa Jumuiya ya Wafanyabiashara *(Chamber of Commerce)* na kutumika kwa mambo ya biashara. Kabla ya kupewa *Chamber of Commerce* jengo hilo Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar kwa wakati ule ilikusudia kutumia kama makumbusho ya wavumbuzi, lakini wakati tumo katika matayarisho hayo tulipata habari ya jengo hilo kupewa Jumuiya ya Wafanyabiashara *(Chamber of Commerce)* na ndio ulikuwa mwisho wa mpango huo.

(b) Mhe. Spika, baadhi ya vifaa vipo Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar katika Makumbusho yetu za Mnazi Mmoja, *Palace* na *Beit el Ajaib*.

(c) Walipokabidhiwa jengo hili Jumuiya ya Wafanyabiashara *(Chamber of Commerce)* na lile bango lilikuwepo, lakini kwa masikitiko makubwa tu, nakiri kwa kutokwepo bango hilo katika eneo lile na kupunguza kasi ya kuutangaza utalii wetu na historia ya jengo lile. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri katika swali langu hili nina maswali yafuatayo ya nyongeza.

Mhe. Spika, tunaelewa kwamba utalii ni muhimu sana katika nchi yetu ukiondosha karafuu na utalii tunautegemea, kwani utalii unatupatia asilimia 70 ya *foreign currency*, asilimia 38 ya mapato yetu ya ndani. Uamuzi wa wizara hii kuitoa nyumba ile kuiondosha katika kumbukumbu za historia mimi zinanitia mashaka. Kwa sababu hata lile bango la *Living Stone House* limeng'olewa kwa makusudi kuondoshwa, sioni sababu kuwa nyumba hii isitumike kama makumbusho ya Living Stone ambaye alikuja hapa Zanzibar katika miaka ya 1851 akaishi pale pamoja na wavumbuzi wengine. Ningelishukuru sana kwamba jengo hili ikakubaliwa Idara ya Makumbusho na Nyaraka kurejeshwa na kuwa jengo la historia. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ni ushauri, naona hamna swali hapo pana ushauri. Nilikuona Mhe. Hamza Hassan Juma kwa swali la nyongeza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikauliza swali dogo la nyongeza.

a) Mhe. Spika, kwanza na mimi nina masikitiko yangu kidogo kuhusu suala la kubadilishwa kwa matumizi kwa hili jengo la Living Stone. Kama unavyofahamu Mhe. Spika, nchi yetu inategemea zaidi mapato yake kupitia utalii na historia ya *Living Stone* dunia nzima inajulikana. Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nauliza hivi,

b) Je, hili jengo la *living stone* kwa sasa hivi bado wamemilikishwa hao *Chamber of Commerce* au bado liko Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Je, hatuoni kwamba jengo hili kuliondoa kwenye makumbusho hatuoni kwamba tunafuta ile historia aliyoiweka Dr. Living Stone kwa upande wa Zanzibar.

(c) Je, hatuoni kwamba nchi yetu badala ya kwamba kuimarisha utalii kwa kutangaza vivutio vyake ikiwemo nyumba kama hizi, leo kuziondoa nyumba hizi za kumbukumbu hatuoni kwamba utalii wetu baada ya kuupeleka mbele tunaurejesha nyuma.

Mhe. Spika: Mheshimiwa jibu (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ahsante sana, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) yote kwa pamoja kama.

(a) Mhe. Spika, jengo lile kama nilivyosema bado wanalo *Zanzibar Chamber of Commerce*. Jengo lile bado wanaendelea kulitumia kwa kufanya biashara zao.

(b) Mhe. Spika, ni kwamba jengo lile kwa kupewa *Zanzibar Chamber of Commerce* utalii wetu na historia ya nchi hii ni kati ya njia moja ya kupotea kwa historia. Lakini namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutasimamia kwa nguvu zote ili tuone jengo lile limerudi mikononi mwetu, lakini pia na historia ya sehemu ile ya Living Stone kwamba bado inarejea na wageni wakija ili tuutangaze utalii wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya Mhe. Hamza Hassan Juma kama ifuatavyo.

Mheshimiwa jengo la *Living Stone House* litaendelea kuwa jengo la kumbukumbu ya kihistoria katika nchi yetu kutokana na historia yake. Wenzetu wa *Chamber of Commerce* wameazimwa kutumia tu, lakini si kubadili kwa aina yoyote kumbukumbu ile na historia yake. Kwa hivyo, watu wa *Chamber*, wafanyabiashara wamepata ofisi pale ya kufanyia shughuli zao wamepewa na serikali mpaka hapo watakapopata jengo lao. Lakini bado jengo lile litaendelea kuwa ni moja katika kumbukumbu muhimu ya historia ya nchi yetu na halitofanyiwa mabadiliko yoyote zaidi ya kuendeleza historia hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha na tuna wizara moja bado haijajibu maswali, lakini tatizo kubwa ni saa iliyokuwa ikiniongoza naona inaniambia bado

dakika kumi wakati muda ulikuwa umeshakwisha. Nimejaribu ku-*cross-check* saa zangu nyengine naona ile ndio ina matatizo. Kwa hiyo, muda wa maswali umekwisha.

Baada ya hapo naomba kwanza nimkaribishe Mhe. Naibu Spika, aje achukue kiti halafu mambo mengine yaweze kuendelea. Mhe. Naibu Spika, karibu.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Naam! Mhe. Nassor Salim Ali.

HOJA ZA DHARURA

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, naomba kutumia Kanuni ya 42(1) ambayo inazungumzia hoja ya kujadili jambo la dharura.

Mhe. Naibu Spika, Timu yetu ya Taifa *Zanzibar Heroes* ambayo iko katika mashindano ya *Challenge CUP* kule nchini Kenya na imekuwa ikiendelea vizuri toka kuanza kwa mashindano haya. Lakini Mhe. Naibu Spika, timu yetu mbali na changamoto inayozipata lakini mbali kuna changamoto ambayo wanazipata, lakini mbali kuna changamoto nyengine ambayo inaikabili. Kwa hivyo, ningeomba kumuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo basi kutueleza jambo fulani katika maandalizi yaliyo bora zaidi ili timu yetu iendelee kufanya vizuri katika mashindano haya yanayoendelea. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MUONGOZO

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Naibu Spika, nasimama kuhusu Kanuni ya 63, lakini nasimamia 43. Kiongozi wa Shughuli za Serikali au Waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo Serikali inajibika na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati 43 kama inavyojieleza.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua Majeshi wa Tanzania wapo katika kuilinda nchi na kutekeleza wajibu wao waliotumwa na nchi lakini kuna wengine wamefariki.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa nilikuwa naomba kujua kauli ya serikali ni Watanzania wangapi waliofariki katika hao, ni Wazanzibari wangapi waliofariki na mustakabali wao wanaletwa lini na kutakuwaje katika masuala yote ya mazishi yao, hilo moja.

Pili, naomba Baraza lako tukufu lisimame kwa muda wa dakika 3 kuwaomboleza na kuwaombea dua ndugu zetu waliofariki.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa ambao mmekuja na hoja za dharura wote wawili mimi nafikiri ni jambo muhimu sana kuzitoa hizo hoja za dharura. Vile vile nimepata muongozo hapa kidogo kwamba lilikuwa suala moja limebakia na nimuombe Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutuongezea muda kwa ajili ya kumaliza masuala hayo. Na kwa kuwa

leo kutakuwa na Mswada ambao tunatarajia sana kwamba tutakwenda nao jioni kwa hiyo tuna muda mkubwa.

Lakini haya ambao mawili yamezungumzwa kwa kuwa ni mambo muhimu sana na masuala ambayo kila mmoja anataka tuyazungumze ndani ya Baraza la Wawakilishi, ningeomba tumalize hilo suala moja halafu tuje tuyazungumze kwa umakini mkubwa ndani ya kikao chetu. (*Makofi*)

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili naomba utuongezee muda mdogo kwa ajili ya kumaliza masuala ili tuendelee na shughuli nyengine, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kama maelekezo yako umuhimu wa suala lililobakia. Kwa hiyo, naomba tuweke kando muda wa maswali ili tuweze kulimaliza suala lililo mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja iliyotolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa nakushukuru, Katibu.

Nam. 42

Mkanjuni Kivumoni

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Serikali kupitia mradi wa *MIVARF* ilizijenga barabara nyingi za vijijini kwa kiwango cha kifusi kwa ajili ya kuwarahisishia wakulima na wavuvi kuweza kufikisha bidhaa zao masokoni. Na kwa kuwa miongoni mwa barabara zimeshaanza kuharibika kutokana na mvua za Masika zilizopita ambazo miongoni mwa barabara hizo ni barabara ya Mkanjuni/Kivumoni na Makongeni/Kinazini, Shehia ya Mtambwe Kusini, pamoja na barabara nyingine ambazo zilizokuwemo kwenye mradi huo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kutokuzifanyia matengenezo sehemu zilizoharibika na kuziwekea misingi ya kupitishia maji barabara hizo kutasababisha kuharibika zaidi kwa barabara hizo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongezea kiasi kinachohitajika ili kuzifanyia matengenezo barabara hizo na kuepuka gharama kubwa zaidi ya kuja kuanza kuzijenga tena pindipo zikiharibika zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vipengele (a) na (b) kwa naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid kwanza napenda kutoa ufafanuzi mfupi kama ifuatavyo:

Ujenzi wa barabara kupitia mradi wa *MIVARF* uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) uliratibiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo, Misitu na Uvuvi ambao ndio wasimamizi wakuu wa mradi huo. Baada ya kukamilika kwa mradi huo, Wizara hiyo iliomba kuzikabidhi barabara hizo zenye refu wa kilomita 149.5 (Unguja kilomita 69.1 na Pemba kilomita 80.4) kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, na hivi sasa taratibu za makabidhiano ya barabara hizo zinaendelea kufikia hatua ya mwisho.

Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Baada ya kukamilika kwa taratibu za makabidhiano hayo, Wizara yangu tazipitia barabara zote ili kubaini aina ya matengenezo yatakayohitajika pamoja na kufanya tathmini ya gharama za matengenezo husika ya barabara hizo na utekelezaji matengenezo hayo yatafanywa kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Serikali itaweka mpango maalum wa kuzifanyia matengenezo hatua kwa hatua kadri fedha zitakapo patikana ili kudhibiti barabara hizo zisiathirike zaidi kwa lengo la kuepusha gharama kubwa za matengenezo hapo baadae. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nilikuwa na suala dogo tu la kumuuliza wakati tunasubiri hayo makabidhiano yenu ya kiwizara lakini mvua zinanyesha na barabara zinaharibika hatuna ahadi na Mungu lini zitakuja mvua.

Sasa wakati tunasubiri hayo makabidhiano yenu nyinyi ni utaratibu gani mtakaochukuwa wa kuzilinda zile barabara ili huo wakati wa kukabidhiwa ziwe hazijamalizika kuharibika hasa ukitilia manani ile barabara ya kutoka Makongeni hadi Kinazini haipitiki tena sasa hivi. Bara imekuwa mbovu, imekufa na itamalizika wakati wa mvua zivyoendelea lini utakwenda kuzikagua na kuziangalia na kuzifanyia marekebisho japo ya dharura. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji nachukuwa nafasi hii ili kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunazijua hizo barabara ni muhimi na ziko sehemu baadhi ya barabara hizo zimeharibika hasa hizi barabara ambazo zinapitiwa na mabonde ya maji.

Lakini nataka kumtoa wasi wasi kwamba sisi hivi sasa tuna utaratibu kila barabara inapokuwa katika athari basi kupitia kifungu chetu kile cha matengenezo ya dharura au matengenezo ya kawaida huwa tunazifanyia matengenezo na mfano vile vile barabara ya Mkanyageni-Kangani hii tayari katika bajeti yetu ya safari hii ambayo ni barabara *MIVARF* tutaitia lami ili tuinusuru ile barabara na tuendelee kuitumia kwa muda mrefu zaidi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa. Mheshimiwa mimi nina maswali yangu mawili.

(1) Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mhe. Waziri alituahidi kwa wananchi waliopata kung'olewa mazao yao hasa katika maeneo mbali mbali yaliyopita barabara hiyo kuwa watawapa fidia. Lakini mpaka leo bado fidia yao hawajaipata. Sasa nataka atwambie ni lini wananchi hawa watapata fedha kwa ajili ya fidia ya mazao yao ilipopita barabara.

(2) Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 alitueleza kuwa maeneo ambayo yanapita maji na hakuna madaraja watahakikisha kuwa mwaka huu wanayatengeneza. Lakini mpaka leo kuna maeneo ya Dongongwe na Kizimbani hayapitiki kabisa kwa sababu ni njia za maji.

Sasa nataka Mhe. Waziri atwambie ni lini maeneo hayo yatapata kujengwa madaraja ili wananchi wapate kupita kwa utulivu zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunayajua hayo masuala na sisi tumesema kwamba kwa wale wote ambao wanastahiki kupata fidia za vipando hata na nyumba basi tutahakikisha zile fidia tunazilipa, na katika bajeti ya mwaka huu tutahakikisha kwamba tunaanza kulipa kila sehemu si Unguja tu hata Pemba ambazo tayari tumeweka baadhi ya fedha kushughulikia suala hilo.

Suala lake kwamba lini tutazifanyia ukarabati. Kama nilivyosema sisi kwa mujibu wa hali halisi ya fedha kila tunapopata fedha basi barabara zile ambazo ziko katika hali mbaya tunazifanyia matengenezo ya kawaida na ya dharura ili kuhakikisha kwamba zinapitka wakati wowote. Mimi namuahidi kwamba kwa hivi sasa tunajipanga ili kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo zimeharibika tunazifanyia ukarabati. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, mimi nimuulize kwa haraka haraka tu.

(a) Mhe. Waziri hii barabara ya *round about* ya Michenzani kwenda Rahaleo ni ya Mawasiliano au ya Tawala za Mikoa.

(b) Lakini kama ni Mawasiliano, ni lini barabara hii itatengenezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said suala lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Bara zote kuu ni barabara ambazo zipo chini wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kutoa ahadi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba mara tu mvua hizi zitakapokwisha, basi barabara ile pamoja na Saateni na barabara nyengine korofi tutazijenga tu. Na tayari lami tani 50 imeshafika tunasubiri mvua zimalizike kwa sababu hatutaki tupate hasara tena. Hii nachukua ahadi ndani ya Baraza lako la Wawakilishi *inshaallah* Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Nam. 56

Deni la Ununuzi wa Vifaa vya Shirika la Bandari

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Shirika la Bandari limelipa Shilingi 5,634,508,998/= kati ya Shilingi 11,035,176,377.33 ambazo zimehitajika kwa ununuzi kwa vifaa vya kazi Bandarini, na kwa sababu bado Shirika la Bandari linadaiwa jumla ya Shilingi 5,400,667,379.33 ambazo linahitajika kulipa kwa kampuni iliyouza vifaa hivyo.

(a) Je, Shirika la Bandari lilinunua vifaa hivyo kutoka kampuni gani.

(b) Je, ni muda gani wa mkataba ambapo Shirika la Bandari linatakiwa kukamilisha malipo yaliyobaki ili iweze kupatiwa vifaa vyake vilivyobakia.

(c) Je, Shirika la Bandari lina uwezo wa kulipa deni linalodaiwa kwa wakati ambao unatajwa kwenye mkataba wa mauziano hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 56 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Bandari lilinunua vifaa vya kufanyia kazi bandarini katika mwaka 2015/2016 kutoka Kampuni mbalimbali za nje ya nchi, vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na *Reach Stackers 2* kutoka Kampuni ya *EFFCO* ambaye ni wakala wa *CVS Ferrari* ya Italy**,** *Krini 2* kutoka Kampuni ya *LIEBHERR ya* Ujerumani**,** *Fork Lifts 3* na *Empty Contaner Handler 1* kutoka Kampuni ya *LINDE ya* Ujerumani, vile vile tulinunua *Terminal Tractors 2,* na *Terminal Trailers 2* kutoka Kampuni ya *MOLFINCO* ya Belgium**.**

(b) Shirika la Bandari tayari limekwishakamilisha malipo yote ya jumla ya Tshs.11,035,176,377.33 kwa Kampuni hizo baada ya kupokea vifaa hivyo kwa mujibu wa mikataba ya ununuzi na hivi sasa Shirika halina deni lolote kwa Kampuni hizo.

(c) Napenda nimuarifu Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Shirika la Bandari linauwezo wa kulipa deni linalokopa kutoka taasisi yoyote kwa mujibu wa mikataba waliyokubaliana. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri kutokana na majibu yake yenye taarifa nzuri za kupendeza. Ahsante.

Mimi nachukuwa nafasi hii kuwapongeza Shirika la Bandari kwa kumaliza deni ambalo walinunua hivyo vifaa. Lakini sambamba na ununuzi wa vitendea kazi hivyo ambavyo tayari wameshavipata wameshavinunua na wamelipa madeni yao yote.

Lakini pia kulikuwa na mchakato wa kuwaajiri wafanyakazi ambapo vifaa vimepatikana pia panahitaji wafanyakazi. Ukitilia mbali kwamba kulikuwa na watu waliokuwa wakilipwa pale Bandarini kama *daily paid* wengine wamefanyakazi kwa muda wa miaka 15. Sasa ili kukidhi mahitaji wa kisheria ya Utumishi wa Umma. Je, ni lini Shirika la Bandari litawaajiri wale wafanyakazi ambao walikuwa wanafanyakazi pale kwa muda mrefu wengine hadi miaka 15 ili kuboresha utendaji wa kazi katika bandari hiyo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli wako wafanyakazi walikuwa muda mrefu pale lakini hivi sasa tumeshaanza utaratibu wa kuwalipa kwanza wale wote ambao wa kukaa muda mrefu kuanzia miaka 51 mpaka kwenda mbele na ambao hivi sasa tunaendelea kuwalipa na baada ya kuwalipa hao sasa wakati wowote tutatangaza nafasi kwa wafanyakazi wengine na vile vile na wale waliokuwepo tutaangalia utaratibu namna gani kwa mujibu wa *CV* zao tuwaajiri sehemu zinazohusika. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo tu la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Lakini nimpongeze sana na niipongeze taasisi hii ya bandari kwa kukamilisha deni hili.

Lakini mara zote Mhe. Waziri kwenye malipo ambayo tunawalipa Taasisi za nje kuna malipo ya kodi mbili yanalazimika kukatwa katika fedha zile tunawalipa hawa ambao tunawapa kazi ndani ya serikali yetu, kodi ya *VAT* lakini zuio ya asilimia mia mbili.

Je, Mhe. Waziri katika malipo haya yaliyoulizwa katika suala la msingi ni kodi ya kiasi gani tuliipata kama serikali katika *VAT*.

Lakini pia na ni kodi ya kiasi gani la zuio la asilimia mbili ambalo tulilipata katika mikataba hii ambayo ilijumuisha kulipa madeni haya. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake kama ifuatavyo.

Kwanza jambo la kupendeza kwamba mikopo hii yote tuliyoichukua tumechukua kupitia *People's Bank*, Benki yetu hapa Zanzibar. Kwa hiyo, taratibu zote zinafanyika kwa mujibu wa kupitia taratibu za *banking*. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 105

Matumizi na Ulinzi wa Eneo la Hifadhi ya Barabara

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi katika kuendeleza miundombinu ya barabara na makaazi ya raia. Lakini barabara huwa ina vipimo vya upana wa eneo lake la hifadhi na katika eneo la makaazi ya watu, Wizara ndio wahusika wa kuwapimia viwanja wananchi na mpimaji huyo anafahamu umuhimu wa barabara. Hata hivyo, wakati wa upanuzi wa barabara wananchi hudai haki zao kwa kuvunjiwa nyumba zao kwa vile ana hati na "site plan",jambo ambalo hupelekea Serikali kutumia fedha nyingi za kujenga barabara kwa kulipa nyumba za watu na pia kuingia migogoro na wananchi.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambayo wakati mwengine ndio chanzo cha migogoro hiyo.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kusimamisha ujenzi wowote wa nyumba zilizo barabarani kwa kipimo cha barabara.

(c) Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi kwa yeyote anaejenga katika eneo la hifadhi ya barabara kwa hatolipwa kwani anaingizia hasara Serikali kwa jambo la makusudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye vifungu (a), (b) na **(**c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali siku zote imekuwa ikiendelea kuhakikisha kuwa wizara husika inaendelea kutatua migogoro inayoikabili sekta ya ardhi kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

(b) Wizara yangu ilishaanza kuweka viguzo kwenye mipaka ya hifadhi ya barabara kwa baadhi ya barabara na pia imepanga mikakati ya kuweka alama kwa kutumia rangi kwenye maeneo ya mipaka ya barabara zote nchini wakati ikitafuta fedha ya kuwekea viguzo vya kudumu kwenye maeneo hayo yatakayowekewa alama.

(c) Mara kwa mara serikali imekuwa ikitoa tamko kupitia vyombo vya habari kwa kuwaelimisha wananchi kutojenga au kupanda vipando kwenye maeneo ya hifadhi

ya barabara. Aidha wizara yangu huchukua hatua tafauti kwa kuhakikisha kwamba inawaandikia barua watu wote wanaojenga majengo yao ndani ya eneo la hifadhi ya barabara na kutaka kuvunja majengo yao hata hivyo baadhi yao hukaidi na kuendelea na ujenzi huo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali la nyongeza nimuulize Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa tunaona katika maeneo ya tuseme kama Tanzania Bara kwamba sasa hivi majengo makubwa yanavyujwa kwa ajili ya barabara na matatizo mengine ambayo yalijengwa kimakosa na sisi hapa tunaweza kuja kufikia pahala tukaja tukatiana hasara kutokana na matatizo kama hayo.

Je, kwa kusaidia wananchi na serikali yao hatuoni umuhimu wa kuweka mabango katika barabara ya kuweza kuelekeza kwamba kaa mbali na barabara katika kima fulani angalau pale iweze kuonekana kama kuna umuhimu wake. Lakini ni lini utatafuta fedha za kuweza kuzipima barabara za Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri wake tutauchukua na tutaufanyia kazi kwani unaonesha kwamba utatusaidia sana katika kuzihifadhi barabara zetu.

(b) Kama nilivyosema kwamba wakati wowote tutakapopata fedha basi tutahakikisha kwamba zile hatua tunazichukuwa pamoja na kuweka viguzo na alama stahiki ili watu wajue kama zile ni barabara zetu na hawaruhusiwi kujenga.

Lakini hata hivyo naweza kumwambia kwamba mfano mzuri barabara ya Mwanakwerekwe. Kwa mujibu wa ile sheria yetu iliyofanyiwa marekebisho ya mwaka 2012 wale wote waliojenga baada ya kupitishwa ile sheria tuliwabomolea na hatukuwalipa fidia. Kupitia Tawala za Mikoa tumekuwa wakati wote Wakuu wa Mikoa wakitoa tahadhari na indhari na sisi tumewahimiza Masheha wahakikishe kwamba wanafuata vigezo vyote, ili mwananchi anapopewa ruhusa ya kujenga basi anafuata taratibu husika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuchukua ahadi kwamba atakikamilisha kipande kile cha barabara ya Michenzani eneo la Mnara wa Makumbusho. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu hayo naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kama utakumbuka hivi karibuni tu tulipata maafa ya mvua barabara nyingi zilibomoka hususan kule Pemba ikiwemo barabara ya Mkoani. Lakini wafanyakazi wale walifanya kazi masaa 24 nathubutu kusema hivyo ambapo kuna pesa za *overtime* walitakiwa wapewe mpaka leo hii hawajapewa. Pia kuna pesa za miezi sita hawajapewa hadi hivi sasa wafanyakazi wale wanalalamika. Je, Mhe. Naibu Waziri, Wizara wanalijua hili.

Kama wanalijua ni hatua gani za makusudi mtachukua ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale pesa zile wanapewa na huyu aliyekabidhiwa pesa hizi kuwapa anawapa kwa wakati na waache kunung'unika. Ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa utulivu wapate pesa zao. Mhe. Waziri naomba majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Ziwani swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukiri kusema kweli wapo baadhi ya wafanyakazi wanaotudai na hii ilitokana na kwamba ilitokea hali ya dharura na ile kazi ilitakiwa ifanywe kwa haraka ikabidi tupeleke pesa ya dharura. Lakini hatua kwa hatua tumeshaanza kuwalipa na wapo wengine ambao wanadai pia barabara za Mgelema, Kipapo na Ole mpaka Kengeja wao wote wale tumeshaanza kuwapelekea pesa zao. Mara tu pesa zinapoingia mimi nitahakikisha kwamba wanalipwa kwa mujibu wa kazi waliyoifanya.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza naomba niwatangaze wageni wetu waliohudhuria leo hii katika ukumbi wetu, nao ni wageni wa Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud, Mwakilishi wa Jimbo la Bububu. Wageni hawa ni kutoka Jimbo la Bububu, Tawi la CCM Dole. Wageni wenyewe ni Ndg. Hamdu Juma Majengo ambaye ni Sheha, tunaomba utupungie mkono Mhe. Sheha, ahsante. Ndg. Kassim Abass Hussein anayetoka Tawi la Dole ni Katibu wa CCM, ahsante tunakushukuru. Ndg. Ali Humoud Mohammed, Mjumbe wa Sheha, halafu Ndg. Salama Mathias Masanja, yeye ni Mwenyekiti wa UWT Tawi la Dole. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe muda mfupi uliopita Wajumbe wawili walileta hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 42.

Lakini Kanuni hiyo hiyo ya 42 (7) inatwambia kwamba hatuwezi kujadili hoja mbili katika kikao kimoja. Lakini sasa, Kanuni ya 147 inaturuhusu kutengua Kanuni ya 42 (7) kutokana na umuhimu wa hoja zilizoletwa mbele yetu. Kwa maana hiyo, nachukua fursa hii kutengua Kanuni ya 42 (7) ili hoja mbili zote ziweze kujadiliwa. Hoja hizi ambayo moja ameleta Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni ataitoa kama mpangilio wa hoja zenyewe zilivyokuja ataanza na hoja hiyo. Halafu baadae itakuja hoja ambayo ameileta Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Kwa hiyo, waheshimiwa wengine tayari wameshaanza hapa kuleta maombi ya kujadili hoja hiyo. Kwa hiyo, nao nitawapa nafasi lakini sitozidi zaidi ya watu watatu katika kila hoja. Natoa nafasi ya muda mfupi sana na nimetoa nafasi hiyo kwa umuhimu wa hoja hizo. Sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA 147

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya Kanuni inabidi ulihoji Baraza lako ili likubali kutengua hiyo Kanuni ya 42 (7) na kanuni ya 147 (1) iweze kufanya kazi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ahsante nakushukuru. Sasa nahoji Baraza ili tuweze kutengua kanuni ya 147.Wale wanaokubaliana na kutengua kanuni hiyo wanyooshe mikono, nashukuru wote.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe.Naibu Spika: Waheshimiwa sasa tunaendelea na taarifa kutoka kwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia kuwa na furaha kubwa sana ndani ya siku yetu hii ya leo. Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Nassor Salim Ali kwa kutoa hoja inayohusiana na timu yetu ya *Zanzibar Heroes* ambayo ipo kule Kenya inatuwakilisha hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo ilikuwa nataka nitoe rambirambi za dhati kwa aliyekuwa Mbunge wa Korogwe na aliyekuwa mwanamichezo mashuhuri Ndg. Joel Bendera ambaye amefariki dunia na natumaini jana amezikwa. Tunatoa rambirambi zetu za dhati na natumai utakapofika wakati wa ile hoja ya pili, basi tutakaposimama tutasimama na kwa niaba yake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, sasa naomba nitoe pongezi zangu za dhati kama ilivyotolewa hoja na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa mnamo tarehe 30 timu yetu ya taifa ilikwenda kushiriki vita dhidi ya mashindano haya ya *CECAFA.* Nashukuru sana kwamba timu yetu imefika salama imeweza kukaa pale na wachezaji wetu salama, pamoja na viongozi wamefika salama na hatimaye wameweza kushiriki mashindano yote mechi tatu zilizopita hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, katika ushiriki wao timu yetu ilikuwa na mambo makuu mawili. Suala la kwanza utii wa nidhamu. Napenda kuipongeza sana timu yetu kwa kuondoka na nidhamu ya kuelewa kwamba Zanzibar ni nchi yenye ukarimu wa aina yake, lakini ni nchi yenye amani, utulivu na usalama mkubwa jambo ambalo wamelitumia katika wakati wao wote wa michezo.
Vile vile Mhe. Naibu Spika, timu yetu iliondoka hapa ikajua kwamba imebeba dhima kubwa ya Wazanzibari, imebeba nyoyo za Wazanzibari na imebeba hamasa za Wazanzibari. Katika michezo yao mitatu Mhe. Naibu Spika, timu yetu mchezo wa kwanza imeweza kuishinda timu wapinzani ya Rwanda kwa kushinda mabao matatu kwa moja baada ya kuonesha mchezo safi na wa aina yake. *(Makofi)*

Vile vile jitihada hazikuishia hapo timu yetu baada ya siku moja kuendelea kupata mapumziko, mchezo wao wa pili walicheza na wapinzani wetu wa jadi ambao wao waliondoka na dhamira moja tu ya kuhakikisha aina yoyote ile watakayokutana na wapenzi wetu, wenzetu, ndugu zetu mchezo wetu utakuwa ni wa aina yake na utaendeleza ule uteja kwa wenzetu. Nashukuru na naipongeza sana timu ya *Zanzibar Heroes* kuweza kuishinda timu ya Tanzania Bara, Timu ya

Taifa ya Serengeti, *Kilimanjaro Taifa Stars* na kuweza kuishinda kwa mabao mawili kwa moja katika mchezo uliokuwa safi na wa aina yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba vijana wetu wamefanya jitihada ya aina yake na kwa vile walikuwa wanatambua ndani ya michezo yao wanacheza na timu ngumu kabisa ya Kenya na hapo wanaweza kukumbana na timu ngumu kabisa ya Uganda. Mhe. Naibu Spika, katika mchezo wao wa tatu timu yetu ya *Zanzibar Heroes* ilionekana wazi kuonesha kwamba vipaji Zanzibar vipo na vina uwezo kuonekana na vinatakiwa fursa tu ya kuoneshwa. Kwa mustakabali ule walicheza na timu wenyeji, Timu ya Taifa ya Kenya. Pamoja na nguvu kubwa walizokuja nazo wenzetu timu ya Kenya, pamoja na matakwa mengi waliyoyafanya wenzetu kuonesha kwamba timu ya *Zanzibar Heroes* haiwezi kuendelea na vile visago vilivyokuwa vinaanza kutolewa. Mechi ya kwanza na mechi ya pili, walipangiwa mechi zao zote saa nane na wameendelea kucheza mchezo huo saa nane na wakaionesha umahiri mkubwa timu ya Kenya kwa kutokuruhusu bao hata moja kuingia. Kwa hivyo wametoka sare na timu ya Kenya na wakabakisha malalamiko tu kwa upande wa wenyeji. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, la kufurahisha zaidi ni kwamba leo timu yetu itakuwepo uwanjani tena kucheza na timu ya Libya na tayari wamehakikisha kwamba wimbi wataliendeleza wao pamoja na lawama zinazopatikana. Hicho kitu hakipo na wao wataendeleza *football* yao kama walivyoondoka nayo na wanahakikisha kwamba watazifurahisha na kuzisuuza nyoyo za Wazanzibari. Ikifika tu saa nane wananchi wote nawaomba waelekee katika televisheni zao ili kuwashuhudia ndugu zetu na vijana wetu wa *Zanzibar Heroes*.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikujulishe wazi na nilijulishe Baraza lako tukufu kwamba vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* wameondoka na juhudi ya kwenda kumtoa nyoka pangoni. Hawakuwa na nafasi ya aina hii kwenda kuonesha michezo yao na vipaji vyao nje ya nchi. Lakini kwa nafasi ya mwaka huu waliyoipata vijana wadogo wasiozidi umri wa miaka 20 wameweza kutumia jitihada hiyo na kutunawisha uso sana na wanatuahidi kwamba hawatatuangusha.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo, naomba sana sasa Baraza lako tukufu pamoja na kuwapa pongezi na serikali kufanya jitihada zote za kuhakikisha kwamba timu ile inakaa vizuri kule, serikali itaendeleza jitihada zake. Mhe. Naibu Spika, kuanzia sasa nataka nikuthibitishie tunawaongezea dau zaidi tutawapelekea chochote tuhakikishe kwamba zile jitihada wanazozifanya zinaendelezwa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo nataka nikuhakikishie kwamba timu yetu mpaka hivi sasa ina majeruhi mmoja tu na tunatarajia na yeye ataweza kucheza mechi za nusu fainali na mechi za fainali baada ya kumpatia matibabu. Huyu ndiye mfungaji wetu mahiri kabisa ambaye hivi sasa anaongoza kwa ufungaji wa magoli, Ndg. Khamis ana magoli mawili na *inshaallah* ataendeleza hilo wimbi la ushindi wa magoli.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naliomba Baraza lako tukufu kutizama na kujadili shukrani zetu na pongezi zetu hizi kwa timu yetu ya *Zanzibar Heroes* namna gani tunaweza kuisaidia changamoto ndogo ndogo walizokuwa nazo. Ni kweli wapo katika mashindano lakini bado wanakabiliwa na mambo madogo madogo. Itaonekana kwamba pale walipokuwa wakicheza mechi zao kundi la kwanza watakapoingia nusu fainali ambayo sasa hivi tumefikia watakwenda

mji mwengine kwenda kucheza nusu fainali. Kwa hivyo, changamoto za usafiri wa ndani hapa na pale zitakuwepo, ni vyema basi Baraza lako tukufu likajadili nao kuona umuhimu wake namna gani wanaweza na wao kuwaunga mkono timu yetu hii ya *Zanzibar Heroes*.

Serikali kwa umoja wake tutaendelea kuiunga mkono na tunahakikisha kwamba tutawapokea vijana wetu kwa shangwe kubwa sana na serikali tutakuwa kitu kimoja sote kuhakikisha hatua yoyote watakayofikia vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* basi sisi tutawapokea kwa shangwe kubwa sana. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa taarifa hiyo muhimu. Sasa Waheshimiwa Wajumbe nitawapa waheshimiwa ambao wameniletea majina yao hapa dakika tano kila mmoja ili aweze kuchangia. Waheshimiwa naomba nitoe dakika hizo kwa sababu kuna hoja nyengine, lakini tukumbuke tuna mswada leo ambao tunataka leo leo tuupitishe. Kwa hiyo kidogo tupo nyuma ya muda. Sasa ningemuomba Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy awe mchangiaji wa mwanzo kabisa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya dharura kuhusiana na suala la timu ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi mambo yangu yatakuwa ni machache ya kuchangia kwenye suala hili. Kwanza niwapongeze sana vijana wetu Wazanzibari wazalendo wadogo ambao wameweza kwenda kushindana katika mashindano magumu ya hasa waliowazidi umri na walioshiba ugali na sembe na vitu vyengine na tukaweza kuwafunga.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi ningeenda kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kwanza kwenye mazingira ya wachezaji tungeomba sana yaje yawe mazuri kwa sababu wamefanya vitu ambavyo hata kiutalii sasa hivi Zanzibar kwa upande wa Kenya na sehemu nyenginezo ikiwa na timu nyengine, basi hata kwenye suala la utalii washatangaza ukiachia mpira. Ni sifa kubwa imeipa Wizara hii, ni mambo makubwa ambayo wameyafanya kuweza kushinda hizi timu kubwa kubwa na hasa kuweza kuishinda timu ya Rwanda na timu ya Tanzania Bara kwa magoli mbili moja na tatu moja nakumbuka kitu kama hivi.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja ambalo mimi binafsi nataka nimuombe Mhe. Waziri kupitia Baraza lako tukufu kwamba wawakilishi wote tuchangishane kwanza ukiacha kama kuna nyengine, shilingi 25,000 kila mwakilishi kwa watu 87 itakuja shilingi milioni 2,175,000 tutaweza kupata pishi 25 za biriani. Siku watakayorudi timu ya *Zanzibar Heroes* tuje tule nao Wawakilishi wote pamoja na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi katika ukumbi wetu wa *restaurant* nyuma. Wawakilishi wote pamoja na watendaji wa Baraza la Wawakilishi waalikwe na timu yote ya *Zanzibar Heroes* waje wale na sisi biriani, soda na maji huko nyuma. Hizi fedha alizozitaja nimeshafanya hesabu zitatosheleza moja kwa moja kuweza kula nao pamoja na kupiga picha nao pamoja na kuwapongeza kwa upande wa Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna jambo moja ambalo lipo kwa kweli hii timu inataka *support* ya hali ya juu kupitia serikali. Hii timu ni ya Zanzibar ni ya taifa, kuna hali imejitokeza hapo nyuma sio nzuri, lakini ningeomba sana serikali kwa sababu inapata pia makusanyo mazuri kupitia kwa Mhe. Waziri wa Fedha kwamba waweze kuwa-*finance* vizuri. Leo timu ya taifa imeweza kuondoka kwenye mazingira magumu kwa uzalendo kwenda Kenya lakini hatujaweza

kuwaondosha kwa njia ya ndege awamu ya mwanzo. Sasa hili suala halipendezi, leo tunataka mambo mengine ya *FIFA*, haya ya *CECAFA* kwanza yanaanza kutupiga piga chenga. Lazima serikali mfuko wao wautayarishe vizuri wampatie Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo aweze haya masuala kuyasukuma. Kwa fedha za mchango wa Uwakilishi wetu sisi hazitofika kokote, tunachotaka kwamba serikali ni timu ya taifa, ni vyema kwamba wawape wao fedha za kutosheleza na wakirudi warudishwe kwa ndege si mtindo wa kwenda na basi kama wachukuzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili kidogo limewavunja moyo hata wao wachezaji. Lakini kwa tunavyokwenda tutakwenda katika njia nzuri na naamini Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo atapigania kwenye suala hili kuhakikisha mazingira ya wale wachezaji wote yapo vizuri pamoja na viongozi kule walipo.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba sisi sote tunatamani kwenda, lakini ningeomba vile vile kwamba sisi sote tunatamani kwenda. Lakini ningeomba ikiwezekana hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aende kule nchini Kenya akawape pongezi kabla ya kufika huku Zanzibar, kwa sababu tayari wapinzani wetu wakubwa tumeshawapiga bao, Rwanda tumeshaifunga, Kenya tumetoka nao sare, Tanzania Bara ambao tunaupinzani nao mkubwa tumeshawapiga bao tena tunataka nini.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba serikali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hata kama atamwakilisha Waziri wake, pamoja na Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na Wajumbe japo wawili ndani ya ukumbi huu waweze kwenda Kenya, ili kwenda kuwapa *support* kwenye japo mechi moja kabla ya kurudi kwao. Hili ni jambo la lazima kwetu, wakirudi huku ni lazima kuwapokea kwa sababu wale ni Wazanzibari.

Kwanza mimi ninachowapongeza zaidi kwamba wale ni watoto wadogo, wameweza kuonesha mpira wa hali ya juu ukilinganisha na timu zote wanazocheza nazo. Tumeweza kuona juzi na Kenya tofauti ya miaka ni mikubwa, kuna wengine mule wanaweza hata kuwa hata wanawazaa, lakini tumewapiga sare vizuri na tumekwenda nao vizuri.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kila Mwakilishi ningeomba tuwachangie shilingi laki moja moja nyengine, ambayo itaweza kuwa ni mchango wetu kutoka kwa Wawakilishi Wazanzibari wa Zanzibar kwa ndugu zetu wapendwa wa *Zanzibar Heroes* wapelekewe hizo fedha zitakazopatikana kwenye shilingi milioni 8,700,000, ukipiga hesabu ya shilingi 100,000/- mara 87 unapata 8.7 milioni ziweze kukabidhiwa kwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ili kuangalia nini fedha hizi zitaweza kusaidia.

Vile vile shilingi 25,000/- tusisahau za biriani, itakuwa jumla shilingi 125,000/-. Mimi Mhe. Naibu Spika, sina makubwa isipokuwa ninachoomba ni kwamba tunawaombea heri wazidi kucheza vizuri, waje na ushindi kwa sababu ushindi wao ndio ushindi wetu. Mimi sio mchezaji mpira, mimi nina mambo yangu mengine, lakini napongeza sana kwenye suala la mpira na niko nao pamoja na ninawasubiri Inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu watashinda, mimi nitawasubiri Zanzibar sina haja ya kwenda Kenya, lakini watakaokwenda watakuwa wametuwakilisha sote.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa mchango wako mzuri, na mimi naunga mkono ile kauli yako uliyosema kwamba Waheshimiwa Wawakilishi tujiangalie kuona kwamba na sisi tuchangie kwa kiasi fulani, ili tuhakikishe vijana wetu wapo katika hali nzuri na ya kuridhisha. Wameonesha uzalendo mkubwa sana waheshimiwa.

Sasa nimpe nafasi mheshimiwa. Hapa nimepata vikaratasi viwili Mhe. Suleiman Makame Ali wa Ziwani umefuta, kutokana na kwamba Mhe. Nadir Abdul-latif ameshasema yale ambayo ulikuwa unataka kuyasema. Lakini sijui kama Mhe. Suleiman Sarahan Said uliomba kuchangia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi kwa sababu ni mwanamichezo na nilikuwa mchezaji wa zamani wa mpira. Kwa hivyo najua umuhimu wa mpira na dunia ya leo, ajira ndio mpira wenyewe wenye viwango vingi vya fedha, lakini wachezaji wetu wanacheza kwa moyo wa kujitolea kwa kuipenda nchi yao na wananchi wao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maneno mengi waliyokwishakusema wenzangu kuhusu suala la michezo. Lakini sasa hivi kwa utaratibu tulionao katika dunia ya leo, basi mkono mtupu huwa haurambwi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli vijana wetu wamekwenda kujitolea, lakini wamekwenda kujitolea katika mazingira magumu. Ni kama mwanga hata sote hatukutegemea mambo waliyokwenda kuyafanya, lakini kwa sababu wameyafanya na sisi tuna haja ya kujitutumua tukaweza kuwaunga mkono kile walichokifanya, wale ni majeshi yetu wamekwenda kupigana kwa niaba yetu, lile jasho lao ndio damu yao na sisi ndio damu yetu na ni lazima tuweze kuithamini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeomba sana maneno waliyosema wenzangu basi kwa moyo mmoja tuweze kuwachangia, tunawaona wenzetu wanafanya madogo tu basi wanaingia kwenye Mabunge wanakwenda kusalimiana na viongozi, wanakwenda kwa Mhe. Rais kuonana na viongozi. Lakini na sisi hawa watakapokuja basi sio vibaya tukawaita kwenye Baraza la Wawakilishi na wao wakaja wakaungana na sisi, tukala nao chakula kwa pamoja wakajisikia, lakini pia na viongozi wetu wakuu wakaweza kuwapokea kwa pamoja baada ya kuwa wamefanya mambo mazuri. Pia tuwapelekee salamu waliko kwamba wasitosheke na hapo, lengo na madhumuni ni kurudi na ushindi. Kwa hivyo, wao wakituona kwamba kwa moyo mmoja sisi tuko nyuma yao bega kwa bega na wao nakuhakikishieni watafanya mambo ambayo tusiyoyatarajia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ni vitu vya msisimko. Alivyosema mwenzangu tunajaribu kujiandaa kwenda katika *FIFA*, hebu tuangalie hapa tulipo tunawasaidiaje wachezaji wetu na tunaisaidiaje timu yetu katika mazingira magumu. Lakini moja ninachoomba kama alichosema vijana hawa watakaporudi warudishwe kwa ndege ili tuweze kuwapokea sio wasubiriwe kwa boti. Kuna mashirika mengi yapo ya kuweza kuzungumza nayo wakaweza kutupunguzia nauli. Kwa hivyo, tungeomba warudishwe kwa ndege ili tuthamini nafasi yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sasa hivi televisheni zikifika tu wakati wa mechi ya timu yetu basi na sisi tuna uso wa kujiringia, kama zinavyocheza timu za *Manchester United* na nyengine tumepata hamasa kubwa kwa Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Mimi ningeomba sana sina haja

ya kuchukua muda, lakini tuwashukuru sana. Sisi kwa pamoja tunaungana na wenzetu wote walioko katika mshindano huko Kenya, Mwenyezi Mungu awajaalie waende na mashindano yao na warudi salama tuwapokee salama usalimini na tushereheke na Mwenyezi Mungu ajaalie walete ushindi hapa Zanzibar. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said. Nitampa nafasi Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Nimempa nafasi hii maalum kwa sababu Mhe. Ali Salum baadhi ya vijana ambao wamo ndani ya timu hii ya *Zanzibar Heroes* ni vijana wake, yeye ndiye aliyewalea na ndiye aliyewakuza. Kwa hivyo, hiyo ni sehemu ya kazi yake ambayo Mhe. Ali Salum Haji (Kirova) Mnadhimu wetu anaifanya katika jimbo lake. Mhe. Ali Salum pongezi nakupa, lakini vile vile nakukaribisha na wewe kuchangia kidogo, karibu mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji (Kirova): Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya timu yetu ya *Zanzibar Heroes*.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa sana na mimi nitowe ya moyoni kwa vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* kwa namna ambavyo wameweza kuliwakilisha taifa lao kwa hali na mali. Mhe. Naibu Spika, nataka nisema pamoja na hayo uliyoyaongea ya kwamba Jimbo la Kwahani limetoa ushiriki mkubwa katika timu ya taifa, ni kweli lakini kwa mara ya kwanza hata mimi mwenyewe nimeweza kushiriki bega kwa bega mpaka timu ya taifa nimeiondosha bandarini siku waliyoondoka kwa boti ile ya saa 3:00.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana wachezaji wa kutoka Jimbo la Kwahani vijana wetu Feisal Salum kwa umaarufu tunamwita Fai toto, ni kijana ambaye anakaa katika Shehia ya Kwaalamsha, lakini na ndugu yetu Abdul Makame Abui yeye anatoka katika Shehia ya Kwahani. Hizo ni hazina za timu ya taifa, bila ya hizo naamini kwamba timu ya taifa ushindi wake unakuwa kidogo hauko vizuri kwa sababu ndio hazina zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuweka sawa kidogo katika suala la pongezi, kwa bahati wakati tunachangia kuna mjumbe mwenzangu alichangia vizuri na naunga mkono hoja alizoanza kuchangia, hususan ile hoja ya kuchangia Wawakilishi katika maeneo tofauti, kuchangia shilingi laki moja kuwapelekea kwa ajili ya pongezi, lakini kuchangia shilingi 25,000/- kwa ajili ya maandalizi ya chakula vijana wetu watakaporejea. Lakini wakati akichangia alisema kwamba timu yetu iliondoka katika hali iliyokuwa sio nzuri.

Nataka nilithibitishie Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba katika mwaka ambao timu ya taifa ya Zanzibar wameondoka katika hali nzuri na ya furaha na wakatuhakikishia kwamba wanarudi na kombe basi ni mwaka huu. Mhe. Naibu Spika, sababu ya kusema hayo kwa sababu nilisema mwanzo kwamba nilikuwa karibu sana na timu ya taifa ya Zanzibar mwaka huu. Namshukuru Mhe. Waziri wakati alipokuwa akizungumza haraka haraka hakuwahi kutaja mikakati aliyoipanga kwa timu ya taifa ya Zanzibar wakati ikiondoka.
(Makofi)

Mhe. Naibu Spika, iliundwa tume ya watu watatu kuhakikisha kwamba timu ya taifa hii inaondoka katika mazingira mazuri, sina haja ya kuwataja wajumbe hao. Lakini nataka niseme kwamba baada ya mchango wa serikali basi tume hiyo imeweza kufanya kazi ya ziada kwa kushirikiana na taasisi za serikali kupata michango mbali mbali ambayo ilipelekea vijana wale kuondoka katika hali nzuri na ya furaha sana. *(Makofi)*

Miongoni mwa taasisi ambazo zimeweza kutuchangia Mhe. Naibu Spika, walioongoza kwa michango ya juu ni ndugu zetu wa Shirika la *PBZ, ZSTC, ZURA, ZRB*, Shirika la Umeme na Shirika la Bandari. Hizo ni taasisi ambazo zilichangia michango mikubwa kuhakikisha timu ya taifa inaondoka vizuri na inafanyakazi vizuri na hatma yake ndio hii tumeiona. Sababu ya kuondoka na basi kupitia Tanga Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nilikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa kamati mambo ya michezo na mambo yake. Tuliamua kupitia Tanga ili kuwachukua baadhi ya wenzetu kitaaluma kwenda kuhakikisha kwamba timu inashinda vizuri. Lakini mipango yetu tuondoke kwa basi tupite Tanga kwenda kuchukua baadhi ya mipango yetu, lakini marejeo tumepanga tunarudi kwa ndege ya *Kenya Airways*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mipango hiyo tayari Mhe. Waziri tumeshaiandaa na mambo yako vizuri na tunaamini kwa mambo ambayo tumejitahidi kadri ya uwezo wetu na tunaendelea Mhe. Naibu Spika, tulipitikiwa tu hatukujua kuwa siku ya Jumamosi ilikuwa ni *Holiday*, lakini Jumamosi tulikusanya shilingi milioni 8 ili kuwapelekea vijana wetu kuwapa motisha kwa kadri maendeleo yanavyoendelea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nataka niwahakikishie tu kwamba michango inaendelea, vijana wetu waliokuwa tayari kuchangia waendelee kuchangia. Matumaini ya timu ya Zanzibar mwaka huu ni kurudi kwa kombe. Nawatakia kila la heri Mwenyezi Mungu ibariki *Zanzibar Heroes*, Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Sasa nimpe nafasi Mhe. Hamad Rashid Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na yeye aseme machache.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru mbali na kuwa ni Waziri wa Kilimo, Malisiali, Mifugo na Uvuvi pia ni Kaimu waziri wa wizara hii. Kwa hivyo, nataka nichukuwe nafasi hii kwanza kumpongeza sana ndugu yetu Mhe. Nassor Salim Ali kwa kuleta hii hoja. Lakini nataka kwanza tumshukuru Mhe. Rais, kama mlivyokuwa mnashuhudia juhudi anazochukua katika kuimarisha sekta ya michezo na kuhakikisha kabisa kwamba timu zetu zinafanya vizuri na Zanzibar inatangazwa vizuri duniani kwa kupitia michezo, hii ni dhamira na anayafanya mambo haya kwa umakini sana. Hizi juhudi mnazoziona zinachukuliwa na wizara basi zote zinatokana na maelekezo yake. Kwa hivyo, nasema kwanza tumpongezeni sana Rais wetu kwa kuifanya kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Lakini la pili tuchukulie michezo hii kwamba itatusaidia sana katika kuimarisha umoja wetu na kwa hivyo ni wajibu wetu sote kwa pamoja kushiriki kikamilifu kuona kama timu yetu hii inakuwa ni kielelezo katika suala zima la kujenga umoja na mshikamano katika nchi. Kwa hivyo, kwanza nataka nipongeze sana hii hoja na niwaunge mkono na mimi nataka nishauri yafuatayo Mhe. Naibu Spika.

Kwanza mbali na kazi nzuri iliyofanywa na kamati, tunahaja ya kuweka jambo hili kuwa la kudumu katika nchi yetu, kwa sababu sasa tumeshapata mwanga kwamba kama tutajipanga vizuri basi tunaweza tukafanya maajabu sana katika dunia hii kuonesha kwamba Zanzibar inaweza kupiga hatua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa upande wa Baraza la Wawakilishi na kwa uzoefu kidogo nilioupata katika Bunge kule, timu zetu hizi zinapofanya vizuri huwa zinapata heshima maalum katika taasisi zetu hizi kubwa na hasa katika Bunge au Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, nataka kushauri tu kwamba Mhe. Naibu Spika, ule mchango wa kwanza wa shilingi laki moja tungeutoa haraka sana iwezekanavyo ili zikasaidia katika kipindi hiki, tusingoje wakati watakapokuwa wamerudi. Tutowe sasa hivi kila mmoja wetu shilingi laki moja tuhakikishe kabisa zinakwenda kwa wenzetu tuungane na kamati yetu inayofanyakazi ili ziende hizo fedha zikawasaidie pale ambapo pana mapungufu.

Vile vile tujipanga vizuri, ikiwa wameshinda au wameshindwa kwa ngazi ambayo tayari wameshaifikia sasa hivi basi nchi yetu wameshaiweka katika pahala pazuri sana. Kwa sababu katika michezo hasa dunia ya leo uwezo wa kucheza ni jambo moja na wanaoandaa na mazingira ya michezo ni jambo la pili. Inawezekana vijana wetu wakafanya vizuri sana yakaandaliwa mazingira ya makusudi kabisa ya kushindwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimeshaona mambo mengi yametokea katika michezo. Sisi katika ngazi ambayo tumeshafikia, tuseme tayari Zanzibar tumeshashinda lazima tujipange namna ya kuwapokea, kuwatunza na kuwaendeleza vijana wetu ili tutowe nafasi kwa vijana wengine kuona kwamba taifa linathamini juhudi yoyote itakayochukuliwa na vijana wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nina jambo la pili ambalo nataka nilishauri Baraza lako kwamba likubali kuwa tujipange katika hili. Lakini la tatu Mhe. Naibu Spika, mbali na kamati ambayo ipo, mimi nafikiri kama inahitaji kuongezewa hii kamati. Lakini jambo la kuwapeleka viongozi wetu wawili *very strong* wakatoa *support* kwa vijana wetu wale tokea hivi sasa ni jambo la msingi sana. Kwa hivyo, ningependa Baraza lako vile vile liridhie tuchague viongozi wawili wa ngazi ya juu kabisa waende wakashirikiane na vijana wetu kule, na mimi nasema Mhe. Ali Salum Haji amefanya kazi kubwa, basi akijumuika na mtu mmoja mzito na hasa mwenye uzoefu.

Najua hapa Waziri wetu wa Afya aliwahi kusindikiza timu hapa ya Tanzania na akafanya vizuri sana, tungechagua watu wawili wazito wakashirikiana wakaenda kukaa na vijana wakawapa, kuna mambo kidogo ya kisaikolojia, kuna mambo ya kiutuuzima yanataka yaonekane pale, kuna watu wanakwenda kuhonga kidogo wanapita hapa na pale, wakipatikana watu wazima pale inaweza kusaidia kutoa motisha. Kwa hivyo, mimi ningeomba hili Mhe. Naibu Spika, na Baraza lako likubali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema hili ni jambo kubwa na tumpongezeni sana Mhe. Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya, mimi nafikiri na hii itasaidia sana katika kuujenga umoja wetu. Naunga mkono Mhe. Naibu Spika, hoja hii ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tumeshaijadili vya kutosha hoja hii. Sasa nitoe ruhusa kwa ajili ya kujadili hoja ya pili inayohusiana na vifo vya wanajeshi.

Aah! Waheshimiwa Wajumbe, nimeambiwa niwahoji kwanza. Samahanini nimekuwa *carry doubt* na matokeo haya mawili. Kwa hivyo, naomba niwahoji wanao...

Naam. Mhe. Hamza Hassan.

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kukubali hoja zilizoletwa juu ya meza yako, lakini hizi hoja pia zimekuja na mapendekezo mbali mbali

Mhe. Naibu Spika: Naomba uniambie kifungu unachokizungumzia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nilisema naomba muongozo wako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Aah! unataka muongozo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Eeeh.

Mhe. Naibu Spika: Ok.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwamba katika hizo hoja zilizotolewa kuna mapendekezo mbali mbali. Kuna mapendekezo yamekuja ya kuchangia shilingi laki moja, kuna mapendekezo yamekuja ya kuchangia shilingi 25,000/-. Lakini mwisho limekuja pendekezo jengine la kwenda viongozi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tukiangalia mazingira halisi, timu ilivyokwenda inahitaji zaidi *support*, sio kuongeza matumizi. Sasa naogopa sana kuja kuhojiwa nikasema nimekubali ikawa nimekubali na jambo la kuongeza matumizi. Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako na mtoa hoja kama atakubali, tukubali tuichangie timu yetu. Lakini vile vile niongeze jengine serikali iangalie mazingira, timu yetu irudi kwa ndege baada ya machofu ya kazi ngumu.(*Makofi*).

Sasa Mhe. Naibu Spika, lile moja tu la kuongeza matumizi kwa sisi viongozi kwenda. Mimi nafikiri lile tusubiri hapa ili wakija tushirikiane kwa pamoja. Kwa hivyo, kabla ya kutoa hiyo hoja katika yale mapendekezo, sasa sijajua yepi yatakuwa yamekubaliwa na yepi yatakuwa yamekataliwa. Mimi nilikuwa napendekeza kuondoa hilo moja tu la kwenda sisi viongozi, lakini kwa kuchangisha pesa haina tatizo, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kidogo muongozo wako katika hili, kwa sababu kidogo natofautiana na Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Naibu Spika, tofauti yetu iko sehemu moja. Timu hii kwa uzoefu wangu mimi pia wanahitaji *moral support*, wakati juzi wale vijana wamekwenda kupimwa kwa ajili ya matumizi,

wamepimwa mkojo tutamke vile vile kwenye Wizara ya Afya tunatamka vile vile wamekwenda kufanyiwa *test* za mkojo. Pale walikuwa *demoralise* wale vijana, kwa sababu walifanyiwa *test* zile *just* kwa sababu walicheza vizuri, na wale walishtuka kwamba hawa wamewezaje kucheza vizuri kama hivi. Waliposhtuka wakasema hawa lazima watakuwa wametumia dawa fulani, kwa hivyo tuwafanyie *test* hizi.

Katika *test* zile walipofanyiwa viongozi wetu hawakuwepo waliwekwa nje, na aliyekwenda kule naamini na timu ni ndugu yetu Maalim Khamis ambaye nadhani ni Katibu wa Baraza la Michezo Zanzibar ndio kiongozi wa juu kabisa. Wakati timu ya Taifa ya Tanzania ilifanya vizuri Burkinafaso Ouagadougou ilikuwa timu inaongozwa na Naibu Waziri wakati huo Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, na mimi nakumbuka fika wakati huo ulikuja ujumbe mzito. Naomba hili pia nieleze katika kutofautiana na ndugu yangu Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba ulikuja ujumbe mzito kutoka Tanzania Bara ambao ulitumwa na Rais wakati huo Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, alikuwepo Ndg. Ramadhan Dau ambaye alikuwa *Director General* wa *NSSF*, alikuja Ndg. Mohammed Dewji ambaye alikuwa ni Mbunge pia na Mwenyekiti na wengine wajumbe watatu wazito.

Kwa hivyo, ninachoomba mimi katika muongozo wako Mhe. Spika, *moral support* mbali ya michango, mbali ya biriani ya Mhe. Nadir hapo, mbali ya soda. *Moral support* kuwepo kule kwa vijana hao kwa mechi zilizobakia ni muhimu sana. Naomba katika maombi hayo wachaguliwe viongozi wawili mpaka watatu Baraza watakayeona anafaa waende wakatoe *moral support, it will create a huge different.* Mhe. Naibu Spika, wewe utafurahishwa sana kombe likikaa hapo mezani kwako mbele na ile timu ikaruhusiwa kuingia Barazani na Kocha wao itakuwa ni furaha kubwa kwa Zanzibar. *(Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar imeshaonewa na kuteseka sana huko nyuma katika mambo mbali mbali ya michezo kuanzia ngazi ya *FIFA* mpaka *CECAFA.* Zanzibar juzi tumeshuhudia wale vijana wakidhalilishwa kwenda kupimwa hakuna mchezaji mwengine wa timu yeyote aliyekwenda kupimwa mkojo, ila wachezaji wa timu yetu na viongozi wetu walizuiliwa nje wakati wao wameingia ndani. Mimi naomba kwa mechi zilizobakia bajeti ya Baraza la Wawakilishi ipo, watolewe viongozi watatu wazito waende wakaunge mkono timu yetu. Naomba muongozo wake Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Jamani hoja hii naona sasa inakuwa ndefu mno. Namuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kidogo na yeye atoe nasaha zake na iwe tumeshajadiliana, nafikiri nitauliza Wajumbe kwa makubaliano baadae tuendelee na hoja nyengine. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nikushukuru kwa utaratibu huo wa kutoa muongozo lakini kwanza nataka nichukue nafasi hii na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tumbani kupongeza sana *Zanzibar Heroes* kwa ushindi ambao tumeupata.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mawazo yote yaliyotolewa na Wajumbe ni mazuri na sote sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ningewashawishi wenzangu tukubaliane na hoja ya kuchangia shilingi laki moja badala ya ishirini na tano, lakini la pili nakubaliana na Mhe. Hamza Hassan Juma

Muwakilishi wa wananchi jimbo la Shaurimoyo kwamba tutakachokichanga na kama kuna chengine chochote kitatokezea tukiweke kwa ajili ya kuwa-*support* wachezaji wetu pamoja na watu walioko kule Kenya.

Mhe. Naibu Spika, kuongeza *moral support* nakubali lakini suala la kupunguza gharama ili fedha zitakazopatikana zozote zile ziwe zinatoka Serikalini, ziwe tulizochanga, ziwe watakazochanga tuwaongezee nguvu vijana wetu ili waishi vizuri. Sisi viongozi nakubaliana na suala la kwenda lakini tujitolee, kama kuna kifungu kinaweza kikamsafirisha Waziri wa Habari kule Wizarani kiingie katika fungu la timu yetu ya Taifa ili waweze kufanya vizuri zaidi, kama mimi nataka kwenda nitafute fedha zangu mwenyewe nitafute tiketi nikalale hoteli niende kule nikawape *moral support*. Kama ni hivyo nakubaliana na wazo hilo ili kile ambacho kitatolewa na Serikali na kile ambacho tutachangia sisi wenyewe kiende kwa wachezaji moja kwa moja ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Michango yenu lakini pamoja na muongozo ambao ameutoa Mhe. Hamza ameniomba na mimi niweze kutoa muongozo ili kuona kwamba yale ambayo tunayajadili hapa sasa tunayafanyia kazi, baada ya michango mbali mbali kutoka kwa Wajumbe pamoja na Mawaziri waliokuwepo hapa niseme tu kwamba. La kwanza ambalo tumekubaliana na nitakuja kuuliza baadae kama tumekubaliana kwa pamoja ni lile la kuchangia laki moja kila Mjumbe (*Makofi*).

Lakini la pili vile vile ambalo tumekubaliana ni lile ambalo kuwa na mfuko wa dharura pale ambapo litakapotokea lolote basi tutakuwa tuna uwezo mzuri wa kuweza kusaidia, nafikiri hilo litakuwa la pili.

Lakini la tatu ni kwamba na nimefahamu vizuri sana maelezo ya Mhe. Waziri wa Afya, suala zima la kuwapa *moral support* vijana wetu, kwa kweli ni muhimu sana na ndio maana tunaona mataifa mengi sana wakati ambapo yanatokea matokeo kama haya viongozi wakuwa wanakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wale ambao wanajitolea na kufanya shughuli ambazo zinatengeneza jina la taifa wanapewa hiyo *moral support*. Lakini sasa vile vile tunaangalia na hali halisi ilivyo yetu ya kifedha. Kwa hivyo tumeona nafikiri kwa maoni ya Mheshimiwa wa Nchi, Afisi, ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwamba basi zile fedha ziweze kutumika katika masuala ambayo yatajitokeza kwa kuhudimia wale wachezaji.

Lakini hiyo haikatazi Mheshimiwa yeyote ambaye anahisi kwamba anataka kwenda kwa ajili ya kuwapa *moral support.* Kwa maana hiyo, Waheshimiwa hapa kilichojitokeza ni kwamba tujitolee, tujitolee kuhakikisha kwamba tunakwenda kama Waheshimiwa kwa tiketi zetu wenyewe lakini kwa kuweza kujihudumia masuala ya hoteli na mengine ili tukawape *moral support* vijana wetu *(Makofi)*

Sasa Mhe. Waziri ana nafasi nzuri yeye ana uwezo katika Wizara yake kuhakikisha kwamba anaweza vipi kupeleka kwa bajeti hiyo nyengine, anaweza vipi kuwapeleka viongozi, niseme hayo machache na vile vile mimi nichukue fursa hii adhimu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili amesema kwamba Rais wetu amekuwa mstari wa mbele kabisa kuhakikisha vijana hawa wanakwenda katika mazingira mazuri na wanauleta ushindi, hii yote ni juhudi ya Mhe. Rais wetu naomba sana kupongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe sasa baada ya hivyo labda niwaulize yale ambayo yote tumekubaliana hapa kama tumekubali kwa pamoja basi naomba munyooshe mikono, Waheshimiwa Wajumbe tumekubaliana yote.

Waheshimiwa Wajumbe: Ndiyooo!

Mhe. Naibu Spika: Ahsanteni sana nawashukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, hoja inayofuata ni hoja ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh inayohusiana na vifo vya wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na ameomba Serikali itoe taarifa lakini vile vile tuweze kujadili, lakini kabla ya kujadili na Serikali kutoa taarifa ameomba vile vile Waheshimiwa na mimi nakuombeni tusimame kidogo ili sasa kuweza kuwaombea wale ambao wametangulia mbele ya haki, lakini vile vile na kuwaombea wale ambao ni majeruhi wapone kwa haraka sana na vile vile kuwaombea wale ambao wameondokewa na wapenzi wao na ndugu zao na rafiki zao, Mungu awape subra. Waheshimiwa naomba tusimame kwa muda mdogo.

(Hapa Baraza lilisimama kwa muda kwa ajili ya kuomboleza)

Mhe. Naibu Spika: Amin. Naomba tukae.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuweza kutoa taarifa kwa ajili ya hoja ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha nimshukuru sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa hoja yake hii na mimi kwa niaba ya Serikali niungane na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jemedari Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kutokana na vifo vya askari wetu waliokuwapo *DRC* pamoja na wale waliojeruhiwa. Naungana na Mhe. Rais kuwaombea dua Mashujaa wetu hawa waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awajaalie walale mahala pema peponi.

Aidha tunawaombea wale waliojeruhiwa kupona haraka na warudi katika hali zao Mwenyezi Mungu wetu tusaidie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwanza niseme Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jemedari Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kusherehekea sherehe za Uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Disemba, 2017 alitoka kauli rasmi ya kuelezea msiba huu mkubwa uliolikumba taifa la Tanzania lakini na dunia kwa ujumla kutokana na majemedari wetu hawa majeshi yetu walio mstari wa mbele kule *DRC* kwa ajili ya kuhakikisha na kulinda usalama wa wenzetu kule wakiwa katika kikosi cha kulinda amani. Aidha msemaji wa jeshi la Wananchi wa Tanzania jana alitoa taarifa kwa niaba ya Jeshi kuielezea nchi hali iliyotokezea huko.

Kwa upande wetu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tulikuwa tunaendelea kuwasiliana na Makao Makuu ya Jeshi kwa sababu ndio utaratibu wetu kutoa taarifa rasmi pale maandalizi yote

yamekamilika, sisi upande wetu ni kupokea maiti wale wanaokuja Zanzibar na kushiriki hatua zote za mazishi pamoja na kutoa mkono wa pole kwa jamaa, familia na marafiki. Utaratibu huo unaendelea kuandaliwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atawapokea majemedari wetu hawa waliotangulia mbele ya haki na utaratibu rasmi utatangaziwa baadae leo hii na Serikali baada ya matayarisho yote kukamilika kati yetu na wenzetu wa JWTZ.

Hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba tuvumilie mpaka baadae ambapo Serikali itatoa taarifa rasmi lakini maandalizi ya pamoja na wenzetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania tunashirikiana ili kujua ni wakati gani maiti hizi zitawasili, na lini zitakuwa hapa Zanzibar, lini zitazikwa rasmi na mambo yote hayo tutafanya kwa kushirikana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo kwa heshima na taadhima na Baraza lako tukufu naomba litukubalie kwamba baada ya kukamilisha utaratibu mzima tutatoa taarifa rasmi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru sana, namshukuru mtoa hoja, nalishukuru Baraza hili tukufu aidha niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa uvumilivu mkubwa na msiba mkubwa huu tulioupata ni msiba wetu sote Mwenyezi Mungu atujaalie, familia za majemedari hawa ziwe na moyo wa subra na Mwenyezi Mungu awapokee wenzetu hawa waliotangulia mbele ya haki awalaze mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Naibu Spika: Amin. Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameshatoa hiyo taarifa na ametuomba tuwe na moyo wa subra kwa ajili ya taarifa nyengine ambazo zitaletwa vile vile na Serikali. Sasa Waheshimiwa Wajumbe kama kuna mtu yeyote ambaye anataka na yeye kuchangia. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nakushukuru tena kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia huu msiba ambao umetupata ni msiba wa taifa, kama ulivyotangulia kusema sisi lililobakia tuwaombee Mwenyezi Mungu wenzetu hawa mashujaa Mwenyezi Mungu awapokee na awaweke katika malazi mema peponi, Amin.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumza jambo moja mahasusi katika hoja hii, hawa ndugu zetu wamepoteza maisha yao kwa kutetea taifa kama ingelikuwa ule wakati wa kupigania Dini tungalisema wamekufa mashahidi, na mtu anapokufa shahidi tunaambiwa mwili wake hauozi. Mhe. Naibu Spika, nachukulia mfano huu kwa vijana wetu hawa wamelitetea taifa la Tanzania bila ya kujali mahali walipotoka.

Mhe. Spika, mapendekezo yangu kwa Serikali tumekuwa na changamoto kubwa sana kwa mashujaa wetu wanapokwenda kutetea taifa, wanapokwenda kupigania taifa baada ya kupata matatizo aidha ya vilema au ya kufariki dunia, familia zao tunaziacha katika mazingira magumu, wengine wanakuwa wameacha watoto wadogo, lakini vile vile wazazi wao wanakuwa watu wazima, watoto hawa walikuwa wanawategemea.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika jimbo langu ninao mfano mzuri kuna mwananchi wetu alikwenda katika vita vya Uganda na kwa bahati mbaya yeye hakufariki lakini alikatwa mguu alipata tabu sana tulihangaika naye sana, tumepanda tumeshuka lakini kwa kweli huduma zake zilikuwa sio nzuri. Sasa mapendekezo yangu hawa ndugu zetu au vijana wetu waliofariki. Vijana hawa ukiwaangalia wengi wao ni vijana wadogo sana, sitegemei kama yuko angalau anayefika

miaka 40 wengi wao ni vijana ambao wako chini ya miaka 35 na ukiangalia tumejaribu kuona katika mitandao mbali mbali wengine wamepakata watoto wao wadogo wakiwa na miezi miwili wengine wakiwa na miaka miwili na pengine ndoa zao zilikuwa ndio kwanza mapema baada ya kuoa wamekwenda kulitetea taifa. Naomba sana kifo tunajua mtu yeyote anaweza kufa hata yuko ofisini mtu anaweza akafa ndani ya Baraza la Wawakilishi kakamati *mic* kifo pahala popote kinatokea, lakini mazingira ya vifo yanatofautiana.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Serikali tukae tuangalie familia kama nilivyosema vijana hawa wengi ndoa zao ndio kwanza ziko mapema, tunajua mjane ataolewa lakini mtoto anahitaji huduma na katika huduma kuna mazingira mengi ya huduma ndio maana nikasema Serikali tukae, tunaweza tukashauriana mambo mbali mbali mfano ana mdogo wake anaweza akasaidiwa na yeye mazingira ya kupatia ajira *atleast* kuweza kumhudumia yule mtoto au kuweza kuhudumiza zile familia zao.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naomba siku ya kuwapokea mashujaa wetu hawa basi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia Waziri wake tunaomba sana ripoti tuipate mapema ili tujiandae kwa ajili ya kwenda kushiriki kwa pamoja, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda kuonyesha umoja wetu na utaifa wetu na vile vile kuwapa moyo wafiwa wa ndugu wa marehemu hao.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika naunga mkono hoja ambayo iliyotolewa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh, mwenzangu hapa alisema katika siku ambayo Mhe. *DAISPORA* katoa hoja ya maana sana ndani ya hapa Baraza la Wawakilishi, basi hoja hii kwa hiyo naomba tumuunge mkono, lakini pia ule ushauri wangu Serikali kuangalia mazingira kuweza kusaidia familia za marehemu hao. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru Mhe. Hamza na ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yaani kwa maana kwamba na Serikali kama alivyosema Mhe. Hamza kwamba Serikali yenyewe iweze kutoa kauli hapa kwa yale ambayo Mhe. Hamza ameyazungumza. Lakini hata hivyo nimepata pia Mhe. Maudline Cyrus Castico ambaye ni Waziri wa Uweshezaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nimpe na yeye nafasi dakika tano aweze baada ya hapo ndio utatoka muongozo kutoka Serikalini.

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa sikukusudia kama Serikali itoe kauli hapa, nilisema Serikali wakae, kwa hiyo...

Mhe. Naibu Spika: Ndio sawa lakini anapokea, lazima Mhe. Waziri aseme kwamba amepokea ni hilo tu.

Mhe. Waziri wa Uweshezaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukuwe nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba na mimi nimeweza kuhudhuria katika Baraza hili leo.

Nilitamani sana ningeweza kuchangia hata ile ya vijana lakini naona imepita na nitaendelea kuibariki na kuungana na wenzangu wote na hasa kwamba inatengeneza ajira kwa vijana, tuendelee kuwatia moyo na kuwabariki sana.

Lakini katika hili mheshimiwa na msiba ni suala ambalo la kitaifa na linagusa sisi zote wataona kwamba ni vijana mashujaa ambao wamepelekwa kwa kule, walikwenda kwa ajili ya kutetea nchi yetu ni mzigo ambao ni wa taifa zima, ninachotaka kusema tu kwamba namuunga mkono Mhe. Hamza alipokuwa amezungumza kusema kwamba mara nyingi wafiwa na watoto wanapokuwa wamefiwa mazingira yanayofatilia yanakuwa ni mazingira magumu sana na mimi kwa wizara yangu nimekuwa niki *experience* wengi ambao wazazi wao tokea nikiwa mwalimu Skuli ya Ng'ambo wakati wa vita vile vya Uganda walikuwa wakisichana walikuwa wanaolewa kipindi kile lakini walikuwa ni wari wakafiwa na waume zao maisha yao yakawa maisha ya mashaka.

Ninachopenda kusema tu kwamba tumekuwa tukiadhimisha sikukuu za mashujaa kila siku na kila mwaka Tanzania kataifa yetu ambayo ni siku kuu muhimu lakini hatuoni ni jinsi gani tunavyokuwa tunawashirika wale ambao ni wahanga watoto na wanawake wanaokuwa wamefikwa na waume zao, ambao ningehisi kwamba nalo linaweza kuchukuliwa likangaliwa ni jinsi gani basi siye tunaweza kutambua na kuwafatilia kwa karibu kwa sababu wale wamekwenda kwa ajili ya kutetea taifa ni jambo ambalo linaweza likajadiliwa likaangaliwa baadaye namna gani ya kuweza kulifanyia kazi.

Lakini ningependa kusema tuu kwamba sisi kama wanawake ambao tunakuwa tunahusika moja ka moja kwenye masuala haya wakishaondoka hawa familia zinakuwa ni kubwa na wengine wanawake wanaachwa wakiwa ni wajawazito namna ya kuja kutambuliwa na mara nyengine familia inapokuja kwenye masuala ya nini wanakuwa wanaathirika. Kwa hivyo, ningesema kwamba ni vyema tukaendelea kuwatia moyo wale ambao wanakuwa wanaondokea na kama kutakuwa na utaratibu wa makusudi vijana au watoto wanaokuwa wanabakia katika mazingira yake Serikali yetu ingalie jinsi gani ya kuendelea kuwashakilia ili waweze kukaa kwa amani na salama kuepuka suala zima la watoto wengi wanaobakia katika kuhangaika pasipokuwa na mtizamo na malezi mazuri katika jamii.

Mimi nilikuwa nataka kusema hilo tu mheshimiwa naungana na wenzangu wote tutaendelea kuwaombea na kuwatia moyo wanajeshi wasiogope lakini bahati nzuri wamepata nchi ambayo ina viongozi wazuri sana tangu tumepata uongozi wa Mwalimu Nyerere na Karume tumekaa kwenye amani na viongozi wote ambao wameingia katika Serikali yetu tumekuwa na amani Tanzania.

Kwa hiyo, suala zima la misukosuko ya msiba ya maaskari inakuwa hatukuipata Mungu katubariki sana tuendelee kuiombea amani na kuendelea kuitunza na kuwa karibu na hawa wanaofiwa. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri nampa nafasi sasa Mhe. Ali Salum Haji kama Mnadhim wetu kutoka Chama cha Mapinduzi ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika nakushukuru kwa mara nyengine na nipende kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Adhaa wa Jaalah kwa kutujaalia afya njema na uhai na mimi niliona niseme lolote katika hoja hii ya tukio lililowapata wapiganaji wetu nchini Congo.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijasema lolote kwanza nilikuwa naomba niiombe Serikali mwenzangu Mhe. Hamza wakati akichangia hoja hii alisema tupewe taarifa ya kufika uwanja wa ndege tujipange vizuri, lakini mimi nilikuwa naomba tu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pindipo miili ya marehemu wale itakapowasikili wajitahidi kupanga mazingira mazuri ili kila marehemu apate uwakilishi mzuri wa Serikali, kwa sababu hofu yangu wasije wakazikwa kwa wakati mmoja ikawa Serikali imeenda sehemu nyengine, sehemu nyengine uwakilishi wa Serikali haukuwa mzuri. Vyenginevyo basi tuwe na uwakilishi wa kupeleka watu katika maeneo hayo labda huku akienda Waziri wa Tawala huku aende Waziri wa Fedha kwengine aende Waziri mwengine kwasababu vijana waliofariki ni wengi na viongozi kama tunavyoelewana tuko wachache haitokuwa vyema maana yake kusubiriana kwenda katika msiba wa maeneo yote. Sasa nilikuwa naomba tuu kupanga utaratibu mzuri wa kupata uwakilishi wa Serikali katika kila eneo hilo lilikuwa na kwanza.

La pili Mheshimiwa na mimi niseme niombe Serikali baada ya kustiri miili muda utakapofika na kuiliza katika maeneo matakatifu basi ni vyema tukajaribu kuziangalia familia za marehemu hawa ili nazo zione Serikali yao inawajaali na tuone kwamba ndugu zetu hawa wamefariki katika kupigania nchi yao na amani ya nchi zetu.

Chengine Mhe. Naibu Spika, basi niziombe familia hizi na nipende kuzipa pole ili waelewe kwamba hii ni mipango ya Mwenyezi Mungu lakini pia niziombe familia za wana jeshi wengine ambao wako Congo basi Serikali ijitahidi kutupa taarifa za uhakika.

Mhe. Naibu Spika, nasema hili kwa sababu miongoni waliokutana na kadhia hii mimi mwenyewe nina mdogo wangu wa kuzaliwa kabisa yuko Congo alikuwa katika tukio hili na Mwenyezi Mungu amemnusuru hakupata haya majanga ya mauti na majeraha makubwa lakini tangu juzi familia imekuwa ikiteseka na kuhangaika kujua hali za ndugu zetu waliokuwa kule. Sasa niiombe Serikali basi iwe inatupa mashirikiano katika kutupa taarifa za vijana wetu ambao wako Congo na wamekubwa na kadhia hii, unakuwa hujui wapi pa kwenda na hujui wapi pa kupata taarifa za kusikiliza kwa sababu familia ndio familia.

Lakini la mwisho Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme kwa niaba ya Chama changu cha Mapinduzi suala la uaskari halina chama, lakini Chama cha Mapinduzi ndicho kinachotawala Serikali hii. Sasa kwa niaba ya Chama Cha Mapinduzi na kwa niaba ya Mhe. Rais napenda nitoe pole za dhati kupitia Baraza lako Tukufu kwa wale wote waliofikwa na kadhia hii Mwenyezi Mungu azijaalie roho za marehemu azilaze mahala pema peponi na wale majeruhi wote Mwenyezi Mungu awajaalie wapone haraka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kidogo na wewe uzungumze machache kuhusiana na yale ambayo Waheshimiwa wameyapendekeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru tena na niwashukuru Waheshimiwa waliotoa hoja katika hoja hii inayotuhudhunisha sote na sote tunajuwa umuhimu wa wenzetu hawa majemadari wetu walioko kule *DRC* unaosimamia hali ya amani ya nchi yetu.

Ni kweli ni *mission* imetoka Serikali ya Jamhuri ya Muungani lakini kupitia Umoja wa Mataifa, hivyo kuna utaratibu ulio kamili ya namna ya kushughulikia utaratibu mzima unaohusiana na masuala haya ya vifo pamoja na majeruhi wanaotokana wanapokuwa katika utaratibu huo. Wanajeshi wetu wanahudumiwa kwa mujibu wa Sheria wa Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu vyovyote vile utaratibu utafanywa ili haki zao kwa mujibu wa sheria zikamilike.

Napokea ushauri uliotolewa na wajumbe nitauwasilisha Serikalini kwa yale yote ambayo tumesema yafanyiwe kazi vizuri tuone lipi kama Serikali itazidi kulifanya. Lakini nataka niwahakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunashirikiana na familia kuhakikisha maziko yanafanyika na taarifa Wajumbe zinapatikana ili waweze kushiriki na haya yote yaliyoshauriwa ili utaratibu mzuri ufanyike wa maziko tutafanya kama ambavyo waheshimiwa wametushauri. Nina hakika kila kitu kitakwenda sawa kwa sababu matayarisho yamo njiani na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha tuwapokee majemadari wetu hawa kwa kila heshima ya kitaifa ili na utekelezaji wa maziko yao yaende kwa mujibu wa taratibu na sheria zilivyo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kupokea maoni mbali mbali kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Kuweka Vifungu vya Usajili na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzia Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na hali ya uzima ambayo imetuwezesha kukutana tena hii leo katika mkutano huu.

Mhe. Naibu Spika, aidha nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa ya kuwasilisha Mswada wa sheria ya kuanzia Wakala wa Kuanzisha Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, shukrani za pekee zimuendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza ala Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniagiza kuwasilisha rasmi Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi, jambo ambalo linanizidishia ari, nguvu na kasi ya kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora kutokana na maelekezo yake anayonipa mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Shamata Shaame Khamis Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Micheweni, hakika usaidizi wake umekuwa na manufaa makubwa katika ofisi yetu.

Vile vile napenda kutowa shukrani zangu za pongezi kwa katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utekelezaji wa majukumu yake katika kuhakisha kuwa kuwa majukumu ya wizara yanatekelezwa kwa umahiri na kiwango stahiki katika Ofisi hii ambayo kwa sasa ni takribani mwaka wa nne sasa tuko kuundwa kwake upya nami nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia ofisi hii bila ya kusahau watendaji wote wa Ofisi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwani ushirikiano wao kwangu ndio chanzo cha mafanikio haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuwashukuru Mhe. Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kwa kukubali kupokea, kujadili na kuridhia hatua zinazoendelea za Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Chimbuko la Mswada

Mhe. Naibu Spika, chimbuko la mswaada huu ni kuwepo kwa haja ya kuwa na sheria mpya ya kuanzisha wakala wa usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar itakayoendana na mahitaji ya sasa na kutoa huduma bora na kwa urahisi kwa wananchi.

Madhumuni ya Mswada

Mhe. Naibu Spika, mswada huu unalenga kufuta sheria tatu ambazo kwanzo ni Sheria ya Usajili wa Mzanzibar Mkaazi namba 7 ya mwaka 2005 pili Sheria ya Usajili wa Vifo namba 6 ya mwaka 2006 na tatu Sheria ya Ndoa na Talaka kwa waislamu sura ya 9 na kutunga sheria itakayoanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa usajili wa matukio ya Kijamii. Aidha, wakala utakuwa ni wakala wa Serikali na utafanya kazi chini ya ofisi yenye dhamana ya matukio ya kijamii.

Kabla ya kupitishwa kwza mswada huu kazi za taasisi hizi zilikuwa zikitekelezwa na taasisi mbili tofauti kwa sasa ofisi hizo zimeshaunganishwa kibajeti lakini kuna mifumo miwili ya usajili inayofanya kazi kwa kujitegemea.

Mifumo hiyo ni mfumo wa usajiri wa Mzanzibar Mkaazi na Utzambulisho na Mfumo wa Pili ni Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Matukio ya Kijaamii ambayo yatasajiliwa chini ya Wakala huu ni Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Kadi za Utambulisho.

Maelezo ya Mswada

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umezingatia maagizo ya Serikali kwa lengo la kuanzia Wakala wa Usajili ni Taasisi yenye Kujitegemea katika kutekeleza majukumu yake aidha wakala huu utaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atakuwa ni Ofisa Mtendaji Mkuu na atateukiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha kutakuwa na Bodi ya Ushauri na vile vile kutanzishwa Idara na Vitengo mbali mbali vinavyohusiana na masuala ya usajili ambavyo vitaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji.

Muundo wa Sheria

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Uwakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar umegawika katika sehemu sita (6) na vifugu hamsini na sita (56) vinavyosomeka kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza

Sehemu hii inajumuisha vifungu viwili ambavyo jina fupi la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na ufafanuzi.

Sehemu ya Pili

Sehemu hii ina vifungu viwili ambavyo ni vifungu cha tatu hadi cha nne vinavyoelezea kuanzisha kwa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Kazi za Wakala.

Sehemu ya Tatu

Sehemu hii ina jumla ya vifungu kumi na nne (14) kuanzia kifungu cha tano (5) hadi kumi na nane (18) ambavyo vinaeleza Utawala wa Uwakala, Uanzishwaji wa Bodi ya Ushauri ya Uwakala, Kazi za Bodi, Muda wa Bodi, Uteuzi wa Mwenyekiti, Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, Kazi za Mkurugenzi Mtendaji na Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji, Kuanzishwa kwa Idara na Vitendo vya Wakala na Uteuzi na Sifa za Afisa Usajili.

Sehemu ya Nne

Mhe. Naibu Spika sehemu hii inajumla ya vifungu ishirini na sita (26) kuanzia kifungu cha kumi na tisa (19) hadi arubaini na tano (45) ambavyo vinaelezea usajili wa matukio ya kijamii masharti ya Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Kadi za Utambulisho.

Sehemu ya Tano

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina vifungu vitatu (3) kuanzia Kifungu cha arubaini na sita (46–48 ambavyo vinaelezea vifungu vya usimamizi wa fedha za wakala wa usajili wa matukio ya kijamii.

Sehemu ya Sita

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina vifungu vinane (8) kuanzia kifungu cha 49-56 ambavyo vinaelezea vifungu vyenginevyo. Masuala ya kufuta usajili, ada ya usajili, kurejesha cheti au kitambulisho, makosa na adhabu, utungaji wa kanuni na kufutwa kwa Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi ya 2005, Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo ya 2006 na Sheria ya Ndoa na Takala kwa Waislamu, sura ya 91.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwenye Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa kufuata taratibu za kisheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ili Waheshimiwa Wajumbe waupitie, waujadili na hatimae kuupitisha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri sasa nimpe nafasi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa ajili ya kuja kutoa maoni ya kamati, mheshimiwa karibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): *Bismillah Rahman Rahiym.* Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na kuanza na hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Jamii, Zanzibar na kuweka vifungu vya usajili na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma na Mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki pamoja na kutupa neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umakini na umahiri mkubwa na kuhakikisha kuwa chombo hiki kinaweza kukamilisha matakwa ya demokrasia. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika kutekeleza jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile shukrani za pekee ziende kwa uongozi mzima wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupatia katika kufanikisha kupitia na kuujadili kwa kina mswada huu muhimu katika nchi yetu. Aidha, pongezi za pekee ziende kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa juhudi

zake kubwa za kusimamia na kuhakikisha kwamba mswada huu umekamilika na kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo sitokuwa mwingi wa fadhila ikiwa sitowashukuru wadau wote walioshiriki katika kuuchangia mswada huu kwa juhudi zao walizoonesha katika kufanikisha Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na kuweka vifungu vya usajili na mambo mengine yanayuhusiana na hayo, kwani ni wajibu wao kuweza kuuchangia kwa ajili ya maslahi yetu na taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa kamati inawashukuru wadau hao kwa michango yao mizuri ambayo naamini imesaidia sana kuufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Vile vile, napenda kuwahakikishia kwamba maoni na ushauri wao umezingatiwa na kamati wakati ilipokaa na wizara na kupatiwa ufafanuzi kuhusu mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeelezwa kuwa madhumuni ya kuletwa kwa mswada huu ni kutunga sheria itakayoanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Usajili wa Matukio ya Kijamii. Hivyo, kwa kuwa kamati hii inazifanyia kazi taasisi zote mbili zitakazounganishwa na sheria hii ya Ofisi ya Usajili ya Vizazi na Vifo pamoja na Ofisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho, basi ni wazi kuwa kamati inaunga mkono mswada huu na imejitahidi kwa kila njia kuhakikisha kuwa mswada huu unakuwa bora na unafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia kanuni ya 106 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2016), kamati imepewa jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika. Aidha, kamati kwa kushirikiana na wizara husika pamoja na wadau mbali mbali walioalikwa kwa lengo la kuupitia mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya *108(12)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar (Toleo la 2016), imetoa fursa kwa Mhe. Spika kupeleka Mswada wa Sheria katika kamati na kujadiliwa. Hivyo, kamati yetu imeupitia, imeujadili na kushauri mambo mbali mbali yakiwa na mnasaba wa kujenga na kufanikisha matakwa ya Mswada huu wa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niwatambue Wajumbe wanaounda kamati hii kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul - latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Nd. Haji Jecha Salum	Katibu

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo kamati yetu imeyafanya na pia naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa

Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilikutana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu pamoja na kufanya marekebisho ya kimantiki na kisarufi kwa kila sehemu iliyoona inafaa kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri katika sehemu ya kwanza ya utangulizi katika mswada huu, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho katika tafsiri ya neno "Mkaazi wa muda" inafutwa na kuwa "Asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi". Aidha, marekebisho haya yatafanyika katika maeneo yote ndani ya mswada huu ambapo maneno haya yametumika.

Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri katika Sehemu ya Tatu inayoelezea Utawala wa Wakala, Kifungu cha 6, kuongezwa aya mpya ya (i) mara tu baada ya aya (h) ili kwenda sambamba na Mswada wa Kingereza itakayosomeka kama ifuatavyo:

> "(i) kumshauri Waziri na Mkurugenzi Mtendaji juu ya uteuzi wa Wakurugenzi na Maafisa Usajili wa Wakala".

Mhe. Naibu Spika, marekebisho haya katika kifungu hiki ni kutokana na kukosekana kwa aya hii katika nakala ya Mswada wa Kiswahili jambo ambalo litaleta changamoto katika utekelezaji wa sheria hii.

Aidha, katika kifungu hiki, aya (h) inabadilishwa na kuwa aya (i) na aya (i) itakuwa aya (h). Baada ya marekebisho hayo, neno "na" liliopo mwishoni mwa aya (g) linafutwa na kuwekwa mwishoni mwa aya (h).

Mhe. Naibu Spika, kamati inapendekeza kuongezwa aya mpya katika Kifungu cha 11 itakayoweza kuongeza sifa za Mkurugenzi Mtendaji ambaye atateuliwa na Mhe. Rais. Hivyo, katika kifungu cha 11(2) inaongezwa aya (d) kama ifuatavyo:

"(d) anaheshimika kutokana na mwenendo wake mzuri kwa serikali na jamii kwa ujumla".

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 17(1) Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(1) Mkurugenzi Mtendaji kwa kushauriana na Bodi atateua mtu anayefaa kuwa Ofisa wa Usajili katika kila Wilaya ya Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 17(2), neno "atakayechaguliwa" liliopo baina ya neno "mtu" na "kama" lisomeke "atakayeteuliwa". Aidha, yanaongezwa maneno "na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar". Mwishoni mwa kifungu hiki ili kuweka wazi kuwa taasisi au chuo alichosoma mtu atakaeshika nafasi iwe kinatambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika Sehemu ya Nne ya Mswada huu, inayohusiana na Usajili wa Matukio ya Kijamii kamati inashauri katika maneno ya pembeni yaliyopo katika kifungu cha 20 kinachosomeka "*Usajili wa vizazi*" kufutwa na kuandika upya kama ifuatavyo:
"Rejista la vizazi".

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 37(2) kimeshauriwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(2) Rejista litajumuisha taarifa za talaka katika mfumo utakaowekwa".

Marekebisho haya yanakusudia kuleta mantiki na kuepusha kuleta uzito katika kufahamika, hivyo, inapendekezwa kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(2) Rejista litajumuisha taarifa za talaka katika mfumo utakaowekwa".

Mhe. Naibu Spika, katika Sehemu ya Sita, kamati inapendekeza katika kifungu cha 53(2), neno "zisizozidi" liliopo baina ya neno "na" na "shilingi" lisomeke "isiyozidi". Aidha, neno "isiyozidi" liliopo baina ya neno "na" na "miaka" lisomeke "kisichozidi". Marekebisho haya pia, yanafanywa katika vifungu vidogo vya (3) na (4) vya kifungu hiki.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu wamepata fursa ya kuupitia kwa kina mswada huu, na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri serikali kuhusu utekelezaji bora wa sheria inayotarajiwa kutungwa.

Mhe. Naibu Spika, hivyo ni matumaini ya kamati kwamba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu, watauchangia, wataujadili ipasavyo na hatimae kuupitisha mswada huu kuwa sheria ikiwa ni sehemu ya jukumu la Baraza, na hatimae kuipa fursa serikali kutekeleza sehemu ya jukumu lake la utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wa uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati inawaomba waujadili kwa kina na hatimae kuupitisha kwa ajili ya kuwekewa misingi iliyo bora katika utekelezaji wake ndani ya jamii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa baada ya kutoa hii ripoti naomba na mimi nichangie dakika zangu ambazo utakazonipa, niendelee kuchangia mtu wa mwanzo.

Mhe. Naibu Spika: *Inshaallah*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, sasa hivi anaongea Nadir haongei kamati, naomba kuchangia kama mjumbe ambaye ni Mhe. Nadir na sio kamati.

Nitakuwa na mambo yangu machache ambayo nataka kuyatoa na maoni yangu katika Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar na kuweka vifungu vya Usajili na Mambo Mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningetoa tu ushauri kwa Mhe. Waziri katika kifungu Nam.53 makosa na adhabu. Kama tulivyoona hapa mtu ambaye hajasajili matukio ya kijamii kwa mujibu wa vifungu vya sheria hii atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi laki tano. Yameelezwa baadhi ya mambo hapa ambayo ametoa taarifa za uongo au ameeleza mambo ya uongo.

1. Anatoa taarifa kwa ajili ya kuingizwa katika *register*
2. Anarekebisha taarifa katika *register*
3. Anathibitisha taarifa zinazoonekana sahihi katika *register*.

Mhe. Naibu Spika, haya ni mambo mengi sana yameelezwa katika mswada huu ambayo mtu yeyote atakayekwenda kinyume na sheria na kuweza kufanya mambo kinyume na utaratibu. Mimi ushauri wangu kwa Mhe. Waziri mambo haya ni muhimu sana katika makosa na adhabu yakafanyiwa kazi. Lakini tuangalie tunapokwenda huko mbele, tungeomba sana Waheshimiwa Masheha na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na wote ambao wanaohusika kuanza na taratibu hizi za kuwapatia watu barua au vitu vyengine vyovyote ambavyo vinamuwezesha mtu kuja kumiliki *passport* au kitambulisho cha Zanzibar, au kitambulisho cha kuzaliwa au *ID card* ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi kwamba kuna fununu ambazo zipo ndogo ndogo mimi mwenyewe bado sijawa na uhakika nazo lakini zinazungumzwa kwamba inawezekana kuna watu wanamiliki kitambulisho cha Mzanzibari ambao sio Wazanzibari halisi. Sasa suala hili litakuwa kuleta madhara huko baadae kwa watoto wetu na wajukuu zetu tutakuja kufika hatua watu waliokuwa na Uzanzibari ambao si Wazanzibari halisi. Sasa maoni yangu mimi na mchango wangu kwako Mhe. Waziri lazima wawe makini sana Waheshimiwa Masheha, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya pamoja na wizarani wanaohusika na vitu hivi, wakawa makini sana kwenye kuzuia na kutowapa watu ambao hawahusiki na Uzanzibari. Hivi vitu ni vya Wazanzibari wenyewe na wafate kwa mujibu wa sheria na sisi tunataka familia yetu huko mbele inapokuja isije kukutana na matatizo na watu ambao hawahusiani na suala hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwenye mchango wangu mwengine kwa sababu kuna sheria hapa takriban tatu tunaziondosha kama ulivyosema. Sheria ya Usajili ya Mzanzibari Mkaazi ya 2005 ambayo ni kifungu 56(1), Sheria ya Usajili ya Vizazi na Vifo ya 2006 na Sheria ya Ndoa na Talaka kwa Waislamu, Sura ya 91.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningependa kwenda kwenye Sheria ya Usajili wa Mzanzibari ya 2005. Hii kwa kuwa sasa hivi inafutwa, kwa mfano tu natoa kuna vitu ambavyo nahisi havijakuwemo kwenye hii sheria mpya, lakini kule nyuma vilikuwemo kwenye sheria hizi. Mfano, kuna suala la *registration or return* hili kwenye sheria ya mwanzo imo lakini kwenye sheria mpya hamna. Sasa tuje tuangalie tu, tusijekuwa tumetoka kule tunapokwenda kwenye sheria mpya ikawa vitu muhimu tumeviacha katika maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukienda kwenye suala la Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo kuna masuala kadhaa ambayo yamo. Mfano, zamani Sheria ya Vizazi ilikuwemo sasa hivi hakuna. Vile vile kuna Sheria ya Mtoto wa Nje ya Ndoa kwenye sheria ya mwanzo ilikuwemo lakini ya safari hii sijaiona inawezekana Mhe. Waziri utakapokuja utakuja kunielekeza pengine binadamu umenipitikia.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna suala jengine vile vile kwenye sheria hii ya Usajili na Vizazi na Vifo ya 2006 tuliyoifuta zamani ilikuwa kuna cheti cha daktari kuhusu sababu za kifo, lakini kwenye sheria hii mpya sikubahatika kuiona. Sasa tuangalie tunapokwenda tusije tukachanganya vitu ambavyo baadae tutakuja kujilaumu na ningeomba Mhe. Waziri ukija uje unipe maelezo kwenye masuala haya ambayo nimeyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, lakini *concern* yangu ipo kwenye *page* 142, sehemu ya tatu kuhusu Utawala wa Wakala na Bodi ya Ushauri. Ukurasa wa 5(1) kutakuwa na Bodi ya Ushauri ya Wakala ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao.

Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mhe. Rais, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Tanzania na Wajumbe wawili ambao watateuliwa na waziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwenye *concern* hii kidogo nina wasi wasi na nina mchango wangu ambao upo zaidi kimaslahi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa suala hili linahusu Zanzibar na linawahusu Wazanzibari na sio suala la Muungano, basi mimi ningeomba huyu mtu namba (g) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Tanzania awe mualikwa na asiwe katika Bodi hii kama ilivyokuwa imewekwa, na uwalikwaji wake uwe sio wa lazima itapobidi kualikwa aje ndani ya kitengo hiki basi iwe amekuja kama mualikwa, lakini sio wa lazima.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza hivi kwa sababu Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) mimi niliwahi kuuliza swali nikajibiwa kwamba kwenye vitambulisho vya Kitaifa katika Bodi Wazanzibari wamo. Lakini *point* yangu ilikuwa sio kule kuwemo kwenye vitambulisho vile vya Kitaifa lile suala ni la lazima kwetu sisi kwa sababu ya Muungano na sisi hatufanyiwi *favor*, lazima kwenye Vitambulisho vya Kitaifa vya Tanzania tuwemo kama ni *part* ya Muungano kwa makubaliano waliyoyafanya wazee, waasisi wetu Mhe. Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Haya ni mambo ambayo lazima Wazanzibari waende, lakini hatufanyiwi *favor*. Sasa ningeomba kwenye suala hili ambalo linahusu moja kwa moja vitambulisho vya Mzanzibari pamoja na vyeti vya kuzaliwa vya kizanzibari huyu mtu asiingizwe kwa sababu bado Zanzibar wapo watu wanaweza ku-*fit* nafasi hii, hakujakuwa na umuhimu wa kufanya hivi kumuingiza mtu kutoka Tanzania Bara kama kwamba labda kutakuwa hakuna mtu wa Zanzibar.

Sasa ushauri wangu huyu mtu atolewe awekwe katika *pending*, nafasi ya kualikwa itapobidi kualikwa kama anahitajika basi aalikwe, lakini asiwemo kwenye sehemu ya tatu ya utawala wa wakala.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hili suala limefahamika mimi nitasubiri kwenye majumuisho nije nione majibu, lakini kama nilivyoeleza *concern* yangu kwamba hakujawa na umuhimu wa kuwemo mtu huyu katika Bodi hii. Ni vyema tukatafuta Wazanzibari wenzetu, ni vyema tukafanya wenyewe hizi kazi, tutapotaka jambo la ziada tutamualika mtu aje na atakuwa ni mgen wa kualikwa wa mara moja sio mtu wa kudumu katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana mimi mchango wangu ni huo, naomba kuwasilisha ripoti hii ambayo nimeichangia na nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mimi mwenyewe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf pamoja na ripoti yako uliyoitoa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni dakika 20, kwa hiyo ni matarajio yangu kwamba tutakuwa na wachangiaji labda wawili kwa kutumia dakika kumi, kumi, naanza na Mhe. Simai Mohammed Said na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nianze na mimi kwa kumtanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa nafasi leo sote kufika hapa na kuweza kutimiza majukumu yetu. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu niweze kutoa mawazo yangu na kuweza kuchangia huu mswada wetu leo ambao unahusiana na masuala ya kuanzisha wakala wa usajili wa matukio ya kijamii hapa kwetu Zanzibar.

Pia nitoe pole kwa wapiganaji wetu, mashujaa wetu na hasa kwa familia zao, ndugu na jamaa kutokana na msiba mkubwa uliowakuta pamoja na hawa wote ambao wamefariki huko *DRC* na wengi ambao wanatoka katika nchi yetu ya Zanzibar, basi *inshaallah* Mwenyezi Mungu atazipa nguvu familia zao waweze kuwa na moyo wa subra. *Innalillahi Wainna Ilayhi Rajiun.*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nataka niseme mawili matatu wakati nikitumia muda wangu kuendelea kuchangia mswada huu. Mhe. Naibu Spika, juzi tarehe 8 Mhe. Waziri anayesimamia masuala ya utalii ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameunda kamati ya watu nafikiri wanaozidi kumi kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakusudia Tanzania Bara, ambapo watu hawa watakuwa wanasimamia au hii kamati imeitwa Kamati ya Kitaifa ambayo watakuwa wanasimamia utambulisho wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nisikitike sana baada ya kuona majina katika ile kamati hapakuwepo mtu yeyote kwa upande wa pili wa Muungano ambayo ni Zanzibar, na hasa katika jambo ambalo linagusa uchumi wetu ni suala la utalii. Waziri wa Utalii wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameamua kwa nafsi zake, kwa uwezo wake mwenyewe kutaka sisi Wazanzibari tutambulike vipi nje ya Jamhuri au sisi Wazanzibari tuwe tunajiuza katika soko letu au kutambulika katika suala la utalii huku akifanya kwa makusudi kuidharau wizara yetu, kutotambua serikali yetu, kutotambua Mahakama zetu pamoja na mengineyo yote.

Kwa hiyo, niseme tu hasa baada ya kutangaza hiyo kamati tarehe 8 akaamua tena kuungaunga siku ya Jumapili (jana) kuongeza majina matano ya Wazanzibari. Majina haya ya Wazanzibari

watano sidhani hata kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajua habari hiyo, ameamua yeye mwenyewe kuwateuwa juu ya hiyo kamati ya kitaifa. Sasa mimi nataka niseme vitu viwili, mwenendo wa Mawaziri wanaosimamia masuala haya kwenye Serikali ya Muungano wanapokuja kusimamia kazi hasa za nchi kuishia maeneo kama Serena kulala na kuondoka na kusema kwamba wao Zanzibar wanaijua kama huyu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hamisi Kigwangalla basi mwisho wao kamati hii itakuwa ni Chumbe.

Mimi naishauri serikali hawa vijana au watu walioteuliwa watano wengine Wazanzibari bila kuhusisha wizara yetu ya Zanzibar wasiende, wasishiriki wala wasitambuliwe. Kwa sababu suala la kuisema Zanzibar tutaitangaza vipi nje ya nchi mambo haya yako chini ya SMZ. Wizara yetu ipo, Baraza la Wawakilishi lipo kushauri, Rais wetu yupo, Mawaziri wapo na Mahakama zetu zipo. Kwa hiyo, hawa watu walioteuliwa wote ambao wamewekwa katika majina yao basi hiyo kamati ibakie Tanzania Bara sisi kwa upande wetu tujipange wenyewe, kama tumeamua kujiita *The Spice Island of Zanzibar* hii ni historia yetu tujipange sisi wenyewe, kama tumeamua tunataka tujiuze katika masoko tofauti ili utambulisho wetu uwe ni tofauti basi ni maamuzi yetu. Waziri wa Maliasili na Utalii wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hana mamlaka yoyote yeye kutuamulia sisi Wazanzibari jinsi gani tutambulike nje.

Kwa hiyo, naomba hizi salamu zimfikie yeye, Mwanasheria Mkuu yupo hapa na Mawaziri wote wamenisikia vizuri, wasikubali mambo ambayo hayamo katika maeneo ya Muungano, watu kupora madaraka haya halafu wao kuamua nani ataingia na kuteuwa majina huku wakimdharau Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar. Kwa hiyo, Dkt. Kigwangalla na kamati yake waishie Chumbe wasije kabisa huku Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niendelee sasa kuuchambua huu Mswada. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika kifungu nambari moja juu ya utangulizi, sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio wa Kijamii ya Mwaka 2017. Lakini ukiangalia kwenye kifungu hiki kinasema waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali, hajatoa muda.

Mhe. Naibu Spika, hapa ningeshauri Waziri aiangalie kwa sababu humu ndani kuna masuala ya *penalties*, kama muda hamna basi lazima hawa watu watahitaji muda. Kwa hiyo, hapa *registrar* ajipange vizuri kuangalia ni muda gani Waziri atatangaza ili ile sheria inapotangazwa sasa iwe tayari *registrar* ameshajipanga pamoja na mawakala wake wote.

Pia katika Sehemu ya Tatu juu ya Utawala wa Wakala, kifungu nambari 5. Ukiangalia katika muundo wa Bodi ya Ushauri ya Wakala utakuta kwamba kifungu (a) 'Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais', lakini pia ukiangalia katika kifungu hicho hicho nambari 5(3) kinasema "Katika kuteua Wajumbe wa Bodi, Waziri atapaswa kuzingatia jinsia, kada na ujuzi".

Mimi nashauri hapa na elimu iongezwe, kwa sababu unaweza kuteua mtu yeyote lakini ukiangalia madaraka ambapo kazi inayotaka kufanywa na wakala bodi inakaa nafasi kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nashauri hapa Waziri anapaswa kuzingatia suala la elimu pia katika kumshauri Mhe. Rais juu ya suala zima la kuwa nani atakuwa mwenyekiti wa hiyo wakala.

Mhe. Naibu Spika, pia ukienda katika kifungu nambari 17(2) juu ya uteuzi wa maofisa wa wakala katika afisa usajili katika kila Wilaya za Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kifungu kidogo cha (2) kinasema:

> "Hakuna mtu atakayechaguliwa kama Ofisa wa Usajili isipokuwa awe angalau na Digrii".

Sawa ni sahihi kwamba elimu ni suala la msingi, lakini ukiangalia sasa hivi hizi Halmashauri zetu na maeneo yote tuna watu ambao tayari wana uzoefu, wapo na inawezekana watu hawa sasa wakawa hawana *degree*. Sasa mimi ningependa kufahamu Mhe. Waziri katika hawa watu ambao tayari wanatumika kufanya hizi kazi na wana uzoefu zaidi ya miaka 10 inawezekana kuwa hawana *degree*, sasa hawa watu tutawapeleka wapi au patakuwa pana *relay*? Yaani kwamba huyu ataondoka atafanya ile kazi halafu baada ya muda fulani atamuachia, halafu huyu utampeleka kutimiza majukumu mengine, kwa sababu na uzoefu unahitajika. Inawezekana mtu amemaliza chuo ana *degree* yake lakini ukimtupa katika sehemu ya kazi basi mambo yakawa tofauti. Kwa hiyo, mimi ningependa kufahamu hawa ambao wana *experience* katika maeneo tunafanya kitu gani.

Ukienda katika kifungu cha 22(1) "Kutokana na taarifa za kizazi, itakuwa ni wajibu kwa watu wafuatao kutoa taarifa:..."wametajwa baba, mmiliki wa nyumba na wengineo.

Ukiangalia kifungu (c) kuna mtu mwenye dhamana ya mtoto halafu pale pana neno 'na'. Sasa baada ya ile 'na' nashauri iondoke ije 'au'. Kwa sababu ukiangalia 'na' na 'au' ni vitu viwili tofauti. Kwa hivyo, iseme kwamba 'mtu mwenye dhamana ya mtoto au mtu aliyemuokota mtoto'

Halafu ukija katika kifungu nambari 26(1) juu ya suala la kutoa cheti cha kuzaliwa. Mhe. Naibu Spika, vyeti kwa kweli sasa hivi ukiangalia ni mtihani mkubwa sana, wananchi wanapata tabu sana katika suala zima unaweza ukachukua miezi miwili au mitatu cheti hujapata. Hii ndio hali ilivyo huko mitaani. Sasa mimi nashauri pawekwe muda maalum kwamba Mkurugenzi Mtendaji au mtu aliyekasimiwa madaraka baada ya kupokea taarifa ya kizazi na kuridhika na taarifa hizo atatoa cheti cha kuzaliwa kutokana na kumbukumbu zilizopo katika ofisi kwa muda usiozidi mwezi mmoja, ili tayari huyo mtu awe tayari haki yake ameipata.

Mhe. Naibu Spika, ukienda pia katika kifungu cha 35(1) kinazungumzia suala zima la usajili wa ndoa. Mheshimiwa kwa kweli kifungu hiki kimenipa mtihani, kinasema wanandoa ambao sheria hii inafanya kazi watafika katika Ofisi za Wakala ndani ya siku 14.

Mhe. Naibu Spika, leo umeowa unaambiwa baada ya siku 14 uwe tayari wewe umeshakwenda kusajili ndoa yako. Mheshimiwa kuna kipindi cha *honeymoon*, kuna kipindi cha furaha cha wanandoa, kuna kipindi cha wanandoa wanasafiri kwenda nje kupumzika. Sasa mimi nashauri hapa pasemwe hivi, "Wanandoa ambao sheria hii itafanya kazi ikiwa ndoa yao wameifunga ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au ndani ya Zanzibar kwa muda wa miezi mitatu watatakiwa tayari wawe wameshasajili ndoa yao. Kwa wale ambao wamefunga ndoa yao nje ya visiwa vyetu vya Zanzibar au nje ya Jamhuri, basi isizidi miezi sita".

Mhe. Naibu Spika, leo kuna watu wanaondoka Zanzibar wanakwenda kusoma nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanakwenda Urusi, Brazil, China, hao wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu wakapendana huko wakaamua kufunga ndoa unawaambia katika siku 14 wawe ndoa yao wameshaisajili itakuwa huwatendewi haki, basi tuwawekee muda maalum katika muda usiozidi miezi sita wawe tayari wameshasajili ndoa zao. Maana yake tunasema hapa kwamba sio kama ndoa hizi zitakuwa ziko nyingi, lakini angalau katika muda wa miezi sita karatasi zao watakuwa wameshazisimamia, wameshazileta katika balozi husika na ndoa zao wameshazisajili.

Pia nataka niseme kitu kimoja, katika hili suala la usajili wa ndoa. Hapa tuna raia wengi sana wa kigeni wanakuja kufunga ndoa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri aliangalie sana katika suala zima hili juu ya mapato na usajili wao wa ndoa katika hao wataokuja kusimamia katika maeneo yote ya Wilaya, hasa hawa ambao watakuwa ni maafisa wao wakuu katika Wilaya zetu wanakwenda sambamba na sheria hii na pia kuweka heshima na kutoa hivyo vyeti kwa raia hao wanaokuja kufanya ndoa zao ambao sio raia wa hapa Zanzibar.

Lakini tukenda katika kifungu cha 48. Mheshimiwa katika kifungu hiki kinamtaka Waziri ndani ya miezi mitatu baada ya kumaliza mwaka wa fedha, atawasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi taarifa ya fedha ya mwaka ambao inajumuisha mambo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika 3(c) inamtaka Waziri alete ripoti ya taarifa ya ukaguzi wa fedha. Leo ukimuangalia *CAG* yuko miaka miwili nyuma anafanya hiyo *audited report.* Ukienda katika ile sheria ambayo ilipitishwa ya *ZAWA* walitakiwa walete *auditor report* hapa mpaka leo haijaletwa kwa sababu bado haijafanyiwa *auditing* na *CAG*. Hiki kifungu cha (c) kiondolewe na Mhe. Waziri hakitekelezeki. Kwa sababu ukisema ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha hutakuwa na *audited report.* Kwa hiyo, kifungu hiki kiondoke.

Leo tumeona katika sheria ya *ZAWA* wanatakiwa walete *audited report* hazijafika mpaka leo, leo sisi tunaangalia hesabu za miaka miwili mpaka mitatu nyuma. Kwa hiyo, mimi nashauri kifungu cha 48(3)(c) kiondoke.

Pia ukienda kwenye kifungu cha 51 ukiangalia usajili kwa mujibu wa sheria hii utafanyika kwa malipo ya ada kama itakavyoelezwa kwenye Kanuni. Mhe. Waziri namuomba hapa aweke maneno yafuatayo, kwamba hapa uongeze suala la hali halisi ya maisha ya Wazanzibari itazingatiwa, sio tena fedha zinaanza kupangwa katika suala zima la usajili inageuzwa sehemu ya mapato *rather than* sehemu ya *registration* na kumtambua mtu. Maana yake tumeona kwenye suala la kutoa *license* sasa hivi kila Wizara inaigeuza sasa sehemu ya kutoa *license* inafanya sehemu ya kupata mapato, nafikiri mwaka ujao kwenye bajeti nitalizungumzia kwa undani suala hili na njia ambayo tunakwenda sio sahihi.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, nashauri sana suala la usajili lizingatie hali halisi ya maisha na alisimamie mwenyewe Waziri kwa kusaidiana na Bodi ili inapotangazwa wasitoke maafisa wake tu wa wilaya, kutokana na masuala ya ugatuzi wakapora mamlaka yake wakatangaza kwamba, katika kila maeneo tunayoingia bei inakuwa ni hii.

Mimi baada ya hayo na baada ya kuyapitia katika maeneo yote nimpongeze sana Mhe. Waziri kwamba Mswada huu wa Sheria wa Kuanzisha Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii ya

Zanzibar ni mzuri. Mimi naunga mkono hoja haya mashauri niliotoa nitasubiri Mhe. Waziri akifanya majumuisho anipatie majibu mazuri, pia naomba salamu nilizomtolea Mhe. Waziri Kigwangalla zimfikie vizuri.

Baada ya hapo naunga mkono hoja nitasubiri majibu kama nilivyosema.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na pia niwashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Nabu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said. Waheshimiwa Wajumbe nilitangaza jina la Mhe. Ali suleiman Ali, lakini kutokana na muda naona ataendelea jioni. Kwa hivyo, ataanza Mhe. Ali Suleiman Ali na baadae atafuata Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuata Mhe. Mohamed Said Mohamed na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Said Soud Said (MBM). *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe mpaka hapa tumefikia mwisho wa kikao chetu cha asubuhi hii. Kwa hiyo, nasitisha kikao hiki hadi jioni saa kumi na moja. Nawashukuru sana.

(Saa 6:58 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Utaratibu

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante kanuni wa 63 maelezo binafsi ya Mjumbe kifungu cha 45. Mjumbe yoyote anaweza kwa kibali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio ya shughuli ambayo imewekwa na kanuni ya 27. Na *concern* yangu binafsi ambayo imejitokeza katika jamii ningeomba kidogo nizungumze kwa kupitia kupitia kanuni hii.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekufahamu Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy kwa vile umesema Mjumbe yoyote kanuni ya 45 anaweza kwa kibali cha Spika, kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambazo zimewekwa na kanuni ya 27. Hii Kanuni Mheshimiwa imejieleza kuwa kwa kibali cha Spika na Spika ni kiti cha Uspika kwa hiyo, nakuomba Mhe. Nadir Abdul-Latifu Yussuf Al-Wardy nimekuelewa *concern* yako, lakini naomba tuendelee na taratibu ambazo zimewekwa nitalitafutia ufumbuzi baadae suala lako. Naomba tuendelee.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Mohamed Said Mohamed ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa laasiri hii kuipata nafasi hii ya kuchangia mswada huu muhimu wa Sheria ya

Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matokeo ya Kijamii Zanzibar na kuweka vifungu vya usajili na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri na serikali yote kwa jumla kwa kuhakikisha kwamba suala la usajili ni jambo muhimu sana katika nchi na usajili ni suala muhimu kwa kuwa utakuwa na vielelezo muhimu vya kuhakikisha kwamba lolote unalolifanya na likitakiwa linapatikana kiurahisi.

Kwa hivyo, nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hii kwa kuhakikisha kwamba mswada huu umekuja wakati unaofaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu kuna mambo 5 muhimu.
(1) Vizazi
(2) Kadi za Utambulisho
(3) Ndoa
(4) Talaka
(5) Vifo

Lakini katika yote nayachukulia uzito wa kwanza vizazi, kadi za utambulisho na hii kifo ambacho hichi huwa uwezo nalo lazima yatokee kama tulivyozaliwa na tutarudi tu. Lakini ndoa na talaka tutaomba sana itokee nasaha zaidi kwa sababu Mwenyezi Mungu hapendi kuona na kuachana, lakini inapobidi tena mambo ya Mwenyezi Mungu hayazuiliki kama nilivyosema mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika muelekeo wangu wa kuchangia mswada huu nitakuwa na sehemu chache sana. Lakini uzito wake nafikiri tutapata maelezo mazuri kwa Mhe. Waziri kama ulivyokuja mswada huu mzuri naamini kama kuweka nyongeza tu.

Sehemu ya 4 ukurasa wa 146 Usajili na matokeo ya Kijamii. Mhe. Mwenyekiti (a) Vizazi katika kitu muhimu sana Mheshimiwa usajili wa vizazi ni jambo muhimu sana na usajili ni kitu kimoja wapo ambacho mtu akizaliwa lazima apate usajili unaokubalika au *register* inayokubalika ili kuwemo katika orodha ya kuwa huyu alizaliwa tarehe fulani siku fulani ikiwezekana hata wakati fulani kwa sababu pia changamoto najua historia katika mtu kuzaliwa, kazaliwa wakati gani saa ngapi nzuri lakini si tatizo. Mimi nachukulia hili hili tu kwamba hili ni suala muhimu na linafaa hasa tukizingatia pana vidudu watu wengi sana hapa au vidudu mtu wanaosababisha kubadilisha badilisha tarehe za vizazi vyao au wanapozaliwa watu wanabadilisha tarehe zao baadae inakuwa matatizo katika maisha yanayoendelea.

Kwa hivyo, mimi ombi langu moja kwa wizara pamoja na mswada huu umeletwa vizuri na nahakikisha umepangika vizuri na utakuwa na umadhubuti mzuri niombe sana walengwa au wadau wanaohusika na msawada huu wawe waadilifu sana. Uadilifdu ni jambo la mwanzo na uadilifu ndio litatupa fursa nzuri ya kuhakikisha kwamba kizazi kile kinapata kuhakikiwa vizuri na kinasajiliwa vizuri ili kuondokana na mtafaruku wa baadae.

Jengine Mheshimiwa tunakumbuka huko nyuma tunakotoka mpaka sasa hivi, lakini nakumbuka zaidi huko nyuma tulikotoka hapa katikati sijui paliingia nini. Mtoto anazaliwa kijijini au anazaliwa sehemu yoyote Sheha ni mtu wa mwanzo anaepata taarifa na ni mtu wa mwanzo anaepokea taarifa ile wakati mwengine akishazaliwa mtoto, hata kama kazaliwa hospitali kama inavyoeleza hapa lakini Sheha ndie mwenye kumbukumbu ya mtoto yule katika eneo lile.

Kwa hivyo, mimi naomba tu hili Masheha wetu kama mswada huu ulivyosema wamepewa uwezo lakini uwezo huo uongezeke kwanza wao ni watu mwazo kupelekewa taarifa ya kizazi kile na kupelekwa panapohusika.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza mswada huu vile vile kifungu cha 2 Usajili na vizazi 21, (2) mzazi, mlezi au mtu aliyekuwa na dhamana na mtoto mara tu baada ya kuzaliwa mtoto au kumpata mtoto atamjulisha Afisa Msajili au Sheha kwa ajili ya kusajiliwa kizazi hicho. Nafikiri hii ni sawa sawa haina tatizo.

Lakini jengine nililoligundua hapa Mhe. Mwenyekiti, kuna mtoto aliyezaliwa kwa matokeo mbali mbali kwa bahati yule mtoto aliezaliwa ulikuwa utaratibu wake haufahamiki. Kwa hivyo, tukaambiwa tu kwamba ili ipatikane taarifa nakuja kwenye ukurasa wa 147 kifungu cha 24 Usajili wa mtoto alieokotwa. Hapa tunaelezwa tu mtu aliemuokota mtoto ambaye wazazi wake hawajulikani au mtu ambaye aliyepewa mtoto kumtunza atapaswa kutoa taarifa hiyo mara tu katika kituo cha Polisi kilicho karibu au Shehia.

Mimi nafikiri narudia pale pale Mheshimiwa mtu wa mwanzo Sheha kwa sababu Sheha ndiye yuko karibu na yule mtoto alipo siku nyengine mtu yuko kijijini sehemu mbali na polisi iko mbali itakuwa ni muda mrefu wa kufatilia, lakini Sheha akishapokea taarifa ile yeye ndie atakaetoa taarifa polisi na mtoto yule kupelekwa pahala panapohusika ili kama kifungu cha pili kilichosema katika sehemu ya Ustawi wa Jamii.

Mimi hili nalipongeza kwa sababu pia panatokea baadhi ya watoto masikini ya Mungu wanaokotwa humu na watoto wale wakishaokotwa inatokea mazonge ya hapa na pale. Lakini kwa dhati kabisa niipongeze Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake, Watoto, Wazee na Vijana kwa kazi nzuri inapotokea taarifa kama hizi wao wa mwanzo wanafika na kuhakikisha mtoto yule anachukuliwa kwa kustiriwa na kuweka mpaka ipatikane hatua ambayo ya mwisho. Lakini niseme tu kwamba ni vyema lolote linalotokea katika jamii katika maeneo yetu Sheha awe ni mtu wa mwanzo kupata taarifa ile na yeye aipeleke panapohusika, huo ni ushauri.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo suala la kadi za utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, suala la utambilisho katika nchi yoyote ni mihumu sana na utambulisho ni alama ya kuwa wewe unajulikana unatoka wapi, uko wapi na kuna mambo mengineyo ambayo inakubidi uyapate. Kwa hivyo, hili ni suala zuri lakini kwa bahati nzuri tumepata marekebisho lakini marekebisho mimi hayanihusu sana kwa sababu mswada wangu nilikuwa nimeshautayarisha ndio haya haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 148 kifungu cha 27 *register* ya utambulisho.

(1) Wakala itaanzisha *register* ya utambulisho kwa ajili ya usajili wa utoaji kadi za utambulisho.
(2) Watu wafuatao watasajiliwa na wakala huo.
(a) Mzanzibari Mkaazi
(b) Mkaazi wa Muda aliye chini ya Sheria ya Uhamiaji ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
(c) Mkaazi wa muda ambaye hayumo chini ya Sheria ya Uhamiaji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa aifafanue vizuri kwa sababu hili ni zuri Mzanzibari Mkaazi anajulikana mimi nipo hapa ni Mzanzibari Mkaazi. Lakini kuna wengine Wazanzibari wanaoishi nje ya Zanzibar au anaeishi nje ya eneo lile lakini Mzanzibari tu. Kwa hivyo, ili kuondoa tatizo la baadae kwa sababu kuna malalamiko kwa watu wengi kadi zao kuna kadi za aina mbili kuna Mzanzibari Mkaazi na Mzanzibari. Sasa haya mambo mawili namuomba sana Mhe. Waziri akija alifanunue uzuri ili kuna baadhi ya watu ambao wana madai ya hapa na pale wajue ukweli wenyewe uko wapi. Kwa hivyo, mimi napongeza sana hili suala ambalo liko wazi kabisa na naamini kwamba hili litatupa muelekeo mzuri wa kujua vipi tunavyoishi katika nchi yetu.

Lakini kifungu cha 28 pia aina ya kadi za utambulisho zimeeleza haidhuru tena Mheshimiwa atajua mwenyewe mbinu zake. Kutakuwa na kadi za aina mbili ndio hizo hapo za utambulisho kama ilivyoelekezwa na wakala kuhusiana na kwanza:

(a) Mzanzibari na Mkaazi wa muda.

Ndio nikasema hapa kidogo hapana tatizo lakini Mheshimiwa nitamuomba sana kifungu hichi akifafanue ili kiwe wazi kabisa.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, kutokana na shughuli zetu mbali mbali ambazo tunakwenda nazo kuna masuala ya ndoa. Ndoa ni jambo la suna na ni jambo la lazima sana kwa kila mwenye uwezo aowe na aolewe. Lakini tuna mambo mengi ambayo yamejitokeza hapa nyuma, leo kama sikosei Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis aliuliza suala zito sana. Aliuliza hii Mheshimiwa siingii katika mambo ya kadhi lakini naelezea hali halisi tu. Alielezea kwamba kuna wanawake wengine wanakuwa na kesi zao mbali mbali na kesi zile zinapofika Hakimu anaamua anavyotaka yeye siku nyengine, siku nyengine kwa shemegi yule kumtaka yeye sijui inakuwaje? Siku nyengine huyu katoka kwa Shihata huyu ngoja nimfanyie mbinu Shihata ana utani wa hapa na pale basi huchukuwa talaka nenda zako siku ya pili anamuoa yeye.

Mhe. Mwenyekiti, haya yapo na tuseme tu kwamba kama kuna sheria hii ya ndoa na talaka naunganisha hiyo Mheshimiwa lazima pawe na kitu madhubutu sana na tuwe wakali sana kwa sababu kuna kesi nyengine zinavunjika kutokana na misingi ambayo haieleweki kuna kesi nyengine zinavunjika kutoka na utashi. Kwa hivyo, hapa pana ampango mzuri ambapo patakuwa na mtu anahusika hasa moja kwa moja Mkurugenzi aangalie uwezekano wa kutoka talaka na talaka ile ikitoka iwe na msingi wa kutoka talaka ile. Mimi kwa mawazo yangu hata kama itakwenda kwa kadhi basi kwanza Mkurugenzi anaehusika aifatilie talaka hiyo mpaka ijulikane mwisho.

Lakini vyenginevyo Mheshimiwa tunapokea malalamiko mengi na malalamiko hayo mtu siku nyengine katokewa na usumbufu fulani kenda na biashara zake nje huko kazongwa au kapaparika na mambo mengineyo, akirudi hapa mke wake anamwambiwa umenikimbia muda wa miezi miwili wewe hujanipa kitu mimi nimeshaachwa. Ile inakuwa inakuwa ni kinyume. Kwa hivyo, mswada huu ni mswada wa sheria lazima sheria tuiheshimu. Hatuingilii mambo ya dini tunaingilia talaka na mambo mengineyo.

Lakini jengine Mheshimiwa nitalolizingumza hapa kwa ufupi na la mwisho kwa sababu mswada huu nimeukubali sina mengi sana nitasema tu kwamba mambo ya vifo. Mhe. Mwenyekiti, nimetanguliza mwanzo kusema kwamba kifo ni jambo la lazima faradhi huwezi kukimbia na kifo ni jambo la mwisho. Kwa hivyo, ili kuweka kumbukumbu sahihi lazima baada ya kuzaliwa tumesema utaishi lakini utakufa.

Kwa hivyo, madhali umezaliwa mwisho wako kifo basi ile taarifa iwepo nzuri na ikae katika pahala pa kumbukumbu nzuri ili ieleweke tu kwamba fulani alifariki kutokana na moja, mbili, tatu lakini kafariki na hati yake hii hapa. Sababu ya msingi ya kusema hilo Mheshimiwa kuna watu wengine humu wanaweza kusingiziwa wamekufa kuna mzozo siku nyengine inatokea mizozo fulani mtu anasingiziwa aah fulani kafa bwana kumbe yule mtu hakufa. Lakini pakiwa na uthibitisho na naamini pakitokea kifo mtu wa mwanzo Sheha, Sheha ndio anaepokea taarifa zile na Sheha atapajua yeye pa kufikisha ile taarifa ya kifo ili twende vizuri katika kuweka vizuri mswada huu.

Lakini la mwisho kabisa niseme tu Mhe. Mwenyekiti kwa dhati kabisa naipongeza wizara kwa kuchukua jukumu hili zito na kuhakikisha kwamba jukumu hili ni roho yetu. Hii ni roho kwa mambo yote matano niliyoyataja vizazi, kadi za utambulisho, ndoa talaka na vifo. Kwa sababu hili ndilo litakalotuondolea utata unajiotokeza mara kwa mara katika mambo mbali mbali ya kuishi maana huu utambulisho huu ni jambo la msingi na ni jambo la mwanzo ambalo zito na la muhimu ili kuhakikisha kwamba tuko salama katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa baada ya hayo machache nasema mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijito Upele mswada huu nimeupokea na nimeukubali asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Said Soud Said ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu muhimu ambao una lengo la kuweza kuanzisha wakala wa usajili wa matukio haya ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuishukuru na kuipongeza sana wizara ambayo inahusika na masuala haya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa kuweza kuandaa mswada huu muhimu ambao umekuja wakati muafaka kutokana na changamoto mbali mbali ambazo zimeweza kujitokeza.

Lakini vile vile niipongeze kamati ya Sheria, Utawala na Idara Maalum kwa ripoti yao ya mapendekezo ya Marekebisho ambayo imesomwa na Mheshimiwa Mahiri Mhe. Nadir Abdul-Latif wa Jimbo la Chaani kwa umahiri mkubwa.

Lakini nichukuwe fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwapongeza wale wote ambao wameweza kuchangia hotuba hii vizuri na hususan Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Nadri Abdul-latif pamoja na Mheshimiwa aliyetangulia hivi punde.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili umekuja wakati mufaka sana, pamoja na kwamba chimbuko lake lilianza nyuma kidogo kama miaka mitano nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba suala la usajili wa matukio ya kijamii pamoja na vitambulisho kwa kiasi kikubwa lilikuwa na changamoto nyingi hapo nyuma, kuliko na changamoto kubwa ya ucheleweshwaji wa vyeti za kuzaliwa, vyeti vya vifo. Lakini kuna changamoto kubwa vile vile ya suala la talaka vyeti vingi vya talaka nafikiri havisajiliwi vizuri. Lakini vile vile kuna wajane wengi ambao wamecheleweshewa vyeti vyao vya talaka. Kwa hiyo, hapa nafikiri mswada huu utakuwa ni channgamoto sana kwa sisi wanaume tunaowacheleweshea vyeti vya talaka wake zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo la vitambulisho vya ukaazi. Kuna vitambulisho feki vingi, kuna vyeti vya kuzaliwa vingi ambavyo vimetoka. Kwa hiyo, nina imani kwamba kuanzishwa kwa sheria hii itakuwa ni muarubaini wa kuweza kuondosha changamoto mbali mbali ambazo zilikuwa zinahusika na masuala haya ya usajili wa matukio mbali mbali ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mswada huu unafuta sheria karibu tatu, na kwa kuwa mswada huu unagusa kila mtu katika jamii. Unamgusa mtoto aliyezaliwa, wazazi wake, wenye kufanya ndoa mke na mume, vile vile Wazanzibari wakaazi. Ni muhimu sana baada ya sheria hii kupita basi niombe sana wizara inayohusika kuweza kutoa taaluma kubwa sana kwa jamii yetu ya Zanzibar. Kwa sababu unapofuta sheria maana yake unaanzisha sheria mpya, basi ule uelewa unatakiwa uwe mkubwa sana kwa jamii. Kwa sababu watu wengi itakuwa wamezoea sheria ambazo zimepita na hivi sasa kuna sheria mpya ambayo ndani yake inaambatana na adhabu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika waraka wenyewe sehemu ya kwanza, niombe tu au nikumbushe suala la kuyaweka maelezo au maneno ya ufafanuzi katika alfabeti. Lakini ukurasa wa 141 katika kifungu cha 4(i) mstari wa pili kuna neno "mifumo ya". Katika "mifumo ya" lilitakiwa liwepo neno "taasisi za kiserikali." Kwa hiyo, napendekeza na ndivyo ilivyo hilo neno "taasisi za" liingie baina ya neno "ya" na "serikali".

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 143 kifungu cha 7. Kwanza nishukuru sana mapendekezo ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) ambayo ameyatoa marekebisho katika jadweli yake ambayo ilisambazwa asubuhi kuhusu suala zima la bodi. Lakini napenda sana nipendekeze marekebisho ya neno la pembeni katika kifungu hicho 7, badala ya "Muda wa Bodi" lisomeke "muda wa Wajumbe wa Bodi".

Vile vile kifungu cha 8 katika masuala yanayohusiana na bodi, Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) alipendekeza mambo mawili ambayo yapo katika waraka wake. Alipendekeza suala zima la akidi ya kikao, vile vile alipendekeza suala la kumualika mtu ambaye anaweza kuisaidia bodi. Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi naendelea kupendekeza suala zima la kumbukumbu za mikutano ya bodi ambalo halipo, vile vile kuweka bayana maslahi binafsi halipo, lakini Katibu wa Bodi, nafasi ya Mjumbe wa Bodi baada ya nafasi kuwa wazi. Vile vile suala la kujiuzulu kwa Mjumbe wa Bodi. Mhe. Mwenyekiti, ningependa vipengele hivi Waziri avitazame ili viingie katika maeneo hayo ya bodi kama ilivyo katika miswada mingine.
Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10 katika maelezo kuna neno mstari wa pili ambalo linasomeka "kama Waziri" napenda niinukuu. "Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wengine wa bodi watalipwa posho na mafao kama Waziri." Hilo neno nafikiri limeingia kwa makosa. Naomba *statement* yote hiyo ibadilike na isomeke kama ifuatavyo:

"Wajumbe wa Bodi watalipwa posho na mafao mengine kama itakavyopangwa na Waziri kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha atakavyoidhinisha muda hadi muda".

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa ukurasa wa 144 katika kifungu cha 12. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 imeelezewa sifa za Naibu Mkurugenzi. Sifa hizi ambazo zimefanyiwa marekebisho kidogo na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) ningependelea kwamba sifa za Naibu Mkurugenzi ambazo zipo sawa sawa na sifa za Mkurugenzi Mtendaji, basi katika kifungu cha uzoefu kifungu cha (c) napendekeza kwa Naibu Mkurugenzi basi badala ya miaka 10 iwe miaka 7. Kwa sababu haipendezi sana sifa za Mkurugenzi Mtendaji na sifa za Naibu zote kuwa sawa. Kwa hiyo, pendekezo langu ni hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 145 kifungu cha 14 napenda kutoa mapendekezo katika neno la mwisho la *statement* ya juu namba moja ambayo inasomeka "Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na uwezo wa". Nilikuwa napendekeza isomeke hivyo kuwe na neno "wa".
Halafu kifungu kidogo cha (a) neno ana uwezo liweze kuondoka. Kwa sababu ukishaweka hapo "uwezo wa", ina maana itaendelea kuonekana "uwezo wa kipekee" na vyengine vitakuwa vipo sawa.

Lakini katika kifungu cha (c) ambapo pana neno kumwita nilikuwa napendekeza isomeke kumwita kwa maandishi. Na hii vile vile ni kutokana na ile *version* ya Kiingereza ambapo kwa tafsiri yake basi isiwe wazi kama ilivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 146 nilikuwa napendekeza katika kifungu cha 48 ambacho kinasomeka hivi:

"Bodi kulingana na matakwa ya sheria ya utumishi inaweza kuajiri idadi ya wafanyakazi kadri itakavyoona sawa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za wakala."

Mhe. Mwenyekiti, haipendezi sana kuweza kuona kwamba bodi imeachiwa kila kitu. Nilikuwa napendekeza isomeke kwamba bodi kwa kuzingatia mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji, ni vyema sana bodi iweze kuzingatia mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji kwa sababu yeye ndiye mwenye taasisi na yeye ndiye anayetangulia kuweza kuona umuhimu wa kuwa na watumishi wa aina fulani. Kwa hiyo, badala ya kuipa bodi moja kwa moja mamlaka, bodi iweze

kuzingatia na kupendekeza bodi kwa kuzingatia mapendekezo ya Mkurugenzi Mtendaji ndio iweze kufanya maamuzi haya.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 117 kifungu cha 13. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili ambalo limezungumziwa ikiwa kizazi kimetokea kwenye chombo cha abiria, kwenye chombo cha usafiri katika bahari ya Zanzibar. Kwa mujibu wa kutoa taarifa, wajibu wa kutoa taarifa utakuwa kwa Nahodha Mkuu wa chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vyetu vinasafiri hata katika bahari nje ya Zanzibar. Hata katika meli zetu, meli yetu hivi sasa inakwenda mpaka Comoro. Sasa inaweza ikatokea kwamba mtoto kazaliwa ndani ya meli na aliyemzaa ni Mzanzibari lakini ipo nje ya bahari ya Zanzibar. Ningependa sana iweze kuangaliwa hii kwa sababu imeangalia zaidi eneo la Zanzibar lakini meli zetu zinasafiri katika sehemu mbali mbali. Nyengine zinakwenda Mtwara inawezekana ikatokea hivyo. Kwa hiyo, napendelea kwamba kifungu hicho, vile vile kifungu cha 23(2) ambacho kina mazingira ya aina hiyo nacho kiweze kutazamwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nije sasa ukurasa wa 151 katika suala la talaka. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 40(2) cheti cha ndoa isomeke cheti cha talaka. Lakini hata lile neno la pembeni wenzangu naona kama wameshalirekebisha kwa hiyo lipo sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia zaidi ni kwamba suala zima la usajili wa matukio ya kijamii ni suala muhimu sana ambalo linahitaji taaluma kubwa sana kwa sababu changamoto nyingi zimeweza kujitokeza. Kwa hiyo, ni vyema suala hili nasisitiza tena ni kwamba liweze kutolewa elimu kwa mapana zaidi kwa jamii ili kuweza kuepusha makosa mbali mbali ambayo yalikuwa yanatokea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nichukue fursa hii ya kuweza kuwataka Wajumbe wenzangu kuweza kuichangia na hatimaye kuweza kuupitisha mswada huu muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa letu. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na atafuatiwa na Mhe. Waziri Soud Said Soud na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajiandae.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana. Vile vile nimuombe Mwenyezi Mungu sana anijaalie nikiwa nachangia hotuba hii nisiwe na tambo, jazba wala kiburi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja kwa wakati sana, mswada huu ni mzuri na ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe nimeleta baadhi ya *schedule of amendment* na mmezipata naomba mniunge mkono sana, ili basi tuweze kurekebisha na tuone jinsi gani sheria yetu hii imepita ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hivyo kwa sababu uzoefu unaonesha sana kuwa tunaletewa miswada hapa, miswada mingi tunaletewa tunajaribu kuisoma, vile vile tunajaribu kutoa mapendekezo yetu katika mswada. Kama Katiba ya Zanzibar inavyotuelekeza kifungu cha 88.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu kwa ruhusa yako niweze kukipitia kifungu hichi haraka haraka ili kuona. Kifungu cha 88A ni kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo linahitajika kuwepo katika sheria hii. Sasa hii ni moja kati ya kazi za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi zilizozungumzwa ndani ya Katiba ya Serikali ya Zanzibar ambayo tunayo.

Lakini wenzetu imekuwa miswada inapitia katika hatua tatu muhimu. Hatua ya kwanza inapitia katika *Standing Committee* ambayo ya Makatibu Wakuu. Huko ndio tunasema Kamati ya Kitaalam. Hatuna shaka na hilo kwa sababu kuna madaktari ambao waliobobea, pana wasaidizi mpaka ma profesa wapo kule. Vile vile baada ya *stage* ya pili inakuja kwa Baraza la Mawaziri nao huko huko kuna madaktari waliobobea, lakini kuna maprofesa pale. Lakini hatua ya tatu mswada ule unatakiwa upitishwe ndani ya Baraza la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi tunao madaktari bingwa tu akina Dk. Makame Ali Ussi na wengine. Lakini *qualification* zetu sisi wengine tunatakiwa tujue kusoma na kuandika tena Kiswahili. Nina maana ya kuonesha hapo jinsi gani unapitia.

Mhe. Mwenyekiti, nimewahi kusema katika Baraza lako hili, nazi ina macho matatu lakini haioni. Nina maana gani. Tunatakiwa hata sisi tuweze kuona tuishauri serikali, vile vile katika miswada hii tunatunga sheria kupitia kifungu cha 88A.

Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea kufanya hivyo. Lakini katika kanuni ya 83(a) ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana ningeomba nikisome hichi. Kifungu cha 83(4) "Kwa madhumuni ya kupata maoni ya wananchi kuhusiana na mswada wa sheria unaotokana na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, kila Mjumbe wa Baraza atatakiwa kurudi kwa wananchi kukusanya maoni yao kabla ya kuanza majadiliano ya mswada huu."

Mhe. Mwenyekiti, tumetekeleza agizo la kanuni hii kurudi kwa wananchi ili tuweze kupata. Lakini wenzetu kila tukishauri, kila tukitoa mapendekezo yanakataliwa. Sasa bora mimi ningehisi hisia zangu kubwa tu, na hii naomba nitoe maoni kupitia kifungu cha 18 cha Katiba yetu. Maoni yangu naweza kutoa popote kwa uwazi ili mradi nisivunje sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana wewe umeweza kulinda Baraza lako tukufu, ili Baraza hili lisigeuzwe kama Idara ya Serikali, huu ni muhimili. Tunapotoa mapendekezo yetu lazima serikali iyaone kama mapendekezo haya ni sahihi au la. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri alivyowasilisha amewasilisha vizuri sana na hata Kamati imewasilisha vizuri sana. Ninaamini kwa sababu Waziri huyu aliyekuwepo tunazungumza kihadimu pamoja anaweza akayakubali mapendekezo yetu sana. Sio kama ile idara kwa muhimili huu kugeuzwa kama idara ya SMZ.

Lakini jengine tuangalie katika muhimili mwengine wa Mahkama panakuwa na Wazee wa Baraza pale wao hawatakiwi kujua hata a, b, c, d ya sheria, lakini wale wanachukuliwa maoni yao, iweje sisi leo tusiweze kutoa humu maoni yetu, maoni ya wananchi katika miswada hii

halafu yasichukuliwe. Hiyo itakuwa si haki. Lakini utengenezwe labda utaratibu tu waziri aje aweke na sisi basi tuhojiwe tu mmekubali kupitisha mswada huu, tumekubali. Hiyo labda italeta afya sana na itapendeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ilikuwa dibaji yangu tu kwa miswada mbali mbali ambayo inaletwa hapa. Sasa nataka niingie kwenye mswada huu na marekebisho ambayo nimeyafanya. Mhe. Mwenyekiti, nimefanya marekebisho katika ibara ya 5, naomba twende ibara ya 5 kwa wale waliyokuwa nayo. Mhe. Mwenyekiti, ibara ya 5 kifungu cha kwanza (g) mimi napendekeza kifutwe hichi. Sababu zangu kwa nini awepo Mkurugenzi wa *NIDA* hapa wa Mamlaka ya Vitambulisho, hakuna haja. Juzi tulikuwa tukimsikia Profesa Mnyaa akimjibu Mhe. Saada Mkuja Bungeni kumwambia tumekuwa kama tunataka labda upendeleo fulani hivi. Sisi hatuwezi kujipendekeza. Hii tunasema tu itolewe kwa sababu hili sio jambo la Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho nimesema tutoe hiyo lakini aongezwe mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Mufti kwa sababu tumeangalia humu talaka, ndoa, nikapendekeza tu kwa nia njema ili awepo mjumbe mmoja kutoka Afisi ya Mufti.

Jengine nimeenda kwenye kifungu cha 8 "Bodi itakuwa kikawaida inakutana mara moja baada ya miezi mitatu."

Sasa mimi hapa nikapendekeza kifungu hichi cha 8 kuongeza vifungu viwili. Vifungu viwili ambavyo nimeviongeza cha 5 kiwe akidi ya kikao iwe zaidi ya nusu ya wajumbe wote waliohudhuria katika kikao hicho. Isipungue akidi hiyo, ikipungua tutakuwa hatuna kikao. Lakini kifungu cha 6 nimesema bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye anaweza kuisaidia bodi kutokana na elimu na ujuzi wake pale anapohitajika. Sio tu lazima awe ndani ya bodi. Pengine tumeshindwa baadhi ya mambo tunamtafuta mtaalam ili aje pale tuweze kumshauri au atushauri atupe elimu ile. Uwezo huo bodi uwe nao.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 11(2) na hii naishauri kuongeza fani zifuatazo. Kifungu cha 11 kimeeleza hapa kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa mtendaji ikiwa ni Mzanzibari angalau awe na digrii ya kwanza au itakayolingana na hayo katika fani ya sheria, utawala, demografia au teknolojia ya habari. Mimi nikaongeza hapa ya ustawi wa jamii. Kwa sababu hii tunayokwenda nayo tunakwenda kwenye mamlaka ya watu. Lakini sasa hivi tumeanza kutoa digrii za ustawi wa jamii, nao hawa wasiachwe nyuma hapa ndipo mahala pake. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri hii aweze kui-*consider* tuweze kuingia nayo.

Lakini kifungu namba 12 Rais anaweza kuteuwa mtu kuwa Naibu Mkurugenzi. Sasa hii nimeona mimi kuna ukakasi tena wa kurudia maneno haya haya. Mtu ataweza kuteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji, ikiwa ana sifa kuwa Mkurugenzi Mtendaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 11(2). Kwa sababu tukirudia maneno yale yale tena nadhani itakuwa lugha kisheria hapa itakuwa inapingana. Lakini turudi tuseme tu kama maelezo yaliyotolewa kwenye kifungu cha 11(2).

Mhe. Mwenyekiti, tuelekee kwenye kifungu namba 21 ambacho kiko kwenye ukurasa wa 146. Kifungu hiki cha 21(7) inashauriwa kuongeza kifungu kidogo kipya kitakachotoa nafasi ya

kukata rufaa kwa mtu aliyekataliwa. Mtu ambaye hatoridhika na maamuzi kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa kumnyima kumpa cheti, atakuwa na haki ya kukata rufaa katika ngazi husika. Sasa ni lazima tuweke *room* mtu huyu hapa chini anaweza akakataliwa kwa sababu mbali mbali mkurugenzi atakazoziona zinafaa, lakini tumpe nafasi ya kuweza kukata rufaa, aidha kwa waziri au kwenye ngazi husika zitakazohusiana na mambo hayo. Lakini ikiwa hatutompa nafasi ya kuweza kukata rufaa basi hayo yatakuwa ni maonevu makubwa sana kwa wananchi. Kila mtu anahitaji kupata haki yake ya msingi katika nchi hii kama katiba yetu inavyotueleza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 23(2) kirekebishwe na kiwe kama ifuatavyo. Jina la mtoto, labda hapa tusome.

"Afisa Usajili kabla ya kuingiza taarifa yoyote kwenye *register* atahakikisha mtu aliyetoa taarifa chini ya kifungu kidogo (1), anatoa taarifa kama hizi.

Jina la mtoto, jinsia, tarehe ikiwa ana ulemavu, uzito, wakati wa kuzaliwa na pahala.

Sasa mimi nimerekebisha hapa, kwa sababu nimeona hakwenda *specific* jina la mtoto, jinsia,tarehe asiandike tarehe tu, lakini aandike tarehe ya kuzaliwa. Tunaweza tukamkuta mtu sio mwaminifu akatuandikia vitu ambavyo sivyo, ikiwa ni mlemavu basi ainishe aina ile ya ulemavu kama hapa itaweza kuingia. Mhe. Waziri yeye mwenyewe ataweza kuona anaweza akatoa *room* ya kuweza kufanya chochote, wakati hii simfungi, hii ni marekebisho ambayo mimi nilizingatia *convention* ile ya walemavu. Vile vile na uzito wakati wa kuzaliwa alikuwa na uzito gani, lakini alizaliwa pahala gani, hilo ni jambo la muhimu ambalo nimelizingatia sana.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki cha 40 nikiongeze kifungu kidogo kipya kisomeke kama ifuatavyo:

"Bila ya kuathiri kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, suala la talaka ambapo maamuzi yake yanatolewa katika Mahakama, Mkurugenzi Mtendaji atatakiwa kuridhia kwamba Mahakama imefikia mwisho katika kusikiliza dai linalohusiana na hilo".

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa sio kuridhia tu, anaweza Mkurugenzi akadanganywa kwa sababu talaka nyengine haziachwi kwa kadhi, talaka nyengine zinaweza zikaachwa tu hata nyumbani wakaja wakamdanganya, tumeshuhudia kwa sababu tunakaa kwenye jamii, watu wanaachana zaidi ya mara sita humu, lakini wanaendelea tu. Sasa wanaweza wakamdanganya kwa nia njema tu ya kutaka waendelee, lakini aridhie sasa na ahakikishe kwamba iko Mahakamani kesi hii imefika mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, hili litatupa afya na itapendeza sana tukiwa tutaifuatilia. Ndio maana ukiangalia kifungu hiki cha 36 kinazungumza hasa mambo ya talaka na ndoa, na ndio maana nikapendekeza ili kwanza kuwa mtu kutoka Ofisi ya Mufti aweze kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na marekebisho hayo tu. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri azingatie marekebisho yetu na aone basi iko haja na sisi kama tunaweza kuchangia na kuona. Lakini ikiwa hakuna haja anaweza vile vile kusema tukaweza kugeuza hili Baraza letu kama idara tu ya serikali na tukaweza ku-*table* hapo tukasema tu tumekubaliana nalo.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunivumilia na kwa kunipa muda angalau nikachangia, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Kabla sijampisha Mhe. Waziri nitampa nafasi Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu, mswada ambao umekuja kwa lengo la kuendeleza na kuimarisha harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kwa Wazanzibari wake.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kwanza kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza zile harakati ambazo zinawaelekeza Wazanzibari katika dhamira yao ya Mapinduzi ya mwaka 1964, katika hali ya kujipangia mambo yao na kuweza kwenda katika utaratibu kama vile dunia inavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu wa vitambulisho utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kuwa na takwimu sawa sawa ya mambo yote ambayo yanahitajika kwa wananchi wake. Kwa mfano, madawa, elimu bure, afya, maji safi na mambo mengine ambayo yanahitajika kwa jamii ya Wazanzibari kuweza kuyapata kwa urahisi na kwa uhakika kabisa kwamba haki hiyo inatoka moja kwa moja kwenda kwa Mzanzibari mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikurupuki tu kufanya mambo ambayo yako kinyume na katiba ya nchi au ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu yote haya ambayo yanapangwa na kuletwa hapa, basi ni katika mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2015/2020.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nisome ilani hii ya uchaguzi sura ya 193 ambayo inaeleza wazi wazi kwamba kuendeleza sera ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar, katika kipindi cha mwaka 2015/2020 Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuwa muumini wa kweli wa amani na utulivu na kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar kwa kuimarisha mafanikio yaliyokwisha kupatikana kuendeleza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuelekeza yafuatayo.

Kuendeleza jitihada za kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa amani, umoja na mshikamano, ili kujenga mazingira ya kuaminiana, kuvumiliana na kushirikiana katika masuala mbali mbali ya kijamii. Hiyo ni moja katika hizo faida ya hivyo vitambulisho.

Kuendeleza kupiga vita kudhibiti vitendo vya ubaguzi vilivyojitokeza katika sehemu za utoaji wa huduma za kiuchumi, kisiasa na kijamii miongoni mwa wananchi wa Zanzibar.

Kuimarisha mifumo ya taasisi za utaratibu na kushughulikia malalamiko na kero za wananchi kwa wakati, haki na uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, hizo ni miongoni mwa faida za hivyo vitambulisho. Kwa sababu utakapokuwa na kitambulisho chako, basi ni lazima utakitumia katika mazingira ya kutafuta haki, uadilifu wako kwamba wewe ni nani, uko wapi na unataka nini.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu katika dunia vitambulisho wanavitumia hata kwenda dukani akaonesha kitambulisho chake na hatimaye akaangaliwa namba yake ikatiwa kwenye mtandao, ikaangaliwa *account number* pale pale na kile anachokitaka akapewa halafu baadae watu wakafuatilia malipo yake katika taasisi za kibenki. Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina dhamira ya kufika huko, ili kuwafanya wananchi wa Zanzibar na wao wasikie na wafaidike na Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 230 cha ilani ya uchaguzi kinasema hivi;

Kifungu cha 230

> "Kusimamia utekelezaji wa ilani wajibu wa CCM kutoa ahadi kwa wananchi kupitia ilani ya uchaguzi na kuzikabidhi serikali zake zote mbili utekelezaji, bali pia ni wajibu mkubwa wa kufuatilia utekelezaji wa ahidi hizo. Hivyo ni muhimu kwa Chama cha Mapinduzi kuzingatia utaratibu uliojitokeza wa namna ya kusimamia na kukagua utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni katika jumla ya watu kuunganishwa kijamii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia sahihi juu ya mswada huu, ili kuwapeleka wananchi katika mazingira ya kuunganisha shughuli zao kijamii. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo sasa ndiyo inayotekelezwa na serikali zote mbili, hii inaendelea kusema tukirejea uzoefu wa miaka ya nyuma jukumu hili la CCM, kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi katika ngazi mbali mbali, kuanzia vijijini hadi taifa kulikojitokeza kwa kiwango cha wastani hasa katika ngazi za vijiji, kata na majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, majimbo haya wasimamiaji wake ni Wawakilishi na Wabunge, ni lazima wahakikishe kwamba kinachotendeka basi kinawafikia wananchi katika mazingira ya kuendelezwa kisiasa, kijamii na kiitikadi katika mazingira ya kuifanyia kazi ilani hii ili wananchi waweze kuona faida ya uchaguzi, faida ya ilani yao na faida ya uongozi wao wa majimbo. Tunaweza tukakosoa vifungu mbali mbali, lakini kama tutashindwa kuvisimamia vifungu hivyo, kazi yetu itakuwa haina maana kwa wananchi. Lakini ni vyema tukiwa tayari kwamba tunakosoa vifungu, lakini pia tunasimamia kitabu hiki ambacho kinaongoza uchaguzi uliopita na kinaelekeza maendeleo yaliyopo Zanzibar, basi ni lazima tuhakikishe sisi kama wawakilishi tunakilinda na kukitetea Chama cha Mapinduzi kwa kupitia ilani yake hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inapiga hatua za maendeleo kama vile inavyopiga hatua za maendeleo katika nchi nyengine za dunia. Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika nchi za dunia kama vile Canada, Marekani na nchi nyengine duniani vitambulisho hakika ni kitu muhimu sana. Sasa hakuna sababu ya kuwa watu 1,500,000 wa Zanzibar kushindwa kuweza kutumia utaratibu huu wa vitambulisho. Pindi tukijipanga kweli kweli na tukakubali wenyewe kuhakikisha kwamba tunataka kubadilika, basi mimi naamini tutaweza kutatua matatizo yetu kupitia vitambulisho. Mtu atakwenda hospitali na kitambulisho huduma ataipata kama Mzanzibari, mtu atakwenda

benki na kitambulisho huduma ataipata kama Mzanzibari, mtu atasafiri huduma ataipata kama Mzanzibari, kitambulisho ni kitu muhimu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja za jamii sisi kama wawakilishi wa majimbo ni lazima tukubali kuwa watumishi wa wananchi na tuwe tayari kuhakikisha kwamba yale yote yanayotendeka katika majimbo tunakuwa tayari kuya-*report* katika serikali. Sio watu wengi walio na uwezo wa kufahamu, ni lazima tufahamishane mmoja baada ya mwengine katika mazingira kama haya. Wengi wao wanavyofikiria katika hali halisi labda sisi tulio katika hali hii, tukikitetea Chama cha Mapinduzi tunaonekana kama labda vile tumekwisha kisiasa, hapana. Sisi tunatetea ilani ya uchaguzi. Ilani ya uchaguzi ndio iliyotufikisha hapa sisi na katiba hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeeleza wazi wazi, kwamba serikali itakayoundwa itakuwa ni ya umoja wa kitaifa. Sasa ukiingia humu wewe huna haja ya kusema mimi nina chama fulani, ukiingia humu wewe ni mtu wa SMZ ilani yako ni ya Chama cha Mapinduzi, kama wewe CCM huwezi kuitetea hii, basi mimi nitaitetea hii. Maana wako CCM hawawezi kuitetea hii. Lakini mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Mwenyekiti, kwamba mimi nitaitetea na nitailinda na nitatekeleza yote yaliyomo kwenye ilani hii. Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu

UTARATIBU

Mhe. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Kanuni ya 45, kuhusu maelezo binafsi ya mjumbe. Mhe. Mwenyekiti, nilikueleza ukaniambia niinuke tena baadae, nimeinuka.

> "Mjumbe yeyote anaweza kwa kibali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambao umewekwa na kanuni ya 27".

Mhe. Mwenyekiti, nina jambo muhimu sana kidogo nataka nilitolee maelezo ili angalau tuweke vitu sawa katika maslahi ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif ulitoa *concern* yako hiyo na nilikuambia katika hiyo kanuni ya 45 imesema "mjumbe yeyote anaweza kwa kibali cha Spika". Kibali cha Spika, ndio hiki kiti hapa, ndio nikakuambia mpaka nikupe hicho kibali. Lakini kwa leo na sasa hivi nikakuambia tuliachie hilo kwanza tuendelee na taratibu tulizopanga, najua una haki hiyo kwa mujibu wa kanuni ya 27, ila mpaka nikupe hicho kibali. Nikasema sasa hivi wacha tuendelee halafu utakuja kupata ufafanuzi wa suala lako, hata kama sio sasa hivi lakini hilo suala lako umelileta na nimelipokea tutalitolea ufafanuzi, nilikujibu hivyo mheshimiwa.

Mhe. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri unaogopa mtu akiinuka na hoja, kwa sababu hujanisikiliza hata nataka kuongea nini unaniambia utatoa

ufafanuzi, ufafanuzi huo utatoka wapi wakati hujui *concern* yangu. Mimi naomba suala hili la nchi ni suala ambalo linatukanwa serikali, kama umeamua kuachilia suala lako mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif nakuomba ukae tuendelee. Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Naibu Waziri ajiandae.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia uwezo na nguvu ya kuweza kuchangia mswada huu muhimu uliopo mbele yetu ulioletwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Welezi, wana mapinduzi wa nchi hii wakulima na wakwezi. Mimi nachukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuleta miswada mbali mbali inayodhamiria kuyalinda kuyaenzi na kuyatetea Mapinduzi ya Zanzibar. Sio siri Mapinduzi ya Zanzibar ndio yaliyotufikiha hapa kwa hivyo si vyema kumuona mtu yoyote yule au taasisi yoyote au kikundi chochote cha watu wanayachezea au wanayakebehi Mapinduzi haya.

Mhe. Mwenyekiti, mengi tumeyasikia kwamba kunako masuala mazima ya hivi vizazi, vifo *registration* na kila kitu kadi za Mzanzibari kila kitu kulikuwa kunachezewa. Lakini leo Mahatma Gandhi kasema *realization as a human potential*, naishukuru sana Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeleta Mswada huu wa Kimapinduzi, ulioletwa na mtoto wa wakwezi na wakulima Mhe. Haji Omar Kheri, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa kuona kwamba Mapinduzi matukufu ya Januari, 1964 kwa maslahi ya wakwezi na wakulima yalikuwa yanachezewa. Kwa sababu wasiostahiki kupata vitambulisho walikuwa wanapata, wasiostahiki kupata vyeti vya kuzaliwa walikuwa wanapata kwa sababu tu ya tofauti za msingi, lakini yote ni kuyakebehi na kuyakashifu Mapinduzi matukufu ya Januari, 1964.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba sana nichukue fursa hii kumshukuru sana leo Mhe. Waziri Said Soud kwa kuyasifu na kuyapongeza na kuyatambua kama sikosei Mapinduzi matukufu ya Januari 1964, lakini kadhalika Mhe. Said Soud leo ingawaje anatoka nje ningependa asikie kwamba ametambua na kutamka hadharani kwamba Chama cha Mapinduzi na ilani yake na Katiba yake ndio chama dume nchi hii na dunia nzima. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bila ya siri nataka kumwambia leo kwamba CCM kweli ndio chama chenye ilani madhubuti kuliko ilani yake na leo ametamka mwenyewe, lakini pia nashangaa najiuliza yeye hana ilani kwani Chama chake lakini ndio lazima Chama cha Mapinduzi ni chama dume na kimebakia CCM ndio nambari *one* na *ANC* ya Afrika ya Kusini. Kwa hivyo namshukuru sana Mhe. Said Soud Said kama ametambua ilani ya Chama cha Mapinduzi ndio ilani bora, ilani itakayoweza kuleta maendeleo na kulinda maslahi ya wakwezi na wakulima wana Mapinduzi wa nchi hii ingawaje nafikiri sijui yeye hana ilani. Lakini pia tunamkaribisha Chama cha Mapinduzi ni chama madhubuti kama ameamua atangaze basi kwamba kuanzia leo au kesho yeye amekwenda CCM tutampokea wengi tumewapokea. Chama cha Mapinduzi ni chama rahimu tutampokea Mhe. Said Soud ni mwenzetu mimi nampenda sana hasa kwa vile anayatambua Mapinduzi matukufu ya Januari 1964.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba kwenda kwenye Mswada sehemu ya tatu utawala na wakala, kuna bodi ya ushauri unaposema bodi ya ushauri ni kwamba ushauri ni maana yake ukitaka unaufuata hukutaka huufati ndio maana ya ushauri. Sasa mimi ningependelea hii ikawa bodi ya usimamizi isiwe bodi ya ushauri kwa sababu ushauri unaweza kukukubalika, unaweza ukapokelewa au usipokelewa iwe Bodi ya Usimamizi hilo moja.

Mbili, namba kumi ukisoma kwamba Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wengine wa bodi watalipwa maposho na mafao kama Waziri atashauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha atakavyoainisha muda hadi muda, sasa ninajiuliza kwa nini bodi hii lazima maposho yake mafao kama Waziri hebu nahitaji ufafanuzi kwa nini iwe kama Waziri, bodi Zanzibar ziko nyingi zimetungwa nyingi, zimeundwa nyingi lakini kwa nini bodi hii tu iwe mafao yake kama Waziri na kwa kushauriana na Waziri wa fedha, kwa nini bodi hii isifuate maposho kwa mujibu wa kanuni za utumishi kama zilivyo nyengine kwa nini bodi hii. Kwa hivyo naomba ufafanuzi wa kina kuhusu bodi kama si hivyo kipengele hichi mimi ningeomba kiondoke kwa sababu hakina kazi hapa, kwa nini bodi hii lazima tunapata wasiwasi, kwa nini bodi hii iwe *so special way not* bodi nyengine ambazo Serikali ya Mapinduzi zimeitunga na zina majukumu sawa sawa na zinafanya kazi ya kimapinduzi kwa nini bodi hii, *why*.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika ukurasa wa 145 kifungu 15(1) bila ya kuathiri kifungu chochote cha sheria hii Mkurugenzi mtendaji anaweza kukasimu kwa maandishi baadhi ya kazi za ofisa yoyote wa wakala. Mhe. Mwenyekiti hii ni hatari Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukasimu kwa Afisi yoyote wa wakala hii ni hatari, tusimpe nguvu hizi za kukasimu Mkurugenzi Mtendaji. Tumpe nguvu hizi mtu mwengine labda Katibu Mkuu, Waziri za kukasimu kwa sababu Mkurugenzi Mtendaji ni mtu mdogo sana anaweza kenyr hii wakala rafiki yake, rafiki yake huyo akawa labda kwa mfumo mmoja au mwengine haendani na misingi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi ile kaipata kwa bahati mbaya. Bila ya kujua siku nyengine Mkurugenzi mtendaji akamkasimu madaraka nini kinachoweza kujitokeza.

Kinachoweza kujitokeza ndio kile tulichokikataa leo tutakitungia sheria wakaja wakapata watu haki za vitambulisho, wakaja wakapata watu vyeti vya kuzaliwa na mambo mbali mbali wasiostahiki kama yaliyokuweko zamani itakuwa hatujajenga itakuwa tupo pale pale. Kwa hivyo naomba kipengele hichi kisimpe nguvu Mkurugenzi Mtendaji, Mkuruganzi Mtendaji ni mtu mdogo sana kuwa na nguvu ya kumkasimu ofisa, siku nyengine samahani anaweza kuweka *girl friend* wake kumbe hizbu akamkasimu ikawa anaturudisha kule kule, haya mambo yapo na yameshatokezea. Kwa hivyo naomba sana asipewe jambo hili nguvu hii Mkurugenzi Mtendaji tumeona mambo haya katika Zanzibar, Tanzania na nchi nyengine, kumkasimu mtu kitu ambaye hastahiki baadae anafanya uasi na mambo yanaharibika. Kwa hivyo naomba sana jambo hili asipewe Mkurugenzi Mtendaji bali apewe Waziri au mtu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo twende katika 26 Mkurugenzi Mtendaji au mtu aliyekasimiwa madaraka baada ya kupokea taarifa ya kizazi na kuridhika na taarifa hizo atatoa cheti cha kuzaliwa kutokana na kumbukumbu zilizopo katika ofisi. Mhe. Mwenyekiti, umeona hapa ndio tatizo sasa Mkurugenzi mtendaji akishaletewa taarifa kumbe mtu yule hakuzaliwa hapa zimeundwa undwa tu na kamkasimu madaraka Ofisa, Ofisa siku nyengine ndio vile wana *relation or what ever* kapewa vitu vile kwa mahaba yake katoa cheti kile, kumbe mtu yule aliyepewa hastahiki. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hapa kukasimu madaraka

asipewe mamlaka haya Mkurugenzi Mtendaji kwa sababu hili ni jambo kubwa la nchi dunia nzima mambo ya vitambulisho, dunia nzima mambo ya vyeti vya kuzaliwa kwanza vinashughulikiwa na *Security Agency* kwa sababu ni kitu *sensitive* hashughulikii raia. Sasa sisi tunakwenda kuwapa watu tu wakashughulikie mambo haya Mhe. Mwenyekiti, tutakingia katika matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia katiba yetu ya Zanzibar ukienda katika 50(3) kwanza naomba nisome katiba halafu nitasoma 50(3) na ningeomba watu wote wasikilize hapa.

Mhe. Mwenyekiti, katiba ya Zanzibar 91 inasema "Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa umoja wa kitaifa na utendaji wake kazi utafanywa katika utaratibu utakaoridhishwa kuendelezwa na umoja chini ya lengo kufikia kidemokrasia".

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukienda 42(2) inasema hivi. "Rais ndani ya kipindi cha siku 14 mara baada ya kuteuliwa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais, Rais kwa kushauriana na Makamu wote wawili Rais atateua Mawaziri kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo, kwa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ipo hapa ukiangalia hii 42(2) kwamba imeruhusu mfumo wa vyama vingi, mfumo wa vyama vingi upi? Ambao nchi yetu ya Kimapinduzi mtu yoyote asiyeyatambua Mapinduzi matukufu ya Januari 1964 bibi yangu mimi aliniambia huyo Hizbu ndivyo alivyonambia bibi yangu, mtu yoyote nini hizbu mtu yoyote asiyeyatambua Mapinduzi matukufu ya Januari 1964 bibi yangu mimi kanambia huyo hizbu yoyote yule. Sasa hapa ndani ya nchi hii ukiacha labda kama sikosei Mhe. Said Soud yeye anayatambua Mapinduzi vyama vyengine haviyatambui Mapinduzi na mengi yalitokezea haya na katiba imeruhusu.

Sasa twende katika 50(3) inasema. "Mtu mbali na waziri Idara au Wakala wa Serikali anaweza kupata matumizi ya taarifa ndani ya *register* kulingana na kanuni zitakazotolewa na Waziri".

Mhe. Mwenyekiti, katiba yetu 42(2) imeruhusu mfumo wa vyama vingi muundo wa Mawaziri leo Alhamdullialahi Waziri wa zamani wa Wizara hii Mhe. Haji Omar Kheri mtoto wa Mapinduzi, Mkulima, Mvuvi yote yake. Lakini tunao mfumo umo ndani ya katiba hatujaufuta bado ingawaje tunataka tukaufute, lakini anaweza kuja Rais mwengine akateua Mawaziri kumpa Wizara hii akawa Hizbu hayatambui Mapinduzi. Sasa leo umempa kutunga kanuni ambazo mtu yoyote yule anaweza kupata taarifa *of course* ndio Waziri kwa hivyo ana dhamana ya kutunga kanuni, zile kanuni yule Waziri Hizbu zile kanuni zika-*favor* Hizbu itakuwa tupo pale pale Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo naomba kipengele hichi kwanza kisiwe mtu yoyote iwe *special agencies* kwa sababu kupata taarifa za mtu ni kitu hatari, leo ukisema mtu yoyote kwa kizungu hapa imewekwa *very clear imewekwa a person or then a ministry a person* yaani mtu yoyote yule. Jamani basi mtu yoyote tu akapate tu taarifa za mtu kutokana na *register,* haiwezekani. Nchi za wenzetu kama Uingereza na Marekani mtu kupata taarifa hizi *only security agencies* na taasisi nyengine *special* sio mtu yoyote.

Kwa hivyo, naomba sana kupata taarifa za mtu pasipo *datas* ni vitu muhimu leo kuna wizi duniani mtu akipata tarehe yako ya kuzaliwa, akipata jina lako, akipata *address* yako anaweza akakuibia kunako benki yako pesa zote. Leo kuna mtu akipata *data* zako kama hizo anaweza kucheza *data* zako akakufanya mambo anavyotaka. Sasa kwa hivyo hatuwezi kutunga sheria tukasema mtu yoyote itakuwa hiyo sheria haijakamilika hatuwezi kusema hivyo. Tuseme mtu maalum au taasisi maalum tusimuachie mtu, huyo mtu akitaka kuomba *data* za mtu apitie kwenye taasisi ambayo taasisi hiyo iwe maalum akaeleze kwamba mimi nataka kupata *data* za Mhe. Abdalla Ali Kombo, akapeleke sababu mpaka taasisi ile iridhike imkubalie taasisi ndio iandike kunako taasisi hii kwamba mtu huyu fulani fulani kwa sababu fulani anataka kupata *data* za Mhe. Abdalla Ali Kombo, atapewa lakini isiwe mtu yoyote. Hivyo mimi leo nataka kupata *data* za Abdalla Ali Kombo niandike nipewe haiwezekani hiyo sio sheria hasa ukizingatia hii nchi ya kimapinduzi, nchi ya kimapinduzi mambo yake hayawi wazi tu yanakuwa yako *close* sawa sawa na nchi zote za wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili mimi naomba sana hapa libadilike leo tunae Waziri Haji Omar Kheri Mwenyezi Mungu amuweke lakini katiba yetu inaruhusu Hizbu asiyeyatambua Mapinduzi awe Waziri, je tukipata huyo Hizbu si atakuja kutukomoa tena vitambulisho vitatoka kama njugu

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo machache naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kuchukua fursa hii kwanza kabisa na mimi kukupongeza sana kwa namna ambavyo umendelea kusimamia kuliendesha Baraza lako tukufu, kwa ruhusa yako na mimi napenda kuchukua fursa hii kuchangia Mswada huu ambao upo mbele yetu ambao tunaendelea kuuchangia katika muda huu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi katika mchango wangu naomba nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja au mambo ambayo yamejitokeza kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, awali ya yote kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Kamati ya Katiba Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa namna ambavyo imeweza kutoa marekebisho mbali mbali katika Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo moja kwa moja nianze na Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa kutoa ufafanuzi mdogo au kwa kueleza machache kwa yale ambayo ameyagusia. Waheshimiwa Wajumbe akiwemo Mhe. Rashid Makame Shamsi ametoa ushauri juu ya kutoa elimu juu ya mabadiliko ya Mswada huu ambao sasa hivi tunatarajia kuupitisha Mwenyezi Mungu akipenda, kwa hivyo suala la ushauri katika suala la elimu ni jambo la lazima na ni vyema kabisa kwamba ushauri wake tuuchukue na tutaufanyia kazi kuona kwamba wananchi wa Zanzibar tunawapa elimu juu ya namna bora ya kuweza kukabiliana na mabadiliko haya ambayo tumeyapokea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niende moja kwa moja nianze na Mhe. Nadir Abdul-latif yeye alitoa ushauri katika kifugu cha 53 kuhusu Wakuu wa Wilaya na Masheha kuhusu kutoa barua kwa watu wanaostahiki na kushauri kwamba wawe makini, naomba nitoe ufafanuzi kwamba ushauri huo tumeupokea na suala la Wakuu wa Wilaya na Masheha wakiwa kama ni wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi kwa miongozo mbali mbali ya kisheria na tunaamini kwamba wako makini, na tunaendelea kuhakikisha kuwa wanaendeleza jambo hilo. Kwamba kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na sio vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kifungu cha 56 Mheshimiwa Nadir Abdul-latif pia alisema kwamba sheria zinazofutwa kwa mfano sheria No. 7 ya mwaka 2005 imezungumzia usajili katika Mswada huu kwamba hakimo. Kwa hivyo naomba niseme tu kwamba kifungu hiki hakikuingizwa katika Mswada huu kwa sababu usajili ni suala la lazima kwa aliyetimiza masharti ya kisheria na sheria inayofutwa iliingizwa kifungu hicho ikiwa Serikali ndio kwanza inaanza usajili wa utoaji wa kadi za utambulisho, na iliweka kifungu chenye sharti la usajili mpaka utangazwe katika gazeti rasmi ndio maana kiliwekwa kifungu kwa watu wanaorejea nchini kuweza kusajiliwa na kupatiwa kitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Nadir Abdul-latif aliweza kushauri kuhusu bodi ya ushauri Mkurugenzi wa NIDA atolewe na awe ni mualikwa tu, vile vile Mhe. Mohammed Said Dimwa na waheshimiwa wengine pia waliweza kutoa *concern* zao juu ya kuweko kwa mjumbe huyu lakini naomba nitoe ufafanuzi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuingizwa kwa Mjumbe au Mkurugenzi Mkuu wa NIDA ni kutokana na uzoefu na uwiano wa kazi za usajili na pia katika *Staring Committee* ya NIDA hata sisi katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ni wajumbe pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hivyo tukaona na sisi jambo hili pia haliwezi kuathiri katika yale ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Nadir Abdul-latif alishauri alisema kwamba sheria haijaeleza kuhusu usajili wa mtoto wa nje ya ndoa, naomba nitoe ufafanuzi kama ifuatavyo. Watoto wote wanaozaliwa Zanzibar wanasajiliwa na utaratibu wa usajili wa watoto hao utawekwa katika kanuni.

Vile vile kuhusu usaili wa mtoto haujaelezwa katika Mswada huu vile vile ufafanuzi ni kwamba suala la usajili wa mtoto utaratibu wake umeelezwa katika sheria ya mtoto No.7 ya mwaka 2011.

Mhe. Simai Mohammed Said yeye alieleza kwamba Waziri kutangaza sheria katika gazeti rasmi la Serikali haijaainishwa muda wa kuitangaza naomba nitoe ufafanuzi mdogo kwamba ni utaratibu wa kawaida wa utungaji wa sheria na sababu ni kwamba waziri anapata muda wa kutunga kanuni kwa utekelezaji wa sheria hiyo.

Vile vile Mhe. Simai alitaka kujua kuhusu uteuzi wa wajumbe wa bodi wawili waziri azingatie lini katika ufafanuzi wa hilo katika kifungu hicho kinacho mamlaka ya uteuzi ya wajumbe wawili kumeainishwa jinsia, kada na ujuzi.

Kuhusu sifa za maofisa wa usajili wa wilaya kiwango cha *degree* na vipi kuhusu wafanyakazi wadhoefu watapelekwa wapi, ufafanusi ni kwamba kwa maofisa usajili wa Wilaya wa kiwango cha *degree* hakiepukiki ukizingatia katika uteuzi wa wafanyakazi waliopo bado wataendelea kuwepo kwa mujibu wa sheria na utumishi watapangiwa maeneo ya kazi kulingana na elimu zao.

Kuhusu siku kumi na nne za usajili wa ndoa ziwekwe miezi mitatu ushauri huu Mhe. Mwakilishi tumeuzingatia na kwa sasa ni kwamba hatukufikia miezi mitatu bali tumesema kwamba ushauri huu tunaongeza hadi kufikia siku 30 kutokana na umuhimu wake na muda wa kutoa vyeti uainishwe. Suala la usajili la utoaji wa vyeti ni endelevu na haliwekewi muda muhusika aliyesajiliwa kupatiwa cheti chake pale ambapo kwa kweli utaratibu au na mambo mengine yamekamilika.

Mheshimiwa kifungu cha 48 Mhe. Simai alitaka kujua kwamba Waziri kuwasilisha taarifa ya fedha ndani ya miezi mitatu kifungu hiki hakitekelezi naomba nisema tu kwamba uwasilishaji wa taarifa za fedha ni utaratibu ulioanishwa katika sheria namba 7 ya mwaka 2016 ya Usimamizi wa Fedha.

Katika kifungu cha 51 Mhe. Simai pia alitaka kujua kwamba alishauri ada iangaliwe hali halisi ya maisha ya wananchi naomba nitowe ufafanuzi kwamba ada zinazotozwa ni za kawaida na utaratibu wake ni lazima ziidhinishwe na Serikali ambayo huzingatia maisha ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna hoja ya Mhe. Ali Sulieman Ali (Shihata) kifungu 27 ni kwamba aina ya watu wanaopaswa kusajiliwa kwa mujibu wa sheria hii naomba nitoe ufafanuzi kwamba watu ambao wanapaswa kusajiliwa ni Mzanzibari Mkaazi n asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi aliyeishi nchini ya masharti ya Sheria ya Uhamiaji, vile vile na asiyekuwa Mzanzibari ambaye halazimiki na masharti ya Sheria ya Uhamiaji.

Katika kifungu cha 28 vile vile Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kutokuwa na kadi za aina ngapi kwa hiyo naomba niseme katika kadi hizi kwamba kutakuwa na kadi za aina mbili ambayo moja itakuwa ni Mzanzibari Mkaazi na asiyekuwa Mzanzibar Mkaazi. Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) vile vile naye pia naomba nigusiye alitaka kujua suala la rufaa, naomba nitoe kwamba suala la rufaa ni suala la kisheria kwa ujumla Mahakama Kuu imepewa mamlaka ya kusikiliza rufaa, kufanya mapitio ya taratibu za kisheria, taratibu zilikiukwa usajili ni lazima kwa aliyetimiza masharti ya kisheria akinyimwa kwa hiyo kwa mujibu wa sheria aliyemnyima sheria itachukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi huo kwamba kuona kwamba waheshimiwa wajumbe ni imani yangu kwamba kutokana na hali halisi ya mswada huu na jinsi ambavyo umetayarishwa ulizingatia mambo mengi na moja kubwa zaidi ni kuona zile hofu ambazo zipo na zile tuhuma ambazo zimekuwa zikizungumzwa mara kwa mara kuhusiana na labda kuchezewa chezewa huu utaratibu au hivi vitambulisho kuwepo na tuhuma kuwepo kwa vyeti feki, basi naomba tu niseme likifanikiwa hili hayo mengine yote ambayo yamekuwa yakiwatia hofu waheshimiwa wajumbe waamini kwamba yamefanya kwa nia njema na tutaweza kusaidia katika kuona hauchezewi na wala hakuna hujuma kama hizo ambazo zimekuwa zikiripotiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mengi na mimi naomba nichukuwe fursa hii kwamba kusema kwamba naunga mkono mswada huu asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais sasa naomba nimwite Mhe. Waziri Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa aje kutoa ufafanuzi.

Mhe. Waziri Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ambazo zimetolewa na wajumbe mbali mbali wa Baraza lako Tukufu kuhusu kuchangia Mswada wa Sheria wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kwa kusema na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia najua kwamba mawazo yao maoni yao kutokana na uwelewa wao wameridhika na mswaada huu, kwa hiyo nataka niwashukuru na kuwapongeza sana.

Lakini wale walipata nafasi ya kuchangia kwa kusema wote walikuwa na nia ya kuishauri Serikali juu ya yale maeneo ambayo wameona yawe ni sehemu ya mswada.Mimi nataka niwahakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea ile ya mwaka 1964 ya awamu ya kwanza mpaka hii sasa ya awamu ya saba, haitakuwa na lengo kabisa la kuwaona wananchi kuishauri Serikali yao si jambo la maana. Kwa hiyo, hata siku moja Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitakiona chombo hiki kama ni Idara ya kawaida bali chombo hiki ni muhimili wa dola, muhimili wa nchi kwa hiyo daima Serikali itaendelea kupokea ushauri, maoni na mapendekezo ambayo yanatolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waloletwa na Wananchi ndani ya chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Isipokuwa katika kutoa maoni tukubaliane kwamba yapo maoni yanaweza yakakubalika na yapo maoni si kwamba hayana maana lakini yatakuwa pengine kwa madhumuni ya sheria iliyokusudiwa pengine yanaweza yasiwe yana *fit* hapa na yanaweza yaka-*fit* katika maeneo mengine. Kwa hiyo nitowe hofu waheshimiwa wajumbe na kama alivyosema ndugu yangu pale Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwamba mswada huu ni wa kimapinduzi Dkt. Shein aloniagiza kuwasilisha mswada huu ni mwana mapinduzi na mimi ni mwana mapinduzi nilolelewa na mapinduzi wanojua historia wanaweza wakajua nimelelewa na nani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nataka sasa niwatambuwe rasmi wajumbe ambao wamechangia mswada huu.

Wajumbe wote walikuwa saba nikianza na:

1. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ambaye amesoma maoni ya kamati Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chaani lakini pia alipata nafasi ya kutoa maoni yake kwa niaba ya wananchi wa Chaani.
2. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)
3. Mhe. Ali Suleiman Ali

4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa)
6. Mhe. Said Soud Said
7. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
8. Mhe. Shamata Shaame Khamis

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nichukuwe fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Katiba, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ kwa maoni na marekebisho mengi waheshimiwa wajumbe kama tunakuwa tumeyasoma haya marekebisho ambayo yamefanywa na kamati nilipokuwa namsikilisha Mhe. Rashid Makame Shamsi zile *error* na zile na nyingi kama tutayapitia haya marekebisho ya Kamati ya Katiba, Utawala Bora na Idara Maalum mengi yamezingatiwa.

Kwa hakika kamati hii imetupa ushauri mwingi na kuufanya mswada huu uwe bora zaidi nawashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Katiba, Utawala Bora na Idara Maalum na kwa leo napenda nimpongeze sana ndugu yangu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa kusoma kwa umakini kabisa kwa niaba ya kamati hii.

Baada ya kwisha kusema hayo, kwa hiyo nataka nikubaliane kwamba ule ushauri wao daima tutaendelea kuupokea na yale maoni yao yote ambayo wameyatoa kwenye kamati tumeyafanyia kazi na yatakuwa ni sehemu ya mswada huu, pale ambapo tutaupitisha vifungu kwa vifungu basi utasomwa na marekebisho yake.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nadir alipopata nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya wananchi wa Chaani mengine ameyasema Mhe. Naibu Waziri wangu alipokuwa akichangia alipopata nafasi ya kutowa ufafanuzi, kubwa zaidi jambo ambalo limezungumzwa na baadhi ya wajumbe akiwemo Mhe. Nadir na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) ni lile la Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA* kuwepo kwenye Bodi ya Ushauri.

Kwanza, nataka niwatoe khofu ni kweli taasisi hii ya Muungano na taasisi ya *NIDA* ni ya Muungano, lakini kwa sababu ya *experience* na ku *share idea* na kupata uzoefu kwa mawasiliano ya karibu ndio maana Serikali sisi tulimuona tumeweke huyu Mkuregenzi Mkuu kuwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri kwa Waziri kwa nini, kwa sababu kama tutaisoma ile sheria ya Mzanzibari inasema. Ili uwe Mzanzibari sharti la kwanza uwe Mtanzania na taasisi ambayo inatoa utambulisho wa Mtanzania ni *NIDA*.

Kwa hiyo, nawaomba sana waheshimiwa wajumbe ni kweli hii taasisi siyo ya muungano lakini kwa sababu ya ukaribu na mahusiano ya kazi zetu ni vizuri tukawa na mjumbe kutoka *NIDA*, ili tukawa tuna *share information* na taarifa juu ya nani anapaswa kusajiliwa kuwa Mzanzibari Mkaazi na mambo mengine ambayo tutakuwa tuna *share,* watakuwa wana *share* ndani ya Bodi kwa madhumuni ya kuweza kupata *information* na taarifa, pale ambapo tutazihitaji kuzipata. Tukumbuke kwamba hii bodi ni ya ushauri kwa waziri hii bodi ni bodi ya ushauri kwa waziri anayehusika na masuala ya usajili wa matukio ya kijamii. Kwa hiyo, kwa heshima kubwa sana na kwa nidhamu kubwa sana nawaomba wajumbe waliotoa hoja hii wanikubalie kwamba Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA* awe mjumbe wa bodi kwa sababu hizo ambazo nilizozisema hapo awali.

Mhe. Nadir nadhani utanikubaluia hili kwa madhumuni hayo kwamba tunakusaidia kusajili Wanzanzibari Wakaazi na ili uwe Mzanzibari Mkaazi lazima uwe Mtanzania, kwa hiyo kumuweka Kamishna Uhamiaji na Mkurugenzi wa *NIDA* ni kwa madhumini yale yale ni kupata taarifa na ku-*share information* juu ya wake watu ambao tunataka kuwasajili.

Mhe. Nadir pia alituhimiza ambapo Mhe. Naibu Waziri ameshasema kuhusu suala la umakini na hofu ile ya Masheha na Wakuu wa Wilaya kufanya kazi kinyume na maadili. Kwa kweli ushauri wako ni ushauri mwema na tunakubaliana nao na sisi tutajitahidi kusimamia hilo uadilifu kwa Masheha na Wakuu wa Wilaya na ndio maana tumeamua tuanzishe mfumo mpya kwa ajili ya kusimamia hilo, kwa hiyo Mhe. Nadir nakubaliana na wewe tutajitahidi sana.

Aina ya vyeti nafikiri au aina ya vitambulishi nadhani Mhe. Naibu Waziri amelisemea hili jambo vizuri sana katika ufafanuzi wake ni imani yangu kwangu utakuwa umefarijika na ufafanuzi ule ambao ambao ameutoa mheshimiwa na maeneo mengine ambayo umeyasema ya *adoption* kama alivyosema Naibu Waziri amesema vizuri kwamba ile sheria namba 7 ya mtoto imeelezea namna ya mtoto atakavyokuwa huko.

Lakini mtoto wa nje ya ndoa vipi atasajiwa hili nawaomba sana wajumbe wa Baraza la Wawakilishji wakubali niliweka katika kanuni nitaweka utaratibu mzuri bila kuvunja masharti yalipo kwenye sheria hii kwenye kanuni nitakazozitunga ili kuweka utaratibu mzuri wa huyo mtoto ya nje ya ndoa namna atakavyosajiliwa. Kwasababu kizazi lazima kisajiliwe kinasajiliwaje nani atakuwa na ushahidi upi sasa huo utaratibu naomba tuuweke katika kanuni.

Ulizungumzia Mhe. suala la sababu ya vifo mimi nadhani mambo menigine haya tuwache kwenye zile taasisi ambazo zimepewa majukumu kwa mfano masuala ya kifo kama kimetokea hospitali basi anayetakiwa kuelezea kifo kile kimesababishwa na nini ni daktari. Kwa hiyo ni jambo zuri lakini mimi nadhani tungeacha kwenye taasisi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria zikatekeleza wajibu wake na sisi tukabakia katika eneo moja tu la usajili wa hayo matukio ya kijamii.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Tunguu naye alikuwa na maoni ambayo baaadhi yake Mhe. Naibu Waziri ameshayatolea ufafanuzi. Lakini nataka niseme tuu lile linalohusiana na Waziri wa Utalii wa SMT. Nadhani Serikali tutakuwa tumelisikia na tunashukuru kwa kutupa taarifa hiyo lakini hili zaidi nataka nimwachie Waziri anayehusika na Sekta ya Utalii wakae na Waziri mwenzake ili waelewane kuhusu hili. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya utalii amelisikia na nadhani kwa *information* zaidi unaweza ukamfuata ukaenda kumpa *detail* ili na yeye akajua namna ya kuweza kulifanyia kazi. Kwa jumla sisi sote tuko Tanzania, Tanzania ina serikali mbili. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kama kuna jambo ambalo tunahisi haliko sawa basi nadhani utaratibu wetu ni kukaa tukashauriana mpaka hilo jambo likakaa sawa. Nina imani kubwa Mhe. Waziri wa Utalii, Mhe. Rashid Ali Juma hilo jambo analiweza, kwa hiyo tumuachie yeye alifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, muda wa kutangaza au muda wa kutumika sheria. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni utaratibu tu wa kutunga sheria, ziko sheria ambazo Mhe. Rais akishasaini

zinaanza kutumika, na ziko sheria ambazo mpaka waziri azitangaze kwenye Gazeti rasmi la Serikali. Ni kwa madhumuni yale yale yakutaka ile sheria iweze kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo, mimi naomba kifungu kilivyo tukiache hivyo, kwa sababu madhumuni yake ni yale aliyoyaeleza Mhe. Naibu Waziri kwamba sheria hii tunachotaka itekelezeke kwa umakini na uzuri zaidi kama vile alivyofafanua Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia juu ya suala la kuteua na kuzingatia suala zima la elimu, na hasa yeye alizungumzia katika maeneo yale ya usajili ndani ya Wilaya. Kwa kweli Sheria ya Utumishi ya Umma Nam.2 ya 2011 imeweka vigezo vya namna gani watumishi wanaweza wakateuliwa, na wameweka sifa. Na kama hao watumishi katika ngazi hizo tunazozisema za Wilaya tunataka wawe ni wasajili wa Wilaya lazima hivyo vigezo wavitimize kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nyengine yoyote ile hata kama itakuwa haikutaja, lakini kwa sababu watumishi hawa ni wa serikali na ni watumishi wa umma lazima wafate vigezo vile vile ambavyo vimeelezwa kule ndani ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Lakini nataka niwahakikishie watumishi waliopo ambao pengine hawana elimu inayolingana na sifa ambazo zitahitajika katika kuteuliwa, ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Uwakala itawapa fursa ya kujiendeleza na wakifuzu vigezo hivyo basi na wao watateuliwa. Lakini hatutawafukuza kazi wala kuwaachisha kazi kwa sababu tu hawana hivyo vigezo. Wataendelea kuwa ni watumishi wa umma na watafanya kazi ambazo watapangiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Uwakala wa Usajili. Kwa hiyo, nataka nikutoe hofu Mhe. Simai Mohammed Said kwamba hilo jambo serikali inalizingatia.

Mhe. Mwenyekiti, muda wa kupata cheti cha usajili nafikiri Mhe. Naibu Waziri ameshaueleza vizuri, kwamba tumekubali ushauri wako kuwa badala ya ule muda uliosema miezi mitatu au miezi sita, kwa sababu hili jambo ni jambo ambalo tunataka litekelezeke kwa ufanisi tumeweka angalau mwezi mmoja. Tumekubali kufanya marekebisho hayo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la usajili wa ndoa. Kwanza nataka wafahamu Waheshimiwa sisi tutahusika na kusajili ndoa zitakazofungwa Zanzibar, ziwe za wananchi wa Zanzibar, ziwe za wageni. Vifo vitakavyotokea Zanzibar viwe vya wageni, viwe vya wenyeji, lakini kwa wale Wazanzibari ambao watafunga ndoa nje ya nchi baadae tutakuja kuzitambua zile ndoa zao, na ile ndoa itasajiliwa kule atakakoifunga, lakini sisi hapa lazima tuje tuitambue. Kwa hiyo, sisi zaidi tunatambua zile ndoa na vifo au talaka na matukio mengine yote ya kijamii yale ambayo yatafanyika hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, upo utaratibu kwa mfano Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumzia suala la mtoto anapozaliwa pengine kwenye meli, meli inakwenda wapi. Nadhani kipo kifungu ambacho kinatoa ufafanuzi juu ya kutambua matukio ya kijamii yatakayotokea katika maeneo hayo kama meli, angani na kwengineko. Kwa hiyo, kwa kutambua hilo nadhani ule mchango wako serikali imeuzingatia katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwasilisha ripoti halitekelezeki. Nataka nikubaliane na mheshimiwa kwamba sisi lazima hatuwezi kuwa nje ya ile sheria ya fedha, madhali sheria ya fedha imeweka

masharti hayo na sheria nyengine yoyote inatakiwa itambue hilo. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe hili watukubalie.

Mhe. Mwenyekiti, jengine suala la uwakala kuongeza ada za usajili. Kwanza nataka nitambue au wajumbe watambue kwamba wakala sio shirika, wakala ni wakala wa serikali, kwa msingi huo ada zote zitakazostahiki kutozwa ni lazima zitashauriwa na bodi kwa waziri, na waziri atashauriana na Waziri wa Fedha. Na kama kuna mabadiliko yoyote yanatakiwa kufanyika basi waziri mwanzoni mwa mwaka atakuja hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi kufanya hayo marekebisho. Kwa hiyo, sidhani kama kutatokea uholela kiasi hicho ambacho kinaweza kikawaumiza wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji wa tatu alikuwa Mhe. Ali Suleima Ali, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kijitoupele. Kwanza nataka kwa niaba ya Mhe. Rais, hii ni Ofisi ya Rais pamoja na sisi watumishi tunaomsaidia Rais tunazipokea pongezi zake ambazo ametupa na tunashukuru kwa pongezi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu vizazi, kadi za utambulisho, ndoa, talaka, vifo ndio madhumuni ya kazi za uwakala huu. Kwa hiyo, tutajitahidi sana kusimamia taratibu na kwa nini tumefanya hivi? Serikali imeamua kuunganisha mifumo hii kuwa ni mfumo mmoja, kwa sababu tunataka kama ulivyoeleza mswada, tunataka toka siku mtu unazaliwa mpaka siku unafariki unaondoka duniani lazima rekodi zako ziwepo na tuwe tunazitambua. Kwa hiyo, lazima tujikite katika hiyo *core function* yetu ya usajili wa matukio ya kijamii. Kwa hiyo, haya yote uliyoyaeleza Mhe. Ali Suleiman Ali ndio madhumuni makubwa ya usajili na tutaufanya kwa umakini, na tutajitahidi sana au serikali imeandaa mkakati mzuri wa kuona kwamba hakuna ghushi katika maeneo haya ya usajili wa matukio ya kijamii. Umesema unakubaliana nao na mimi nakushukuru na ukikubali wewe najua na wananchi wa Kijitoupele wamekubali hiyo inatupa faraja sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mtoto aliyeokotwa atasajiliwa vipi? Nadhani pia sheria imesema utaratibu umewekwa vizuri kwa sababu taarifa za mtoto kama huyu, kama mtoto akizaliwa hospitali mtoa taarifa wa mwanzo anakuwa ni daktari. Kama mtoto akizaliwa mtaani mtoa taarifa wa mwanzo atakuwa ni sheha, na mtoto akiokotwa vile vile zipo taratibu ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria. Nakushukuru sana kwa kutukumbusha hilo ili tuweze kulifanyia kazi vizuri.

Pia umesisitiza juu ya kifungu cha 27(1), (2) (a, b na c) nadhani liko vizuri halina tatizo.

Kifungu cha 28(a) na (b) tupate kutoa ufafanuzi, nadhani umetaka ufafanuzi juu ya jambo hili, Naibu Waziri amejaribu sana kutoa ufafanuzi na nikuombe uridhie ule ufafanuzi ambao ametoa Mhe. Naibu Waziri.

Umerejea kusema kazi ya wakala ni usajili wa matukio ya kijamii, aina ya talaka tuzijue. Nadhani zipo talaka ambazo zinatolewa na mume mwenyewe na zipo talaka ambazo zinatolewa ama kwa Kadhi ama kwa njia nyengine kwa wale ambao hawana dini. Sasa hizo zote sisi kazi yetu ni kuzisajili, yale mambo mengine ya taratibu mpaka hiyo talaka ikipatikana hayo yatakuwa yapo kwa mujibu wa sheria nyengine ambazo zimezungumzia masuala hayo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi nakushukuru sana na wewe kwa mchango wako makini ambao umetukumbusha baadhi ya majukumu hasa lile la kutoa taaluma baada ya sheria hii kupitishwa na kuanza kutumika. Kwa sababu ni kweli sheria ambayo inakusanya mambo mengi inabadilisha mambo mengi inabidi lazima tutoe taaluma ya kutosha na kama alivyosema Naibu Waziri tutajitahidi sana kutoa taaluma ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, mswada umekuja wakati muafaka sisi tumeona hivyo kwamba mswada huu muda huu ni wakati muafaka kuuleta ndani ya Baraza lako tukufu. Lakini tunataka tukuhakikishie kwamba zile changamoto nyingi ambazo zimetokea katika sheria tulizonazo ambazo tunazifuta tumejitahidi sana kwenye sheria hii mpya zisijitokeze na katika utekelezaji pia tutajitahidi sana kwamba zile changamoto zisijitokeze.

Wakala wa Usajili ni muarubaini pengine unaweza ukatoa changamoto zote na mimi nakubaliana na wewe na ndio maana tumeuleta. Kuna changamoto nyingi ambazo tumezibaini nadhani tutazitatua kutokana na kupitishwa kwa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ambayo umeyasema kama nilivyosema mwanzo kamati imeyazingatia sana. Muda wa bodi na muda wa wajumbe wa bodi unataka isomeke “muda wa wajumbe wa bodi”.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani bodi ni wajumbe kwa hiyo na muda wa bodi, nadhani muda wa Mwenyekiti ni miaka minne badala ya miaka mitatu, na wajumbe nafikiri muda wao ulitaka tu isomeke muda wa wajumbe wa bodi badala ya muda wa bodi. Hilo halina tatizo tunakubaliana nalo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mafao ya wajumbe umezungumzia pia hili, na pia alilizungumzia Mhe. Hassan Khamis Hafidh, hilo tumelifanyia marekebisho.

Nia ya serikali kwa wajumbe wote wa bodi zote sio kama ilivyokuwa mwanzo kwamba bodi zinaweza zikajiamulia mafao yao na ikawa ndio imetosha hapana. Bodi zote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma wanatakiwa wapendekeze kwa waziri na waziri lazima afate taratibu zile za kisheria ili kuweza kuidhinisha baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, lile alilosema Mhe. Hassan la kwamba je mafao yao yatakuwa sawa sawa na waziri? Hapana, isipokuwa yanakwenda kwa waziri ili kuhakikisha kwamba yale maamuzi yao ya bodi kwanza yamefata sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini pili yanafata taratibu za fedha namna ya kuweza kulipana na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine amelizungumzia suala la Naibu Mkurugenzi Mkuu na masharti yale. Kama nilivyosema mwanzo, Sheria ya Utumishi wa Umma inatambua ili uteuliwe kukamata nafasi za Ofisa Mwandamizi ni lazima uwe *Senior Civil Servant* angalau uwe umefanya kazi sio chini ya miaka 10 ndipo hapo unaweza ukawa *Senior Civil Servant* kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Sasa sisi hatuwezi kwenda *against* na Sheria ya Utumishi wa Umma, lazima sheria mama ya utumishi wa umma kufuatia masuala yote ya kiutumishi lazima tuifate ile, na ndio maana tumeweka kiwango hiki cha miaka 10 kwamba tufuate ile sheria na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tubakie na muda ambao upo, na sifa za kielimu takriban sifa za kielimu unapoteuliwa kuwa Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi Mkuu *almost* sifa ni sawa ni zile zile. Isipokuwa tunakubaliana na lile pendekezo la Mhe. Mohammed Said Mohammed kwamba miongoni mwa sifa mbali ya zile kuwa na *degree* ya sheria, utawala, fedha tunaweza tukaweka na hiyo *degree* ya ustawi wa jamii yoyote kati ya hiyo ukiwa nayo na uzoefu wa miaka kumi Mhe. Rais anaweza akakupa nafasi ya kutumikia chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Rashid Makame Shamsi nimefafanua baadhi ya mambo mengi ambayo umeyasema.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) ndugu yangu nimesema la kwanza ame-*quote* kifungu cha 88(a) cha Katiba ya Zanzibar sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna wajibu gani? Mimi nalitambua hilo kwa sababu na mimi ni mwakilishi wa wananchi na siogopi kujisifia kwamba sasa hivi ni kipindi changu cha tano nachaguliwa na wananchi. Na nimekuwa *backbencher* kwa kipindi cha miaka 15, na mimi nimekua nikiikosoa serikali kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni za Baraza la Wawakilishi wakati nikiwa *backbencher* Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi niliyechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Tumbatu.

Kwa hiyo, siwezi kumuona mwenzangu kituko akiikosoa, akiishauri au akitoa mapendekezo kwenye serikali. Kwa hiyo, daima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuheshimu misingi ya Katiba, sheria na Kanuni na miongozo mengine yoyote ambayo ipo kwa mujibu wa utaratibu. Kwa hiyo, nataka nimtoe hofu Mhe. Mohammed Said Mohammed juu ya jambo hili, kwamba serikali hii ni serikali ya watu iliyochaguliwa na watu na itafanya kazi kwa maslahi ya watu. Na kwa kuonesha hilo ameleta jadweli la mapendekezo ya sheria hii na mimi nataka nimuoneshe kwamba serikali hii inatambua hilo. Isipokuwa kama nilivyosema mwanzo yapo maeneo itabidi *give and take* mengine atukubalie kwamba yasiwe kama vile alivyopendekeza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe alikuja na marekebisho ya kifungu cha 5(1)(g) ambacho amependekeza kifutwe kwa madhumuni ya kumtoa Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA* asiwe Mjumbe wa Bodi ya Ushauri. Ufafanuzi nadhani nimeshautoa kwa madhumuni gani tumemuweka Mkurugenzi wa *NIDA* kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri. Nadhani atukubalie kwamba Mkurugenzi wa *NIDA* aendelee kubaki kuwa ni Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa sababu zile ambazo nimezisema na kwenye *hansard* zitakuwa zimebakia.

Pia ametushauri tumuongeze Mjumbe wa Mufti. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba sheria hii ni Sheria ya Usajili wa Matukio ya Kijamii. Kwa msingi huo itawasajili Waislamu, itawasajili wasiokuwa Waislamu na itawasajili wasiokuwa na dini. Kwa hiyo, mimi nadhani sheria hii tusingependa kumuweka kiongozi yeyote, wa dini yoyote ndani ya bodi hii, isipokuwa kwa sababu sheria hii inasajili yale matukio zile taratibu nyengine zitafanyika kwa mujibu wa sheria zilizotungwa kama Ofisi ya Mufti na hasa hii ni kwa mujibu wa ile sheria ya kadhi. Maana yake humu inasajili ndoa na talaka, sasa kwenye ile sheria ya Waisilamu inasemaje tuibakishe sheria inavyosema, lakini nimuombe Mhe. Mohamed Said Mohamed mtu kutoka Mufti tusimuingize katika sheria hii.

Vile vile ameshauri kifungu cha 8 kuongezwa vifungu vidogo vya 8(5) na 8(6). Nakubaliana na mapendekezo yake ambayo ameyatoa. Nataka nirejee, kwa sababu serikali hii sikivu nataka nikubaliane na mapendekezo yake yote mawili ambayo ameyatoa. Kwa hiyo vinaongezwa vifungu vingine vidogo viwili, kifungu cha (5) na kifungu cha (6). Hayo mapendekezo tunakubaliana nayo.

Kifungu cha 11(2) inashauriwa kuongeza fani ifuatayo. Nimeshasema kuongeza fani nayo tumekubaliana nayo kwamba tuongeze pia na fani ya ustawi wa jamii haina neno tunaiongeza.

Kifungu cha 12(2) kinarekebishwa kama ifuatavyo mapendekezo yao. Kama nilivyosema *almost* sifa za Mkurugenzi Mtendaji na Naibu Mkurugenzi Mtendaji ni zile zile. Kwa hiyo, kuzitaja na kutokuzitaja kwa sababu kwenye sheria hii imetajwa zile za Mkurugenzi Mkuu Mtendaji na kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma nani anatakiwa awe mteuzi au ateuliwe na Rais sifa zake ni zipi zimeelezwa nadhani tutafuata sheria ile ili kuweka sifa za Naibu Mkurugenzi Mtendaji, na kwa sababu zinalingana na zile za Mkurugenzi Mtendaji.

Pia amependekeza kifungu cha 21(7) anashauri kuongeza kifungu kidogo kipya kitakachotoa nafasi ya kukata rufaa kwa mtu aliyekataliwa kupata huduma kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji. Nacho hiki nakubaliana naye kwamba, mtu akikosa haki kwa Mkurugenzi Mtendaji anayo haki ya ku-*appeal* kwa waziri anayehusika na masuala ya matukio ya kijamii na kwa utaratibu wa nchi yetu mtu huyo asiporidhika kwa hiyo, nakubali kwamba kuongeza kipengele cha kwamba asiporidhika na maamuzi ya Mkurugenzi Mtendaji basi atakata rufaa kwa waziri anayehusika na masuala ya usajili wa matukio ya kijamii, kama hakuridhika na hayo maana yake katiba yetu na sheria ziko wazi kwamba atakwenda kwenye Mahakama Kuu kukata rufaa na anaweza akapata ufafanuzi wa jambo hilo.

Kwa hiyo, utaratibu wa rufaa umeelezwa kwa mujibu wa sheria isipokuwa tumeongeza tu hili suala la kwamba asiporidhika kwa Mkurugenzi Mtendaji anayo haki ya kukata rufaa kwa Mhe. Waziri, kama ilivyo katika sheria yetu ambayo tunaikuta sasa ya vitambulisho kwamba mtu asiporidhika na haki atakayopata kule kwa Mkurugenzi anatakiwa aje kwa waziri na asiporidhika hapo anatakiwa aende Mahakamani. Ahsante sana.

Kifungu cha 23(2)(a) kinarekebishwa, ametoa marekebisho jina la mtoto, jinsia. Mimi nadhani hapa nimwambie Mhe. Mohamed Said liwe kama vile tulivyosema kule mwanzo, kuna taasisi ambazo zimeshawekwa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Kwa mfano, suala la ulemavu, unaposajiliwa unaweza ukawa mlemavu unapozaliwa, unaweza usiwe mlemavu na unaweza ukaja ukapata ulemavu baadae. Kwa hivyo, ningeshauri kifungu hiki kikabakia kwa mujibu wa ile sheria ya watu wenye ulemavu ambayo inawapa fursa pana zaidi ya kuweza kuwasajili, isipokuwa sisi kama ni watu tunaosajili matukio ya kijamii tutakuwa tuna-*share* nao katika kupata taarifa pale inapohitajika na taarifa hizi kwa sababu zipo pia kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Mtakwimu Mkuu pia ni Mjumbe wa Bodi ya Ushauri nadhani jambo hili linaratibiwa vizuri sana na serikali kwa sheria nyengine ambazo zipo hivi sasa.

Vile vile alitoa ushauri kwenye kifungu cha 40, alishauri kuongeza kifungu kidogo kipya kitachosomeka kama ifuatavyo: "Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki suala la

talaka ambalo maamuzi yake yanatolewa katika Mahakama, Mkurugenzi Mtendaji atatakiwa kujiridhisha kwa Mahakama imefikia mwisho katika kusikiliza dai linalohusiana na talaka".

Kwenye kifungu cha 38 jambo hili limeelezwa vizuri sana. Kwa hiyo ningemuomba tukabaki na kifungu cha 38 ambalo linampa majukumu Mkurugenzi Mtendaji kuweza kusajili matukio haya katika eneo hili la talaka. Kwa hiyo hakuna haja ya kuongeza vitu vingine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumalizana na Mhe. Mohamed Said Mohamed sasa pia nataka nitoe ufafanuzi kuhusu hoja za Mhe. Said Soud Said (MBM) ambazo amezitoa.

Mheshimiwa kwanza nataka nikubaliane na yale yote ambayo ameyasema Mhe. Said Soud Said (MBM), mteuliwa wa Jimbo la Ikulu kwa mchango wake ambao ameutoa. Ni sahihi Mheshimiwa kwamba ilani inayotekelezwa sasa hivi uwe umetoka popote pale, uwe umeingia kwa utaratibu wowote ule, uwe umetoka Chama cha Wakulima, uwe umetoka *TADEA*, uwe umetoka *ADC*, lakini unatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hakuna mbadala wa hilo na sisi sote tunatambua hilo. Kwa hiyo, nampongeza sana na nawashukuru sana mawaziri wasiokuwa na wizara maalum kwa kulitambua hilo kwamba wapo kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na sio chama chengine. Na ule ushauri aliopewa na ndugu yangu Mhe. Hassan Khamis Hafidh anaweza akaupokea akiukubali sisi tuko tayari kukupokea. (*Makofi*)

Kwa hiyo namshukuru sana Mhe. Said Soud Said (MBM) kwa mchango wake na vile vile kwa kuona mchango mkubwa ambao anaufanya au anautoa Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein wa kuiendeleza nchi yetu katika nyanja mbali mbali, ndio maana kila Baraza la Wawakilishi serikali hii haikosi kazi ya kufanya ya kuleta sheria mbali mbali kwa madhumuni ya kujenga utawala bora ndani ya nchi yetu, ili shughuli ziweze kutekelezeka kwa ufanisi na kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Kwa hiyo namshukuru sana. *(Makofi)*

Mchangiaji mwengine alikuwa Mhe. Hassan Khamis Hafidh mtoto wa wakwezi na wakulima, mwana Mapinduzi na mimi nakubaliana naye kwamba mswada huu ni wa Kimapinduzi kwa sababu unalenga kuenzi na kulinda Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Kwa hiyo sisi tunaotumikia serikali hii ni lazima tutambue hilo na hatutafanya vyenginevyo na amekuwa na hofu kwa sababu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nadhani limeelezwa vizuri sana ndani ya katiba na hata hao walipokuwepo walitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, huyo Rais ambaye atakuja kuteuwa wengine nje ya watu kama mimi kwani mna tamaa atakuja lini, na-*pause question* kwenu mnatamaa atakuja lini? Kwa sababu Chama cha Mapinduzi kinatekeleza ilani na inawafanyia mambo mema wananchi, CCM itaendelea kushinda tu, hata Mhe. Said Soud Said (MBM) na Mhe. Juma Ali Khatib (MBM) wanalielewa hilo. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mhe. Hassan Khamis kwamba mambo yataendelea kusimamiwa na Chama cha Mapinduzi na yataendelea kusimamiwa kwa mujibu wa ilani iliyorithiwa ya Afro Shirazi ya kuwatumikia wananchi wanyonge wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Bodi ya Ushauri anashauri iwe Bodi ya Usimamizi. Naomba Mhe. Hassan anilikubalie kwamba bodi iendelee kuwa Bodi ya Ushauri kumshauri waziri, ikimshauri waziri maana yake inaishauri serikali, usimamizi wa jumla ubakie kwa waziri ambaye amepewa nafasi ya Mhe. Rais amsaidie

kusimamia taasisi zote ambazo zitakuwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.

Pia alikuwa na hofu na maposho, nafikiri nimeshatoa ufafanuzi kwamba maposho yao hayawezi kulingana na yale ambayo ameyafikiria yeye, isipokuwa kimewekwa kifungu cha kwamba wakishaamua na kupendekeza walete kwa waziri na waziri ashauriane na Waziri wa Fedha na Mipango kwa misingi ile niliyoisema kwamba zaidi waziri tunaangalia sera zetu na maamuzi yetu na kwa mujibu wa bajeti, na kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma inasema nini juu ya mafao ya watumishi, Wajumbe wa Bodi na viongozi wengine. Ni hilo tu, kwamba hatutaki kutoa fursa kwa bodi yoyote kufanya maamuzi ambayo yanaweza yakenda nje ya sera za serikali na sheria za fedha ndio maana tumeweka utaratibu huu. Kwa hiyo, lile ambalo amelisema asiwe na wasiwasi nalo nadhani halikukusudiwa hivyo, lengo ni kuhakikisha kwamba bodi inaleta ushauri na serikali iweze kukubali ama kukataa kutokana na sera au sheria na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Suala la kukasimu madaraka. Hawa zaidi tunazungumzia wale wasajili wa wilaya ambao watakuwa wamefuata taratibu zote za kiserikali pale ambapo watakuwa wameteuliwa, watakuwa wamefanyiwa *vetting* ya kutosha mpaka tuhakikishe kwamba unakuwa msajili wa wilaya na huyu atafanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji zile ambazo atakasimiwa kuzitenda. Lakini asiwe na wasiwasi kutokana na mfumo ambao tunauanzisha nadhani mkurugenzi atakuwa na taarifa za moja kwa moja kwa yale mambo ambayo yatafanyika kule wilayani na hakuna kosa lolote lile ambalo litafanywa na mtu mwengine yeyote bila ya Mkurugenzi Mtendaji kuelewa kinachofanyika.

Mheshimiwa mengi aliyoyasema nilianza kuyatolea ufafanuzi mwanzo na mwisho kabisa alichangia Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na yeye alitoa mchango wake kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja. Natambua mchango wake na namshukuru sana kwa msaada mkubwa ambao ameufanya wa kuweza kunisaidia kutoa ufafanuzi wa michango ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Baada ya kwisha kusema hayo sasa naomba kutoa hoja ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yako. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wajumbe wamejadili Mswada wa Sheria wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, sasa naomba Baraza lako likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitisha kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ya Mwaka 2017

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa wakala pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4 Kazi za Wakala pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Utawala wa Wakala

Kifungu 5 Bodi ya Ushauri pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Kazi za bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 Muda wa bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Mikutano ya bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Maamuzi ya bodi
Kifungu 10 Posho kwa wajumbe
Kifungu 11 Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Naibu Mkurugenzi Mtendaji
Kifungu 13 Kazi za Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15 Kukasimiwa kwa baadhi ya kazi
Kifungu 16 Idara na vitengo vya wakala
Kifungu 17 Uteuzi na sifa za ofisa wa usajili pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18 Wafanyakazi wa wakala pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Usajili wa Matukio ya Kijamii

Kifungu 19 Usajili wa matukio ya kijamii ni lazima pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 Usajili wa vizazi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Usajili wa vizazi pamoja na marekebisho yake

Kifungu 22

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu namba 22(i)c wakati nachangia nilizungumzia juu ya hofu yangu kwenye namba (c) mtu mwenye dhamana ya mtoto hapa neno "na" nilishauri liondoke lije "au". Sasa kidogo Mwanasheria Mkuu atusaidie hapa baina ya hili neno "na" na "au". Kwa sababu "and", "and" "or" sasa Mhe. Waziri alipokuja nahisi hakulitaja naona kama hili linajumuisha wote kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, hii "na" sidhani kama ina mashaka katika uandishi wa kisheria maana yake kinachooneshwa hapa ni kwamba kuna jengine linafuata chini. Sasa wasiwasi wake yeye nini labda angetueleza mashaka yake, lakini sidhani kama kuna matatizo katika kuweka kitu "na" hapa. Kwa sababu kinachoonesha kwamba kuna kitu chengine kinafuata nadhani ndio madhumuni yenyewe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, kama utaweka "na" ina maana hapo mtoto kizazi kitachozaliwa hicho mtoto ambaye anazungumziwa ili taarifa ziende itabidi iwe baba au mama mmiliki wa hiyo nyumba mtu dhamana na huyo mtoto na mtu aliemuokota wote wende kwa pamoja. Sasa inabidi waangalie kwamba yupi na yupi katika hawa wanne. Sasa ukisema "na" ina maana makundi yote manne itabidi yatoke yende kutoa taarifa. Sasa hapo inatakiwa iingie "au"*which is and* kwa "na", "or" kwa "au". Sasa labda Mwanasheria Mkuu atusaidie hapo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Simai Mohamed Said ya kifungu cha 22(i)(c) mtu mwenye dhamana ya mtoto "na"aliyemuokoa mtoto *of course* ushauri wake yeye anasema tuondoe "na" tuweke "au". Sasa inategemea tafsiri yake hiyo "au" inaingia kwa huyu wa chini au "au" inaingia kwa wote waliokuja kutoka juu. Uandishi ulioandikwa hapa ni kama "na" inajumuisha na hawa ambao pia wanakuja kutoka chini. Kwa hiyo, mimi nadhani kiuandishi haina matatizo iko sawa sawa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohamed Said: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Simai Mohamed Said.

Kifungu 22 Wajibu wa kutoa taarifa ya kizazi
Kifungu 23 Namna ya kusajili vizazi
Kifungu 24 Usajili wa mtoto alieokotwa
Kifungu 25 Kubadilisha jina la mtoto
Kifungu 26 Kutoa cheti za kuzaliwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27 *Register* ya utambulisho pamoja na marekebisho yake
Kifungu 28 Aina za kadi ya utambulisho
Kifungu 29 Kutoa kadi za utambulisho
Kifungu 30 Wajibu wa kutumia jina pamoja na marekebisho yake
Kifungu 31 Kutunza na Usalama wa kadi ya Utambulisho pamoja na marekebisho yake
Kifungu 32 Ulazima wa Matumizi wa Kadi za Utambulisho
Kifungu 33 *Register* la ndoa pamoja na marekebisho yake

Kifungu 34 Tangaza la ndoa
Kifungu 35 Usajili wa ndoa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 36 Kutoa cheti za ndoa
Kifungu 37 *Register* la talaka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 38 Tangazo la talaka
Kifungu 39 Usajili wa talaka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 40 Kutoa cheti cha talaka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 41 Talaka rejea kusajiliwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 42 *Register* la vifo
Kifungu 43 Usajili wa vifo
Kifungu 44 Wajibu wa kutoa raaifa za vifo pamoja na marekebisho yake
Kifungi 45 Kutoa vyeti vya kifo
Kifungu 46 Fedha za Wakala
Kifungu 47 Bajeti
Kifungu 48 Ukaguzi wa Hesabu
Kifungu 49 Kufuta usajili
Kifungu 50

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia nilionesha wasi wasi wangu na nikanukuu Katiba ibara ya 9(3). Ibara ya 9(3) ya Katiba Mhe. Mwenyekiti, inasema:-

> "Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa"

Nikatafsiri Umoja wa Kitaifa kwamba Mfumo wa vyama vingi na nikatafsiri Hizbu ni nani na nilisema Mhe. Mwenyekiti, kwamba Hizbu ni yule mtu yoyote asiyeyathamini Mapinduzi na kuyatambua Mapinduzi"

Nikasema Mhe. Mwenyekiti, wizara hii, hii Taasisi inayoshughulikia vyeti za kuzaliwa kwa kusikia kwangu ilikuwa serikali iliyopita ilikuwa inamilikiwa na wizara inayoongozwa na Hizbu na nasikia vyeti za kuzaliwa vikitoka kama njugu kwa simu tu ulikuwa unapata cheti cha kuzaliwa ili watu waweze kutengeza kadi za Uzanzibari kwa dhumuni la kupigia kura. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukitizama 50(3) naomba niisome:-

> "Mtu mbali na wizara, Idara au Wakala wa Serikali inaweza kupata matumizi ya taarifa ndani ya *register* kulingana na kanuni zitakazotolewa na waziri"

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kusema hivi nashukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba leo waziri tulienae anaeshughulika na mambo haya ni Waziri wa sisi Chama Tawala Chama Dume. Lakini Katiba hii inaruhusu Hizbu awe waziri. Sasa je, tukifata kama tulikotoka nyuma waziri akawa wa Hizbu akaanza kuvitoa hivi vyeti kama kwa simu tu kama ilivyokuwa tunavipata itakuwaje.

Sasa ombi langu Mhe. Waziri asiwe na mamlaka ya kutunga kanuni, atunge kanuni azilete katika Kamati za Baraza ya Wawakilishi halafu ziletwe Barazani zipitishwe asimalize yeye, kama yule Waziri wa Hizbu ndio tutarudi kule kule na madhumini makubwa ya kutunga sheria hii leo

kuwazuia Hizbu wasitufanyie vituko kama walivyotufanyia. Sasa kama leo tunakwenda kutunga sheria Mhe. Mwenyekiti, sheria hiyo hiyo, tunaiwacha wazi itakuwa hatujafanya kazi.

Naomba sana Waziri azitunge kanuni ziende kunako kamati halafu zije Barazani tuzijadili na tuzipitishe kwa nini kwa sababu kama waziri ni Hizbu humu Barazani mtakuwawengine si Hizbu hatutomwachia Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hassan Khamis Hafidh lakini Mhe. Waziri kifungu hichi alikitolea ufafanuzi. Bahati nzuri niseme au bahati mbaya niseme ulikuwa humo humu ndani labda kwa kukupa nafasi tu ya upendeleo nimpe Mhe. Waziri akueleze kwa faida yako. Lakini tayari alikuwa ameshaeleza.

Taarifa

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, taaifa. Ni kweli nilikuwa simo lakini nimemsikia yote na naweza kuyanukuu kwa sababu nilikuwa namuangalia nilichokijibu na nimemsikia alichokijibu na *hansard* zipo. Kwa maana hiyo na mimi natumia kanuni kwamba nina hali ya kupiga buti na nafikiri kinafahamika nilichokieleza. Mimi sishindani mimi natoa changu tu kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi laa unahisi wewe sawa tunavyokwenda *Bismilahi* twende mimi sina tatizo.

Lakini kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi niliechaguliwa na wana Mapinduzi kuwalinda na kuwatetea ndani ya Baraza hili na hili naliona si sawa nina haki ya kuyasema hayo na nayasema hadharani. Kwamba kama tunaendelea kufanya hivi itakuwa bado tunatoa nafasi kwa Hizbu kutaka kutufanyia hivyo. Kwa nini kwa sababu sheria, Katiba inaruhusu na wizara hii ameshawahi kuwa nayo Hizbu na vyeti vilikuwa vinatoka vingi. Kwa maana hiyo tulinde leo ili kesho isije ikatokeza haya. Mimi sina tatizo kama unahisi sawa na waziri nae yuko sawa *Bismilahi*. Lakini tujue Mapinduzi Matukufu itakuwa hatujayalinda kwa namna hii. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hassan Khamis Hafidh lakini bado nabakia kukwambia kuwa tayari hoja yako imeshatolewa ufafanuzi. Naomba tuendelee katibu. (*Makofi*)

Kifungu 50 Matumizi ya *Register*
Kifungu 51 Ada ya Usajili
Kifungu 52 Kurejesha cheti au Kitambulisho pamoja na marekebisho yake
Kifungu 53 Makosa na adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 54 Adhabu ya jumla pamoja na marekebisho yake
Kifungu 55 Kanuni
Kifungu 56 Kufutwa kwa Sheria na Hifadhi ya Sheria

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa

kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali mswada huu naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, sasa naomba niwahoji. Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matokeo ya Kijamii Zanzibar na kuweka Vifungu vya Usajili na mambo mengine yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. Lakini kabla ya kuahirisha kikao hichi naomba na mimi nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Mhe. Waziri wake wote nawapongeza.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha naomba nitoe tangazo ambalo tunaambiwa kuwa Tume ya Maadili watakuja tarehe 13 kwa kukusanya zile fomu za maadili wakati na saa za kazi.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa utulivu wenu na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kupitisha sheria hii. Naomba kuakhirisha mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:37 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 12/12/2017 saa 3:00 asubuhi)